CHUO KIKUU CHA EGERTON

IDARA YA LUGHA NA ISIMU

TASNIFU YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA

SHAHADA YA M.A. (KISWAHILI STUDIES)

# "MBINU ZA KIMAIGIZO KATIKA TUNGO ZA ABDILATIF ABDALLA"

NA

ISSA YUSUF MWAMZANDI

X

EULIB

063657

LIBRARY

Septemba, 1996

UNGAMO

"TASNIFU HII NI KAZI YANGU MWENYEWE NA HAIJATOLEWA KWA MAHITAJI YA DIGRII KATIKA CHUO KINGINE CHOCHOTE"

Mwamzandi

Mwamzandi, I.Y.

8/10/96

Tarehe

"TASNIFU HII IMETOLEWA KUTAHINIWA KWA IDHINI YANGU KAMA MSIMAMIZI WA KAZI HII WA CHUO KIKUU"

Profesa Rocha M. Chimerah

8.10.96

Tarehe

HIFADHI YA HAKI ZA UCHAPISHAJI

'Hairuhusiwi kunakili sehemu yoyote ya tasnifu hii kwa njia ya kanda, maandishi au kuhifadhi kwa namna yoyote bila ya idhini kutoka kwa mwandishi au chuo kikuu cha Egerton kwa niaba yake'

## MUHTASARI

Kazi hii inahusiana na matumizi ya mbinu za kimaigizo katika tungo za Abdilatif Abdalla. Tungo zilizoshughulikiwa katika utafiti huu ni pamoja na Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa (1971), na mashairi yake 'Mnazi Vuta N'Kuvute', 'Kutendana' na 'Usiniuwe' - mashairi yanayopatikana katika kitabu chake Sauti ya Dhiki (1973). Swala kuu lililotafitiwa lina misingi yake katika hoja kwamba mwandishi wa kazi yoyote ya kifasihi, akiwemo Abdilatif, hunuia kuwasilisha ujumbe wake kwa nyenzo zitakazouwasilisha ujumbe huo kwa njia ya mvuto na inayonata kwenye bongo za wasomaji wake. Utafiti wetu, kwa kuzingatia hilo, uliangalia matumizi ya mbinu za kimaigizo alizotumia Abdilatif na jinsi mbinu hizo zilivyomwezesha kuuwasilisha ujumbe wake. Kwa kutumia mbinu hizo, mshairi huyu ameusahilisha usomaji wa tungo hizo kwa kumfanya msomaji wake azione tungo hizo zikitendeka kwenye jukwaa la akili yake.

Sura ya kwanza inashughulikia ujenzi wa somo la utafiti wa kazi hii. Somo hilo linahusiana na maigizo - ile nipa nikupe iliyopo kati ya waigizaji na hadhira au watazamaji wao kama asemavyo Elam 1980. Lakini sharti ifahamike kwamba utafiti wetu unayaangalia makala ya Abdilatif na wala si uigizwaji wa kazi yenyewe kwenye jukwaa. Hata hivyo, swala hili haliutingi usomaji wetu wa makala haya kimaigizo. Ndiposa tunawapata wahakiki mbalimbali kama vile Topan (1971) na Chacha (1992), waliowahi kuzisoma tungo hizi kutaja kutumika kwa mbinu za kimaigizo. Wataalam hawa, ingawa walitaja kutumika kwa mbinu hizo, hawakuzizamia kwa urefu.

Kama ilivyo ada ya kazi yoyote ya utafiti, ipo haja ya

kutumika kwa nadharia kabambe ambayo itakuwa mhimili wa hoja mbalimbali zitakazojadiliwa. Hili ni jambo ambalo linaandaliwa katika sura hii kupitia kwa nadharia ya semiotiki. Semiotiki kwa muhtasari ni sayansi ya ishara, hususani jinsi ishara hizo zinavyoubeba ule uwezo wa kuashiria. Abdilatif, kwa kutumia mbinu za kimaigizo katika kuiwasilisha kazi yake, ameingia katika uwanja wa matumizi ya ishara zinazoashiria jambo fulani. Kazi yake, mbali na kuwa ushairi, inahimiza isomwe upeo wa ushairi. Hili linawezekana kwa kuzitalii ishara za kimaigizo alizotumia. Maandishi ya wataalam wengine yanayohusiana na makala haya ya Abdilatif pia yanashughulikiwa katika sura hii ya kwanza. Pia tunaonyesha njia kuu za utafiti zilizotumika kuifanikisha kazi hii.

Kazi za mshairi huyu, kimsingi, ni ushairi. Ushairi umesifika kutokana na na lugha yake ya kufumbata dhana pevu kwa kutumia maneno machache. Hivyo basi, kueleweka kwa tungo hizi, kwa kiwango kikubwa, kunategemea kueleweka kwa lugha iliyotumika. Hili ni jukumu la kishairi katika lugha ambalo linatizamwa kwa mapana katika sura ya pili. Msisitizo kuhusu lugha ya kishairi kama mfumo wa mawasiliano unaojiashiria unaendelezwa. Mkazo kuhusu uashiriaji huo unaendelezwa sambamba na eneo letu la maigizo katika sura hii ya pili.

Sura ya tatu na nne ambazo ni upeo, na vilevile moyo wa tasnifu yetu, zinatuingiza katika kuziona mbinu zenyewe za kimaigizo. Sura ya tatu inashughulikia matini ya <u>Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa</u> ilhali sura ya nne inayazamia mashairi yaliyomo katika <u>Sauti ya Dhiki</u>. Mbinu mbalimbali alizotumia mshairi huyu wa kijukwaa zimetangulizwa na kuonyeshwa jinsi

zinavyodhihirika, hadi hadhira ikaweza kuyahisi maigizo yakitendeka kwenye jukwaa letu la akili.

Sura ya tano ni hitimisho la utafiti. Sura hii inatoa muhtasari wa masuala muhimu yaliyojitokeza katika utafiti wetu. Mshikamano wa mbinu mbalimbali za kimaigizo alizozitumia Abdilatif Abdalla, na jinsi mbinu hizo zinavyousisitiza uigizikaji wa tungo zake unafafanuliwa. Sura hii pia inatoa mapendekezo ya maeneo mengine yanayohitaji kufanyiwa utafiti.

## SHUKRANI

Shukrani zangu za dhati, kwanza, ziwaendee wasimamizi na walimu wangu. Hawa ni pamoja na Prof. Rocha Mzungu Chimerah, Mw. Onyango Ogolla na Mw. Furaha Chai. Ningependa kuwashukuru kwani ndio walionipa matumaini wakati mambo yalipokuwa mizonge mitupu. Kwangu wamekuwa nuru katika kiza, hadi polepole, upofu wangu ukaanza kujibari nami. Hawa ndio walioshuhudia yote ya kupanga na kupangua, tangu kazi hii ilipozaliwa, ikaanza kutambaa, ikasimama dede na hatimaye ikachanganya mwendo, mithili ya kitoto kichanga. Walimu hawa hawakuwa wasimamizi tu, bali ndugu wa nia.

Vilevile, ningependa kuwashukuru walimu wangu wa Idara ya Lugha na Isimu, Egerton. Hao ni Profesa Chacha, ambaye alinisaidia sana, sio kwa kunisomesha tu, bali pia kwa vifaa ambavyo vilinisaidia katika utafiti wangu. Hususani, sitasahau mwanga alionipa katika masuala ya nadharia za kiutafiti. Walimu Beja, Ntarangwi, Gituku, Mayaka, Kirigia, Muindi, Liguyani na walimu wengineo, wote nawashukuru.

Pia nawashukuru wanafunzi wenzangu Mohochi, E., Okindo, O., Buyonge, C., Mwanda, J. na Obiero, J.. Kadhalika ni Sheilah, W. ambaye alijinyima na kunitolea nakala za kazi yangu.

Ndugu Suleiman Mohammed, Biwwot na Mutahi, wa Kitivo cha Sanaa na Sayansi ya Jamii, Bernie na Jackline wa Idara ya Lugha na Isimu wanastahili heko kwa usaidizi wao.

Nikiwa katika shughuli zangu za kiutafiti, nilipata wasaa wa kukutana na baadhi ya watu ambao ni muhimu kuwataja. Walimu, Clara Momanyi, Yusuf Maitaria na Matti wa Chuo Kikuu cha Kenyatta walinifaa sana katika mahojiano yetu. Walimu Mwenda Mbatia na Kithaka wa Mberia, wa Chuo Kikuu cha Nairobi, ni aula kuwataja

kwa kuniruhusu kuipekua maktaba yao ya idara, na vilevile, ushauri wao juu ya maeneo mbalimbali ambayo yalihitaji kutafitiwa. Sitaweza kumsahau Mwalimu Mahiri Mwita, ambaye kabla ya kuja kwake Chuoni Egerton, alinizindua na baadhi ya mambo ambayo hayakunielea vyema. Ningependa kumshukuru mwanafunzi mwenzangu, Ndugu Marete, wa Chuo Kikuu cha Moi, kwa mjadala wetu uliofana sana. Bwana Nassoro 'Zoa' Mwamzandi, mwigizaji na mshairi maarufu pia alinifaa, hasa katika uwanja wa ushairi.

Shukrani za kipekee zimwendee ami yangu, Mhe. Kassim B. Mwamzandi, ambaye, nikiwa jijini Nairobi nilipata wasaa wa kujihifadhi nyumbani kwake.

Mwanarusi, daima sitamsahau kwa kunistahamilia na kunipa moyo wakati nilipokuwa nimejiinamia, nikijiuma vyanda bila ya kufahamu la kutenda. Ushauri wake ulinihamasisha, nikaona 'kumbe naweza'. Pamoja nawe, ni rafiki zetu Richard Mulwa na Lydia Mbula.

Mwisho ni shukrani kwa akraba zangu, Baba na Mamaangu, Kaka Bakari, Yunus, Zakaria, Muhammad, Twalib, Bahati na Idris. Dada zangu Fatma, Mwanamgeni, Saumu, Riziki, Mwanaulu na Mwanamisi.

# TABARUKU

Kwa wazazi wangu,

Mama Mwanasha

Pamwe Baba Yusufu.

walionilea,

tangu nikiwa mdogo.

wakanielimisha,

nikafika nilipofika.

## YALIYOMO


MUHTASARI . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . i
SHUKRANI . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . iv
TABARUKU . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . vi
YALIYOMO . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . vii
SURA YA KWANZA . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1
UTANGULIZI . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1
1.1. Kichocheo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1
1.2. Maelezo ya Istilahi . . . . . . . . . . . . . . . . 4
1.3. Mada ya utafiti . . . . . . . . . . . . . . . . . . 6
1.4. Makisio . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 8
1.5. Madhumuni ya utafiti . . . . . . . . . . . . . . . 8
1.6. Umuhimu wa utafiti . . . . . . . . . . . . . . . . 8
1.7. Upeo na mipaka ya utafiti . . . . . . . . . . . . . 9
1.8. Misingi ya nadharia . . . . . . . . . . . . . . . . 10
1.9. Mapitio ya maandishi . . . . . . . . . . . . . . . 15
1.10. Njia za utafiti . . . . . . . . . . . . . . . . . 21

SURA YA PILI . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 23

LUGHA KAMA MFUMO UNAOJIASHIRIA: JUKUMU LA KISHAIRI NA MAIGIZO KATIKA TUNGO ZA ABDILATIF . . . . . . . . . . . 23
2.1. Utangulizi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 23
2.2. Umuhimu wa Lugha katika Ushairi . . . . . . . . . . 23
2.3. Semiotiki ya Ushairi . . . . . . . . . . . . . . . 25
2.4. Jukumu la Kishairi na Maigizo katika Tungo . . . 27
2.4.1. Lugha ya Kishairi na Maigizo katika Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa . . . . . . . 28
2.4.1.1. Taswira . . . . . . . . . . . . . . 29
2.4.1.2. Sitiari na Tashbihi . . . . . . . . 32
2.4.1.3. Metunumia . . . . . . . . . . . . . 35
2.4.1.4. Takriri . . . . . . . . . . . . . . 36
2.4.1.4.1. Takriri Vina . . . . . . . 37
2.4.1.4.2. Takriri Neno . . . . . . . 37
2.4.1.5. Uteuzi wa Maneno katika Mishororo . . . . . . . . . . . 38
2.1.4.6. Mpangilio wa Maneno katika Mishororo . . . . . . . . . . . 39
2.4.2. Lugha ya Kishairi na Maigizo katika 'Kutendana' . . . . . . . . . . . . . . 40
2.4.2.1. Taswira . . . . . . . . . . . . . . 40
2.4.2.2. Sitiari . . . . . . . . . . . . . . 42
2.4.2.3. Takriri . . . . . . . . . . . . . . 43
2.4.2.3.1. Takriri Neno . . . . . . . 43
2.4.2.3.2. Takriri Kibwagizo . . . . 44
2.4.2.4. Mahadhi (Ridhimu) . . . . . . . . . 45
2.4.3. Lugha ya Kishairi na Maigizo katika 'Mnazi: Vuta N'kuvute' . . . . . . . . . 46
2.4.3.1. Nafasi ya Tashibihi . . . . . . . . 46
2.4.3.2. Sitiari . . . . . . . . . . . . . . 49
2.4.3.3. Methali na Misemo . . . . . . . . . 51
2.4.4. Lugha ya Kishairi na Maigizo katika 'Usiniuwe' . . . . . . . . . . . . . . . 52
2.4.4.1. Nafasi ya Taswira . . . . . . . . . 52
2.4.4.2. Tashihisi . . . . . . . . . . . . . 53




UNIVERSITY LIBRARY

2.4.4.3. Takriri Neno . . . . . . . . . . 55
2.4.4.4. Mahadhi (Ridhimu) . . . . . . . 55
2.5. Kimalizio . . . . . . . . . . . . . . . . 56

SURA YA TATU . . . . . . . . . . . . . . . . . 57

MBINU ZA KIMAIGIZO KATIKA UTENZI WA MAISHA YA ADAMU NA HAWAA . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 57
3.1. Utangulizi . . . . . . . . . . . . . . . 57
3.2. Lugha ya Kimaigizo katika Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa . . . . . . . . . . . . . 58
3.3. Kaida za Kimaigizo . . . . . . . . . . . 62
3.3.1. Kaida za Kimaigizo katika Utenzi . . . . 62
3.3.2. Msimulizi . . . . . . . . . . . . 62
3.3.3. Lugha ya Kishairi . . . . . . . . . 64
3.4. Ploti . . . . . . . . . . . . . . . . . 64
3.4.1. Ploti katika Maigizo ya Utenzi . . . . . 65
3.5. Kitendo . . . . . . . . . . . . . . . . 69
3.5.1. Kitendo katika Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa . . . . . . . . . . . . . . . 70
3.5.1.1. Kitendo katika Faslu ya Kwanza na ya Pili . . . . . . . . . . . . 71
3.5.1.2. Faslu ya Tatu . . . . . . . . . 73
3.5.1.2.1. Adamu na Hawaa . . . . . . 73
3.5.1.2.2. Hawaa na Ibilisi . . . . . 76
3.5.1.3. Faslu ya Nne: Adamu na Hawaa Tena 77
3.5.1.4. Faslu ya Tano na ya Sita . . . . 81
3.5.1.4.1. 'Adamu na Hawaa Duniani' . 81
3.5.1.4.2. 'Uzazi' . . . . . . . . 83
3.6. Wahusika . . . . . . . . . . . . . . . . 84
3.6.1. Utangulizi . . . . . . . . . . . . 84
3.6.2. Kudhihirishwa kwa wahusika katika utungo 85
3.6.3. Wahusika katika Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa . . . . . . . . . . . . . . . 87
3.6.3.1. Msimulizi . . . . . . . . . . . 87
3.6.3.2. Adamu . . . . . . . . . . . . . . 90
3.6.3.3. Ibilisi . . . . . . . . . . . . . 95
3.6.3.4. Hawaa . . . . . . . . . . . . . . 99
3.5.3.5. Kabili na Habili . . . . . . . . 103
3.6.3.5.1. Kabili . . . . . . . . . 104
3.6.3.5.2. Habili . . . . . . . . . 105
3.7. Mandhari . . . . . . . . . . . . . . . . 106
3.7.1. Utangulizi . . . . . . . . . . . . . 106
3.7.2. Mandhari katika Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa . . . . . . . . . . . . . . . 107
3.7.2.1. Mandhari ya Mbinguni na Peponi . 108
3.7.2.1.2. Mandhari ya mti . . . . . 110
3.7.2.2. Mandhari ya Duniani . . . . . . 112
3.8. Kinaya Drama . . . . . . . . . . . . . . 113

SURA YA NNE . . . . . . . . . . . . . . . . . 116

MBINU ZA KIMAIGIZO KATIKA 'KUTENDANA', 'MNAZI: VUTA N'KUVUTE' NA 'USINIUWE' . . . . . . . . . . . . . 116
4.1. Utangulizi . . . . . . . . . . . . . . . 116
4.2. Lugha ya Kimaigizo katika Tungo . . . . . . . 116

4.3. Kaida za Kimaigizo . . . . . . . . . . . . . . . 119
4.3.1. Maelezo . . . . . . . . . . . . . . . . . . 119
4.3.2. Mnong'ono kwa msomaji . . . . . . . . . 123
4.3.3. Uzungumzi Nafsia na Uhusika Bubu . . . . 124
4.4. Ploti . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 125
4.4.1. Ploti katika 'Kutendana' . . . . . . . . 125
4.4.2. Ploti katika 'Mnazi: Vuta N'kuvute' . 131
4.4.3. Ploti katika 'Usiniuwe' . . . . . . . . 133
4.5. Kitendo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 135
4.5.1. Kitendo katika 'Kutendana' . . . . . . . 135
4.5.2. Kitendo katika 'Mnazi: Vuta N'Kuvute' . 140
4.5.3. Kitendo katika 'Usiniuwe' . . . . . . . 143
4.6. Wahusika . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 146
4.6.1. Wahusika katika 'Kutendana' . . . . . . 146
4.6.1.1. Mwanamke . . . . . . . . . . . . 147
4.6.1.2. Mwanamume . . . . . . . . . . . . 151
4.6.2. Wahusika katika 'Mnazi Vuta N'kuvute' 153
4.6.2.1. Alii . . . . . . . . . . . . . . 154
4.6.2.2. Badi . . . . . . . . . . . . . . 157
4.6.3. Wahusika katika 'Usiniuwe' . . . . . . 160
4.6.3.1. Mtoto . . . . . . . . . . . . . . 160
4.7. Mandhari . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 163
4.7.1. Mandhari katika 'Kutendana' . . . . . . 163
4.7.2. Mandhari katika 'Mnazi Vuta N'kuvute' . 165
4.7.3. Mandhari katika 'Usiniuwe' . . . . . . 167
4.8. Maleba . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 169

SURA YA TANO . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 172

HITIMISHO . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 172
5.1 Utangulizi . . . . . . . . . . . . . . . . . . 172
5.2. Masuala ya Kuhisi, Tajriba na Maana katika Maigizo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 172
5.3. Mapendekezo na Maagizo . . . . . . . . . . . . 178

MAREJELEO . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 180

KIAMBATISHO I . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 185

KIAMBATISHO II . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 187

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1. Kichocheo

Ushairi una sifa za kipekee ambazo zinaubagua kutokana na tanzu nyenginezo za kifasihi, riwaya na tamthilia. Senkoro (1988:iv) anasema yafuatayo kuhusu tofauti hizo;

> Ushairi ni aina ya fasihi inayotofautiana na hadithi na tamthilia hasa katika umbo na matumizi ya lugha. Wakati ambapo fasihi ya kinathari inatumia lugha ya mjazo na ya mtiririko, ushairi hutumia lugha ya mkato yenye kueleza maudhui yake kimuhtasari, na aghalabu huyaficha maudhui hayo ndani ya taswira.

Baadhi ya sifa zinazoutofautisha ushairi kutokana na tanzu nyenginezo ni urari wa vina na mizani, lugha ya mkato, au hata msisitizo juu ya uimbikaji wa shairi (Senkoro 1988). Jakobson, mmoja kati ya wafuasi wa shule ya mawazo ya Prague, aliwahi hata kuufafanua ushairi kama mabavu teule yanayotendewa lugha ya kawaida (Eagleton 1983).

Ushairi wa Kiswahili kama turathi ya kifasihi umekumbana na mabadiliko mengi. Awali, ushairi wa Kiswahili unasemekana ulikuwa ukiimbwa tu (Senkoro 1987,1988). Pia tunatajiwa utendwaji wa ushairi miongoni mwa jamii za Waswahili. Chiraghdin (1971) anaeleza jinsi utendaji huo ulivyotekelezwa; kuwa malenga wawili wasiofahamiana huko Mvita wangeweza kujibizana kishairi, kwa mafumbo, hadi paibuke mshindi kati yao. Huu ni utendaji ambao, kama vile tamthilia, ulitegemea majibizano kati ya magwiji wawili.

Baadaye vikaja vipindi vya ushairi huo kuwekwa katika maandishi. Ushairi, kwa kupitiwa na wakati, umekuwa ukibadilika. Miaka ya sabini, kwa mfano, ilishuhudia uibukaji wa ushairi huru ambao ulilitupilia mbali suala la urari wa vina na mizani kama

'roho' ya ushairi. 'Wanamapinduzi', kundi jipya lililohimiza ushairi huria huko Tanzania, kwa ufupi, hawakuona umuhimu wa kufungwa fungwa na sheria za kijadi. Urari wa vina na mizani kwao kilikuwa kikwazo ambacho walidai kiliwanyima watunzi uwezo wa kuzieleza fikra na maudhui mapya katika jamii. Wazo hili, kwamba vina na mizani ni adui wa maudhui, linadhihirika hata katika tahakiki zilizofanyiwa washairi waliofuata utaratibu huo. Senkoro (1988:80), akiihakiki fani ya ushairi wa Semghanga, anasema;

> ... Japokuwa mshairi kajitahidi kuzingatia kanuni za tenzi za kimapokeo ... kanuni na minyororo hii ya "sheria" imemfunga mno ikamletea matatizo ...

Senkoro, kama wanamapinduzi wengine, anajaribu kuonyesha kwamba kinachowashughulisha waandishi wa kijadi ni urari wa vina na mizani tu kiasi kwamba kazi zao zinaishilia kuwa chapwa kimaudhui. Aidha, wanamapinduzi wanadai kwamba ushairi wao ni bora kwa kuwa unasisitiza maudhui kuliko vina na mizani tu. Vilevile ushairi wao, wanadai, unafaa zaidi kwa kuwa una uwezo wa kueleza maudhui mpya.

Abdilatif, akiwa mshairi wa kijadi, anasisitiza ufuataji kanuni za kijadi katika utunzi wa mashairi. Mshairi huyu, kama wanajadi wengineo, anasisitiza masuala ya urari wa vina na mizani, mguso wa hisi za moyoni na ustadi wa lugha. Abdilatif (Senkoro 1988:4), anaueleza ushairi kama;

> Utungo ambao katika kila ubeti wake kuna ulinganifu wa vina vitukufu vilivyopangwa kimoja baada ya chenziye; wenye vipande vilivyo na ulinganifu wa mizani zisizo pungufu wala zilizo zaidi; na vipande hivyo viwe vimetandwa na maneno ya mkato maalum na yenye lugha nyofu, tamu na laini, lugha ambayo ni tetelezi kwa ulimi kwa kuitamka, lugha ambayo ina uzito wa fikra, tamu kwa

> mdomo wa kuisema, tumbuizi kwa masikio ya kuisikia na yenye kuathiri moyo uliokusudiwa na kama ulivyokusudiwa.

Katika tahakiki yake, Senkoro (1988) anamwona Abdilatif kama mmoja wa watu ambao wanastaladhi vina na mizani tu katika tungo zao. Kwa kauli yake, mhakiki huyu anasema;

> ... Jambo ambalo wanamapokeo kama vile Jumanne Mayoka na Abdilatif Abdalla hawakuzingatia katika vita vya maneno baina yao na wanamabadiliko ni kwamba akina Kezilahabi, Kahigi, Mulokozi na wenzao hawana vita na ushairi wa Kiswahili unaofuata hizo sheria. Kwa mfano, katika diwani ya Mulokozi na Kahigi ya Malenga wa Bara zaidi ya nusu ya mashairi yao ni ya kimapokeo yafuatayo "sheria" za vina na mizani...

Hata hivyo, yapo madai yanayotanza kuhusiana na tungo za Abdilatif. Madai haya, kwa kiwango kikubwa, yanaupiku na kukifanya kijelezi chake cha nini ushairi kukosa mashiko. Fauka ya hayo, madai ya Senkoro kwamba ushairi wa kijadi si chengine ila ustadi wa vina na urari wa mizani tu yanakosa mashiko. Chacha (1992:13) anatufunulia maoni yake kuhusu tungo za Abdilatif, hususani <u>Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa</u>, anaposema;

> Abdilatif anatumia kanuni za kimapokeo katika uandishi wa utenzi huu. Muundo huu umetumiwa na watunzi wengine wengi waliowahi kutunga tenzi za masomo mbalimbali. Pamoja na kuzingatia muundo huu <u>mbinu za kitamthilia</u> zinatumiwa pia.
>
> (Msisitizo ni wetu)

Tamthilia ni utanzu wa kifasihi wenye sifa zake mahsusi. Kimsingi tamthilia ni utanzu ulioandikwa kwa madhumuni ya kuigizwa kwenye jukwaa. Mwandishi wa tamthilia, kwa kulizingatia hilo, hutumia sanaa changamano yakiwemo maelekezo ya jinsi mchezo wake utakavyoigizwa ili azalishe picha za kimaono kwa wasomaji wake

(Reinert 1970, Perrine 1988, Hall 1987).

Kwa kutolewa madai kwamba Abdilatif ameandika tungo zinazozingatia mbinu za kitamthilia, na hivyo basi mbinu za kimaigizo, mshairi huyu ameuondoa ukavu wa ushairi kama utanzu huo unavyofahamika (Peck & Coyle 1984, Perrine 1988). Badala yake, amezifanya tungo zake zipendeze zaidi kwa msomaji kwa vile vitendo vya kimaigizo huwa vinampitikia akilini mwake huku akistaladhi urari wa kishairi. Jambo hili linaashiria kwamba si urari wa vina na mizani uliozingatiwa tu, bali pia mbinu za kimaigizo ambazo mwandishi amezitumia katika kuuwasilisha ujumbe wake. Ni kutokana na madai haya yanayoelekezewa ushairi wa Abdilatif ambapo utafiti huu ulipata mashiko.

## 1.2. Maelezo ya Istilahi

Maigizo: Istilahi hii imetumika kufafanua mawasiliano ya kijukwaa ambayo yanatilia maanani mzunguko wa utatu; yaani kuwepo kwa waigizaji, jukwaa na hadhira inayowasilishiwa kazi hiyo.

Mbinu za kimaigizo: Tumeitumia istilahi hii kurejelea vipengele maalum vya kiujumi vinavyojitokeza katika mawasiliano ya kijukwaa aliyoyatumia Abdilatif Abdalla. Vipengele hivi ndivyo vinavyozipatia tungo za mshairi huyu ubainifu wake unaozifanya tungo hizo kuwa tamthilia badalia.

Hisi ya maigizo: Taathira inayoibuliwa kwenye jumba la maonyesho kupitia kutumikishwa kwa milango yetu ya fahamu. Milango hiyo ya fahamu ni kupitia hisi za maonjo, kunusa, kuona, kusikia na kugusa.

Semiotiki: Wataalam mbalimbali wanakubaliana kuwa hii ni nadharia inayohusiana na mawasiliano (Hawkes 1977, Elam 1980, Frost &

Yarrow 1993). Katika utafiti huu, tumeitumia nadharia hii kama juhudi za uzalishaji na uwasilishaji wa maana, sio kwa upande wa mwandishi tu bali pia kwa hadhira.

Wahusika: Wahusika, kama wanavyofahamika, ni viumbe wa kibunifu wanaopatikana kwenye hadithi (Mohamed 1992). Hata hivyo, ni muhimu kutaja pia kwamba viumbe hao, vilevile, wanajitokeza kwenye tamthilia. Katika utafiti huu, tumeitumia istilahi hii kurejelea viumbe wa kibunifu wanaopatikana katika tungo za Abdilatif. Tumeipendelea istilahi hii kuliko ile ya waigizaji kwa kuwa tunategemea maandishi kujizalishia picha za kimaono kwenye jukwaa la bongo zetu.

Ploti: Katika utafiti huu, dhana ya ploti imetumika kurejelea mtiririko wa vitushi, kama vilivyowasilishwa na Abdilatif.

Kitendo: Hii ni dhana pana, tena dhahania kutokana na mtazamo wa Aristotle (Kernan 1963). Tumeitumia dhana hii kurejelea utendaji, sio wa maneno tu, bali hata wa kimwili unaotekelezwa na wahusika. Hivyo basi, kitendo ni jumla ya maneno na kutumikishwa kwa miili ya wahusika katika yale wanayoyatekeleza kwenye jukwaa.

Mandhari: Ulimwengu au eneo wanalosuhubiana wahusika katika tungo za Abdilatif.

Jukwaa: Upenu au mahala ambapo shughuli za uigizaji zinatekelezewa na wahusika.

Maleba: Jumla ya mapambo yanayopewa wahusika na msanii. Katika utafiti huu, maleba ni mapambo ambayo Abdilatif anawapatia wahusika wake, akiwa na lengo la kuwasilisha hisi na maana inayoambatana na maleba hayo.

Kaida za kimaigizo: Ukubaliano unaohusiana na uwasilishaji wa

maigizo kati ya mtunzi na hadhira yake.

### 1.3. Mada ya utafiti

Zipo baadhi ya tungo za Abdilatif ambazo zinadaiwa zinayatimiza matakwa yote ya kitamthilia. Hili linazungumziwa na Chacha (1992) anaposema kuwa ingawa Abdilatif hajaandika kitabu cha mchezo wa kuigiza, ushairi wake unaweza kuitikia misingi ya tamthilia. Swala kuu hapa ni jinsi utanzu wa ushairi unavyomiliki sifa ambazo zinaufanya uwekwe katika medani sawa na tamthilia; kwamba ushairi wa Abdilatif una uwezo wa kufidia pengo lake la kutoandika tamthilia.

Tamthilia yoyote, inapoandikwa, huwa inalengwa kuwa amali ya kuonyeshwa jukwaani na wala si kwa madhumuni ya kusomwa au kuwekwa maktabani tu. Hivyo basi, kufanikishwa kwa tamthilia kama kitendo kinachoendelea, kwa kiwango kikubwa, kunategemea kuwepo kwa waigizaji, jukwaa na watazamaji (Perrine 1988). Wazo hili linamaanisha kwamba kazi za Abdilatif si za kusomwa na kusikilizwa na baadaye kutafakariwa tu, bali ziangaliwe pia kama amali ya kuigizwa kwenye jukwaa.

Tulichonacho, kwa sasa, ni tungo za Abdilatif na wala si michezo tunayoiona kwenye jukwaa halisi. Lakini mtunzi wa kazi ya kuigizwa, kama ilivyo ada, huwa anafahamu kwamba mchezo wake ni wa kuigizwa. Hili linadokezwa na Reinert (1970:xii) anaposema;

> ... Hili linamaanisha kwamba utendwaji wa drama ni zaidi ya usanii wa lugha ... Na kwa kuwa kile mwanadrama anachoandika ni andiko linaloweza kuigizwa, picha anazozisawiri hujenga kile Ronald Peacock anachokiita "umbo mseto, linalotumia sanaa mbalimbali kufikia lengo moja." ...
>
> (Tafsiri Yetu)

Anachotufahamisha Reinert ni msisitizo juu ya dhima ya mwandishi yeyote anayeandika mchezo kwa madhumuni ya kuigizwa kwenye jukwaa. Kulingana na maoni haya, Mwanadrama huwa hatumii sanaa ya lugha pekee bali, kupitia lugha, hutumia pia mbinu za sanaa nyenginezo kama ile ya uongozi katika maandiko yake.

Mada yetu ya utafiti ilikuwa na misingi yake katika hoja kwamba, mwandishi wa kazi yoyote ya kifasihi, huteuwa na kuipanga kazi yake kwa namna ambayo itamwathiri msomaji wake. Kwa mfano, mwandishi huiteuwa fani ambayo anaikadiria kuwa itauwasilisha ujumbe wake kwa njia ya mvuto zaidi. Kwa kulizingatia hilo, tulichunguza jinsi Abdilatif alivyozitumia mbinu za kimaigizo katika tungo zake ambazo zilituwezesha, kama wasomaji, kuyahisi maigizo yakitendeka, huku tukiibukiwa na maana anayoiwasilisha. Uwezekano huo wa msomaji kuzihisi drama zikiwa katika maandishi unaelezwa na Reinart (1970:xv) anayesema;

> Kutokana na kijelezi hicho cha drama, bila shaka usomaji mzuri wa tamthilia huijaza akili mfuatano wa picha mwafaka zinazoonekana vyema, hili likiwezeshwa na maongezi na maelekezo ya mwandishi. Uwezekano huo wa kuziona drama zikitendeka katika jukwaa kambifu akilini hujiri pindi msomaji huyo anapotafakari na kukitafsiri kila kinachoweza kuigizika na kukiweka katika vitu au mambo halisi ambayo kwa pamoja yanajumuika katika kuunda picha mseto za maneno, mirando ya wahusika, na onyesho linalounda kazi ya kidrama ...
>
> (Tafsiri Yetu)

Kutokana na dai kwamba tungo za Abdilatif zinatimiza matakwa ya kitamthilia, utafiti huu ulilizamia suala la jinsi mwandishi anavyotumia mbinu mbalimbali za kimaigizo katika tungo zake, na hatimaye kuibukiwa na maana anayoiwasilisha. Mada hii ilibainisha kwamba ushairi wa kijadi una uwezo wa kueleza maudhui yoyote kifasaha na kupanuliwa kifani bila ugumu wowote. Vipengele

tulivyovizingatia ni lugha, kaida za kijukwaa, ploti, kitendo, wahusika, mandhari jukwaa na mbinu nyinginezo zikiwemo maleba na kinaya drama.

**1.4. Makisio**

1. Abdilatif Abdalla anatumia mbinu za kimaigizo katika baadhi ya tungo zake.
2. Matumizi haya ya mbinu za kimaigizo zinamfanya msomaji azihisi tungo hizo zikiigizwa anapozisoma.
3. Mbinu hizi za kimaigizo zinazohusisha kuyaona maigizo yenyewe yakitendeka zinazifanya tungo hizo zieleweke zaidi.

**1.5. Madhumuni ya utafiti**

1. Kujadili kwamba, kwa kutumia mbinu za kimaigizo, Abdilatif amedhihirisha uwezo wa ushairi wa kijadi kujadili maudhui yoyote.
2. Kufafanua, kwa kuzingatia vipengele mbalimbali vya kimaigizo alivyotumia Abdilatif, jinsi dhana ya maigizo ilivyojitokeza katika tungo zake.
3. Kuueleza usomaji wa tungo hizi kimaigizo, yaani usomaji maalum wa kisemiotiki, hadi kufikia kuyahisi maigizo yakitendeka.

**1.6. Umuhimu wa utafiti**

Kwa muda mrefu, ushairi wa Kiswahili umeangaliwa katika misingi finyu. Fafanuzi nyingi zilizotolewa kuhusiana na ushairi zimekuwa zikisisitiza ama fani au maudhui yake. Mzozo kati ya wanamapokeo na wanamabadiliko katika ushairi wa Kiswahili, kwa

mfano, unaashiria kupendelewa kwa fani au maudhui. Kwa upande wao, wanamapokeo wanasisitiza ufuataji wa kanuni za kijadi huku wakinzani wao wakiupendelea ushairi huru utakaosheheni maudhui. Wahakiki na wachambuzi wa kazi za kishairi pia wamejishughulisha sana na masuala ya maudhui, vina na urari wa mizani, matumizi ya lugha na hata mwandishi mwenyewe na hisia zake kama kiungo muhimu cha kuuchanganulia ushairi.

Abdilatif ni miongoni mwa washairi wachache wa kijadi ambao wamejitahidi katika uandishi wao wa mashairi. Ustadi anaoudhihirisha katika utunzi wake unastahili kutafitiwa kwa undani. Kufikia sasa, ni kazi chache sana zilizojishughulisha na ushairi wake (Chacha 1992). Kazi hii inaitikia mwito wa kuutafiti kwa undani ushairi wake. Kuziangazia mbinu za kimaigizo katika ushairi wa Kiswahili kitakuwa kitu tunu cha kuzingatiwa. Tuna imani kwamba utafiti huu utawasaidia wasomaji wa tungo hizi na tamthilia kwa jumla, katika usomaji wa kimaigizo; wakipanuliwa uwezo wao wa kujichorea picha za kimaono kama hadhira ya maandiko husika.

## 1.7. Upeo na mipaka ya utafiti

Zipo tungo za Abdilatif ambazo zimetuhumiwa kuwa zinaitikia mwito wa kitamthilia, na hivyo basi, kutumia mbinu za kimaigizo katika kuwasilishwa kwake. Tungo hizi ni Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa, 'Mnazi: Vuta N'Kuvute', 'Kutendana' na 'Usiniuwe'. Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa ni utenzi mrefu ambao unajenga kitabu kizima kwa jina hilohilo. 'Mnazi: Vuta N'Kuvute', 'Kutendana' na 'Usiniuwe', kwa upande mwingine, ni miongoni mwa tungo zinazopatikana katika mkusanyiko wa mashairi

ya Abdilatif katika kitabu chake <u>Sauti ya Dhiki</u> (1973).

Kuteuliwa kwa tungo hizi kunatokana na kuzingatiwa kwa baadhi ya vipengele vya kimsingi vya kiuigizaji. Majibizano, yakiwa ndilo sharti la kimsingi kwa maigizo yoyote, yanazingatiwa. Vipengele vya wahusika, kaida za kijukwaa, kitendo, ploti, mandhari jukwaa, lugha, maleba na kinaya drama pia vinazingatiwa. Tunapolitafakari suala la drama, jambo kuu linalotupitia vichwani mwetu ni kuona vitendo vikitekelezwa na watendaji jukwaani. Mchezo ama dhana inayotendwa jukwaani huwa na uhai zaidi. Watazamaji huguswa na kuibuliwa hisia zao (Gianakaris 1975, Perrine 1988, Woods 1984). Utafiti huu unakosa uhondo huo kwani haukuzitafiti tungo za Abdilatif kwenye jukwaa zikiigizwa. Suala hili lilikuwa nje ya mipaka ya utafiti wetu. Tulimtegemea Abdilatif kutupatia picha ya kimwigo kwa kuutafakari umbuji wake wa mbinu za kimaigizo katika tungo tulizoziteuwa.

Kilichojadiliwa katika mada yetu ni mbinu za kimaigizo ambazo mwandishi anazitumia katika kutuwezesha kuyaona maigizo katika tungo zake kama wasomaji. Hapa ilitubidi tuchanganue maneno huku tukijizalishia ruwaza za kimaono; ruwaza ambazo zilituonyesha picha kamili za maigizo yanayotendeka kwenye jukwaa la bongo zetu.

## 1.8. Misingi ya nadharia

Nadharia ya semiotiki au semiolojia ndiyo iliyotumika katika utafiti wetu. Semiotiki, kama dhana, ni zao la Saussure, ambaye anaifafanua kama taaluma ya kisayansi inayojishughulisha na kuuchunguza uhai wa ishara katika jamii. Katika ufafanuzi wake de Saussure (Guiraud 1971:1) anasema;

> Lugha ni mfumo wa ishara unaoeleza mawazo, na hivyo basi unawekwa katika tapo moja na maandishi ... Sayansi inayochunguza uhai wa ishara ... ni sehemu ya saikolojia; tutaiita semiolojia (kutokana na neno la Kigiriki semeion, 'ishara'). Semiolojia ingetufunza vijengo vya ishara na sheria zinazotawala tabia za ishara hizo. Kwa kuwa sayansi hii haijajitokeza kama taaluma mahsusi, hakuna anayeweza kusema kwa uhakika iko vipi, isipokuwa ina haki ya kuwepo kwani nafasi yake imedhihirika. Isimu ni sehemu tu kati ya mwanda mpana wa sayansi ya semiolojia: sheria zilizovumbuliwa na semiolojia zitakuwa na nafasi yake katika isimu, na isimu itajikuta ina utangamano na eneo mahsusi katika masuala ya sayansi ya wanadamu.
>
> (Tafsiri Yetu)

Kulingana na de Saussure, uhai huu wa ishara unapewa uzito hasa kwa kuzingatia masuala ya uamilifu wa ishara hizo katika jamii.

Takribani wakati huu huu, mtaalam Peirce (Hawkes 1977) alitoa ufafanuzi wake juu ya kile alichokiita semiotiki. Kulingana na Peirce, ufafanuzi wa kanuni zinazozifafanua ishara zenyewe si jingine ila kuziangalia kwa makini sifa za ishara hizo. Peirce anadai kwamba tunafikia ukomo kwa kutoa madai na kauli ambazo zinajaribu kuamua kile ambacho lazima kiwe kiungo cha ishara. Katika kuieleza ishara, Peirce (Hawkes 1977:126) anasema;

> ... ishara au <u>kiwakilishi</u> ni 'kitu kinachofasirika kwa mtu kama kibadala cha kitu kingine katika uwezo fulani'; Ni kitu chochote kinachosimamia kitu kingine (<u>fasiri yake</u>) ili kurejelea kitu ambacho hiyo ishara yenyewe inakirejelea (<u>inachokirejelea</u>). Hivyo basi, ishara husimamia kitu (<u>kirejelezi chake</u>): inasimamia kitu kwa mtu (<u>fasiri yake</u>); na mwisho husimamia kitu kwa mtu kwa uwezo fulani (<u>msingi wake</u>).
>
> (Msisitizo Wake, Tafsiri Yetu)

Kutokana na vijelezi vya waanzilishi wa dhana hii, yaani de Saussure na Peirce, nadharia ya semiotiki inajishughulisha na

mifumo yoyote inayoweza kuitwa ishara na jinsi ishara hizo zinavyoweza kufasirika na kuwa mifumo ya kuashiria na kuleta maana kwa watumiaji wa ishara hizo. Umuhimu wa semiotiki kama njia ya uashiriaji katika jamii, umemfanya Hawkes (1977) kutoa rai kwamba semiotiki pamoja na umaumbo, ziwekwe katika himaya moja na taaluma ya mawasiliano.

Elam (1980), akigusia juu ya shughuli yoyote ya kisemiotiki, anasisitiza suala la mawasiliano au uashiriaji. Mtaalam huyu (1980:1) anasema;

> Semiotiki ni sayansi inayojishughulisha na jinsi maana inavyotolewa katika jamii. Vilevile tunaiona kama njia ya uashiriaji na mawasiliano, yaani njia ambazo maana zinazalishwa na kuwasilishwa. Vifaa vinavyotumiwa kufikia haya ni mifumo-ishara na misimbo mbalimbali inayotumika katika jamii na ujumbe unaozalishwa kutokana nayo.
> (Tafsiri Yetu)

Taaluma ya semiotiki, mbali na kuwa sayansi ya ishara, inajaribu kutueleza vijengo vya ishara zenyewe. Roman Jakobson (Hawkes 1977), anapendekeza jinsi ya kuvitalii vijenzi hivyo vya ishara. Kulingana na mtaalam huyu, kila ujumbe unaopitishwa huwa umejengwa na ishara mbalimbali. Ishara hizi ndizo changamoto ya taaluma ya semiotiki. Jakobson anaiona ishara yoyote kama amali ya vitu viwili - cha kwanza kikiwa kitu tunachoweza kukiona na kukihisi (signans) na cha pili tukikitambua kutokana na kukiambatanisha kwa unasibu na kile cha kwanza (signatum). Dhana hizi ni sawa na zile za de Saussure za kiashiria na kiashiriwa (Hawkes 1977). Tunapochunguza kwa makini, ipo kila sababu ya kuukatalia mbali mtazamo huu wa kuangalia vijenzi vya ishara. Maoni ya Jakobson yanatokana na mawazo kwamba hakuna uhusiano wowote kati ya kiashiria na kiashiriwa katika kuzalisha maana.

Yeye, kama vile Saussure, wanaiona fasihi kama kitu kikamilifu ambacho hakihitaji urejelezi wa nje katika kupata maana. Kiashiriwa, kulingana na Jakobson, ni 'kiumbe huru'; kikiwa na urazini wake (Jefferson na Robey 1982).

Roland Barthes (Hawkes 1977), kwa upande wake, anaiona ishara kama zao la uhusiano uliopo kati ya kiashiria na kile kinachoashiriwa. Tofauti na Jakobson, ambaye alikiona kiashiria kama mwongozo wetu wa kukifikia kiashiriwa, Barthes anaviona vitu hivi viwili vikiwa na hadhi sawa. Kulingana na mtaalam huyu, uwiano unaounganisha kiashiria na kiashiriwa ndio unaofafanua na kuijenga ishara. Anatoa mfano wa koja la maua ambalo baadhi ya jamii hulitumia kama ishara ya upendo. Kwa wawili wanaopendana, itikadi zilizomo nyoyoni mwao, pamoja na mfumo wa kijamii unaoupa uzito kitendo cha kupana maua kama ishara ya mapenzi, koja hilohilo la maua linakuwa kiashiria cha mapenzi. Mapenzi katika ngazi hii yanakuwa kiashiriwa. Koja hilo linapotolewa katika muktadha huu linakuwa ishara iliyojengwa na koja lenyewe kama kiashiria na mapenzi kama kiashiriwa.

Katika utafiti huu, tuliitumia nadharia ya semiotiki kama njia ya uzalishaji na uwasilishaji wa maana katika jamii. Nadharia hii ilitufaa hasa tunapofahamu kwamba Abdilatif anatumia mbinu za kimaigizo katika kuzalisha na kuwasilisha ujumbe wake. Akiwa mwanajadi, mshairi huyu hazingatii vina na urari wa mizani tu, bali anatumia vipengele vingine ili kuiwasilisha kazi yake. Kwa kujiteulia mbinu za kimaigizo katika kuiwasilisha kazi yake, Abdilatif anatumia ishara ambazo zinatambulikana kuwa ni za eneo la taaluma ya maigizo. Matumizi ya wahusika, jukwaa, kitendo na hata hadhira kusudiwa ya wasomaji ni baadhi tu ya ishara ambazo

amezitumia katika kuwasilisha ujumbe fulani kuhusu tungo zake; kwamba si ushairi tu bali pia vipengele vilivyotajwa, kwa pamoja, vinaonekana vikitendeka katika bongo zetu na hivyo basi kuashiria kutumika kwa mbinu za kimaigizo kama njia ya mawasiliano. Mbinu hizo ni jumla ya viashiria ambavyo vinaunda mfumo wa mawasiliano au viashiriwa. Tungo zenyewe katika ukamilifu wake zinakuwa ishara. Tulimwangalia Abdilatif, kwa maoni ya Elam (1980), kama 'mzalishaji na mwasilishaji wa maana katika jamii'. Kwa kuziangalia mbinu mbalimbali za kimaigizo, ambazo ni mchangamano wa viashiria anavyovitumia Abdilatif ili kuuwasilisha ujumbe wake kwa njia maalum ya kimaigizo, tulikuwa vilevile tukilizingatia suala kuu la nadharia ya semiotiki.

Nadharia ya semiotiki ilitufaa hasa katika kujadili maswala ya fani. Nadharia ya uhalisi wa kijamii, kama alivyoitumia Chacha (1992), haingetufaa kwani inaelekea zaidi kujadili maswala ya maudhui. Hili lilimfanya Chacha ayarashierashie maswala ya nyenzo za fani alizozitumia Abdilatif, kwani uzito wa kwanza ulipewa maudhui. Semiotiki, ikiwa nadharia ya hivi majuzi, inaliziba pengo hili, hasa tunapotilia maanani hoja kwamba ina ukuruba na nadharia nyingine kama vile umuundo na nadharia ya mawasiliano. Fauka ya hayo, nadharia ya semiotiki inatupatia jibu la kitendawili cha ushairi kuwa 'ushairi' na wakati huohuo ukawa 'tamthilia'. Ushairi huwa na umbo maalum ambalo, kwa kuliona tu, tunaupata ujumbe kwamba tulioouona ni ushairi. Ujumbe huu wa macho una nguvu zaidi katika kuamua iwapo linaloonekana ni shairi kuliko yale yanayojadiliwa (Hawkes 1977). Hata hivyo, matarajio yetu yanaweza yasiwe ya kiyakinifu tunaposoma shairi fulani na kudhihirikiwa na vipengele ambavyo si vya kishairi na

kugundua kwamba ni vya kitamthilia. Tegemeo na tajriba yetu juu ya mbinu zinazopatikana katika vipengele vya kitamthilia vitatupelekea kuona na kudai kwamba kinachojadiliwa si ushairi bali ni tamthilia. Hili ni suala ambalo nadharia ya semiotiki linakiri. Uchanganuzi wa kisemiotiki huliangalia suala hili kama njia mojawapo ambayo kazi fulani inatumia katika kuunganisha ujumbe wake. Kulingana na kaida za kisemiotiki, kila kazi ya kisanaa inajiamulia njia ya kuuwasilisha ujumbe wake (Hawkes 1977). Katika mkabala huu, tunaweza tukafahamikiwa na tuhuma za wataalam kama vile Chacha (1992) ambaye, kwa kuzisoma tungo za Abdilatif, anaziona kama tamthilia badalia za mwandishi huyo.

### 1.9. Mapitio ya maandishi

Knappert (1967) ni miongoni mwa wahakiki wa mwanzo waliozichunguza tenzi za Kiswahili. Tenzi alizozishughulikia ni pamoja na Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa. Lengo lake kubwa lilikuwa ni kuufafanua ulimwengu wa tenzi kama ulivyowadhihirikia washairi wa Kiswahili. Knappert anaziona tenzi zikiwa na majukumu mawili. Kwanza, ni kukifunza kizazi kipya jinsi uadilifu unavyotukuzwa, na uovu unavyotwezwa na kuadhibiwa. Pili, anaziona tenzi kama kilinge cha kushindwa kwa mahasidi kwa kuwa Mungu, wakati wote, hayuko pamoja nao. Anauona Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa ukiwa na mafunzo kama haya. Anawataja Ibilisi, Adamu, Hawaa, Habili, Kabili, Mungu na Malaika kama wahusika wanaojenga mafunzo haya.

Knappert anadokezea kuonekana kwa drama katika utenzi huu. Swala la mandhari analijadili vilivyo kama linavyomkabili mhusika Adamu. Maelezo ya Abdilatif yanamwezesha Knappert kuifananisha

mandhari ya ushairi na ile ya Hijaaz au Yemen. Knappert pia anayahisi manukato ya peponi anapousoma utenzi huu. Maoni haya ni ushahidi wa kutumika kwa mbinu za kijukwaa katika utenzi huu. Hata hivyo, swala hili halikupewa uzito unaostahili. Knappert ametaja kwa kupitia tu uwezo wa kuonekana kwa utenzi huu kwenye bongo la msomaji. Lengo lake kuu lilikuwa ni kuufafanua ulimwengu wa washairi wa Kiswahili kama unavyowadhihirikia.

Kiango (1973) anaangalia vipindi mbalimbali vya kihistoria na jinsi vilivyoathiri michezo ya kuigiza. Kulingana na Kiango, michezo ya kuigiza haikuanza karne hii na majilio ya wazungu kama baadhi ya watu wanavyofikiria. Badala yake, msomi huyu anatutanabahisha kuwa, chanzo cha michezo hii imo katika sanaa za maonyesho za Kiafrika. Mtaalam huyu anautaja 'Utenzi wa Fumo Liyongo' na Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa kama michezo miwili ambayo imeandikwa katika hali ya utenzi. Sifa kuu inayomfanya kusema hivyo ni kuwa wahusika wa tenzi hizi wanajibizana katika maingiliano yao. Anaendelea kusema kuwa tofauti na 'Utenzi wa Fumo Liyongo', wahusika wa Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa wanaachwa wajitokeze wenyewe. Kauli hii inaoana na maoni yetu kuwa majibizano ndilo swala la msingi katika mchezo wowote wa kuigiza. Hata hivyo, hatufahamu barabara vigezo vingine alivyovitumia Kiango katika kuuita utenzi huu mchezo wa kuigiza. Haja ya kuviangalia vigezo vingine vinavyoupatia utenzi huu sifa ya kuwa mchezo wa kuigiza ipo.

Topan (1971) anausifu ustadi wa Abdilatif katika Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa. Anauona utenzi huu kama kipoza-kiu ya mtu anayesakamwa na ari ya kujionea mchezo ukiigizwa kwenye jukwaa. Analomuasa mtu kama huyo, ni kuituliza akili yake, na

kuvisawiri vitendo hivyo moyoni mwake. Atakapofanya hivyo, angalau, atakuwa ameipoza harara inayomkaba. Kinachodhihirika katika maelezo ya Topan ni kwamba usomaji wa utenzi huu na kuitafakari drama inayotendeka si kama kuiona drama yenyewe katika jukwaa. Topan, mbali na kuiona drama ikitendeka katika utenzi huu, hasongi mbele zaidi na kueleza sifa za kidrama katika utenzi huo. Pengine Topan alikuwa ameshughulishwa sana na nyanda pana ya michezo ya kuigiza aliyokuwa akiijadili. Tunathibitikiwa pia na ukweli kwamba Abdilatif amezitumikisha vilivyo nguvu za sanaa ya lugha hadi kufikia uwezo wa kuwazalishia wasomaji wake picha mbalimbali za kimaono katika jukwaa la bongo zao.

Chacha (1992) ni miongoni mwa wataalam waliozishughulikia kazi za Abdilatif. Kama mhakiki, anaangalia jinsi mazingira ya mwandishi yanavyomwezesha kuzungumzia hali halisi ya kiuchumi, kijamii na kisiasa ambamo wanajamii wenzake wanajikuta. Hii, kwa ufupi, ndiyo sehemu ya maudhui ambayo Chacha anaizamia. Vilevile, anaangalia kunga mbalimbali za fani ambazo Abdilatif anatumia katika ushairi wake. Hapa tunafahamishwa uwezo wa mwandishi katika kueleza kwa ufundi maudhui yake kwa kutumia taswira, mafumbo, istiara na jazanda katika kuikebehi na kuisawiri hali ya kiuchumi ya nchi ya Kenya.

Chacha (1992), anasisitiza utamthilia wa baadhi ya mashairi ya Abdilatif, ambao wasomi waliotangulia kama vile Knappert na Topan walikuwa wameshautaja. Chacha anatoa kauli kwamba wahakiki hawa hawakuenda mbali ila kutaja tu utamthilia wa <u>Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa</u>. Msomi huyu anaenda hatua moja mbele kwa kutoa maelekezo ya jinsi ya kuionyesha hadhira tamthilia yake ya 'Adamu na Hawaa'. Mbali na utenzi huu, mtaalam huyu

anayataja mashairi ya 'Mnazi: Vuta N'Kuvute' na 'Kutendana' katika Sauti ya Dhiki, kuwa yana hadhi ya tamthilia.

Chacha anatoa maelezo ya kimwongozo katika kuuigiza mchezo wa 'Adamu na Hawaa'. Maelekezo haya, ingawa mafupi, yalitupatia mwanga katika kuvifuatilia vitendo vya wahusika wa mchezoni. Hata hivyo, ni muhimu kutahadharisha kwamba maelekezo haya si lazima yamdhihirikie msomaji kama yanavyopendekezwa na Chacha. Kwa upande wetu, tumemtegemea sana Abdilatif katika maswala ya kiuongozi. Aidha, msomi huyu hajazama kikamilifu katika kutuonyesha mambo ambayo yanaufanya utenzi huu kuwa tamthilia badalia. Mashairi ya 'Mnazi Vuta N'kuvute' na 'Kutendana' katika Sauti ya Dhiki, ambayo Chacha anasema yana utamthilia, hayazingatiwi ila yanatolewa kauli kwamba yana utamthilia. Hata hivyo, maudhui aliyoyajadili kuhusiana na tungo hizi yatamfaidi msomaji kuifahamu misingi ya kihistoria ya maigizo haya.

Matteru (1975) ni mmoja kati ya watu waliohakiki Sauti ya Dhiki. Mtaalam huyu anadokezea juu ya fani ya ushairi wa Abdilatif na mada mbalimbali ambazo mwandishi anaziibua. Kulingana na Matteru (1975:28) Sauti ya Dhiki;

ni Utetezi
ni Maombolezo
ni ujumbe
ni Kiu ya Heri
ni Sauti ya Shime
ni Mjadala wa Nafsi
ni Kitulizo

Yote haya yanaashiria jinsi mashairi ya mtunzi huyu yalivyosheheni ujumbe. Tuliangalia iwapo Abdilatif amefaulu kutupatia picha kamili ya maoni haya katika tungo zake, na iwapo sifa za kiutetezi zimejitokeza katika maonyesho yake.

Mohammed (1977), alikipitia tena kitabu hichohicho na

tasnifu ya makala yake ikaizamia fani ya mashairi yake. Mtaalam huyu anaiona fani ya Sauti ya Dhiki ikiwa ni zao la kariha, ghamidha na ghadhabu za mtunzi. 'Kariha', kwa ufupi, inaelezwa kama lile dukuduku ambalo humpelekea mwandishi kutafuta njia za kulitoa. 'Ghamidha' nayo, anaieleza kama ukingo wa kusakamwa na kariha moyoni, ikawa hapana budi ila kusemwa kwa kitu kinachomsumbua mtu. Mwisho ni 'ghadhabu' zinazoelezwa kama aina ya hujuma ambayo haimjalishi mtu na hatima yake ingawa huenda ikamdhuru. Anapoijadili fani, Mohammed anataja mtindo wa mtunzi, lahaja anayotumia kiutunzi, na uteuzi wa maneno kama njia yenye mguso hasa katika kueleza maudhui.

Massamba (1983) anazungumzia kwa kirefu maswala ya fani katika ushairi wa Kiswahili. Mhakiki huyu anasisitiza matumizi ya mitindo sadifu katika utunzi wowote wa ushairi. Shairi la kuonya au kutanabahisha, kwa mfano, anasema ni lazima lisisitize jambo hilo. Mawazo haya yalitufaa hasa katika kujadili sababu za mshairi Abdilatif kuteua mtindo wa kijukwaa katika ushairi wake. Maoni ya Massamba yanatuelekeza katika kuziona jitihada za Abdilatif katika kuzivuta nadhari za wasomaji wake. Wasomaji wa tungo hizi wanayatilia maanani maswala yanayoibuliwa sio kwa kusoma tu, bali kwa kuyaona yale yanayosemwa katika bongo zao.

Mbali na uteuzi wa mitindo sadifu, Massamba anagusia kipengele cha lugha katika ushairi. Kulingana na msomi huyu, kipengele cha lugha kinagawanyika katika vipengele vinne muhimu. Hivyo ni pamoja na lugha ya ushairi au ya kishairi, lugha ya wahusika, matumizi ya picha na tamathali mbalimbali za usemi na lugha kwa mintarafu ya hadhira. Vipengele hivi ni sehemu tu ya jumla ya kunga za kishairi ambazo Abdilatif anazizingatia. Sura

ya pili ya tasnifu hii, kwa mfano, inaangalia kwa undani swala la lugha ya ushairi na uhusiano wake na maigizo katika tungo ambazo tumezichanganua. Mbali na kuitumia lugha, tumeonyesha pia jinsi wahusika wa Abdilatif walivyoshikamanishwa kupitia matendo ya kimwili na hata mavazi. Vilevile, Abdilatif anadhihirisha ustadi wake katika matumizi ya picha. Tunaafikiana na Massamba kuwa picha ndicho kitu muhimu katika ushairi. Kwa kiasi kikubwa mbinu hii ya kishairi ndiyo iliyozipatia tungo za Abdilatif uwezo wa kuonekana zikiigizwa.

Muhando na Balisidya (1976) wanatoa mjadala wa kuzindua kuhusiana na sanaa za maonyesho za Kitanzania na za Kiafrika kwa ujumla. Wataalam hawa wanalalamika kuwa lolote la Kiafrika hubezwa kwa kupendelewa Umagharibi. Wakizijadili sanaa za maonyesho, wanaukubali ufafanuzi wa kinadharia unaoieleza sanaa ya maonyesho kama kitendo chochote chenye sifa nne kuu. Hizi ni pamoja na mchezo, mchezaji, uwanja wa kuchezea na watazamaji. Utesi wa wataalam hawa na ufafanuzi huu ni neno 'mchezo' ambalo wanadai haliafikiani na ufafanuzi wa sanaa za maonyesho za Kitanzania. Mahala pa neno hilo, wanapendekeza, pachukuliwe na 'dhana inayotendeka'. Mawazo ya wataalam hawa yalitufaa hususani tulipoangalia mwoano uliopo kati ya 'tamthilia' za Abdilatif na ushairi kama zao la jamii ya Waswahili wenyewe.

Muhando na Balisidya hawatoi kauli za kuridhisha wanapouangalia ushairi katika hali finyu. Ushairi, kwa wataalam hawa, ni moja kati ya 'Sanaa za Ghibu'; kwamba ni sanaa ambayo uzuri wake haujitokezi kwenye umbo linaloonekana kwa macho au kushikika bali katika umbo linalogusa hisia. Ushairi wanauona kama sanaa ya kusikizwa tu; wakiukadiria uwezo wake wa kuwa

sehemu muhimu ya sanaa za maonyesho za Kiafrika.

Tunapoyaangazia yalioandikwa kuhusu tungo za Abdilatif, ni wazi kwamba uhusiano kati ya Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa na tamthilia umegusiwa. Knappert (1967), Topan (1971), Kiango (1973) na Chacha (1992) wamejaribu kutueleza kuwa utenzi huo una uwezo wa kuonekana kwenye bongo la msomaji. Chacha amewahi kutuonyesha jinsi utenzi huu unavyoweza kuelekezwa na kuwa mchezo wa kuigiza. Maelezo kuhusiana na utamthilia wa utenzi huu ni machache huku nafasi kubwa ikipewa maudhui. Wataalam hawa hawatuelezi sifa mahsusi au mbinu maalum ambazo zinaufanya utenzi huu kuwa na uwezo wa kuonekana ukiigizwa pindi msomaji anapousoma.

Sambamba na utenzi huu, tumeangalia pia 'Mnazi: Vuta N'Kuvute', 'Kutendana' na 'Usiniuwe'. Mashairi haya yameangaliwa kwa ujumla na mashairi mengineyo yanayopatikana katika Sauti ya Dhiki. Kama ilivyobainika, Chacha (1992) alikuwa akiyatumia mashairi haya matatu na mengineyo kama mifano ya maudhui yake yakiwemo kweli, maonyo ya mshairi kwa watu wengine, siasa na kadhalika. Maswala ya kiuwasilishaji au fani katika mashairi haya kama vile mbinu za kimaigizo hayakuzingatiwa.

Pengo hili liliupatia utafiti huu nafasi ya kuziangalia mbinu alizozitumia mshairi huyu katika ushairi wake ambazo zinazifanya tungo hizi ziigizike kwenye jukwaa.

### 1.10. Njia za utafiti

Mtafiti wa kazi andishi za kimaigizo huitumia matini ya mtunzi iliyobuniwa kwa minajili ya kuigizwa kama mali ghafi ya utafiti wake (Elam 1980). Kutokana na rai hii, tungo za

Abdilatif zilitumika kama mali ghafi ya utafiti wetu. Mashairi ya 'Mnazi: Vuta N'Kuvute', 'Kutendana' na 'Usiniuwe' yanayopatikana katika Sauti ya Dhiki (1973), na Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa (1971) ndizo matini kuu zilizoufanikisha utafiti huu. Tungo tulizoziteuwa zilichambuliwa na kuchanganuliwa ili kudhihirisha mbinu za kimaigizo zilizotumika. Kazi hii, kwa kiwango kikubwa, ilitekelezewa maktabani.

Aidha tulitumia mbinu ya mahojiano kama njia ya ziada katika utafiti wetu. Hapa tuliwalenga wataalam wa Kiswahili katika nyanda za ushairi na taaluma ya maigizo. Maswali yaliyoongoza mahojiano hayo na majina ya wataalam tuliohojiana nao yameambatishwa mwishoni mwa tasnifu hii.

# SURA YA PILI

## LUGHA KAMA MFUMO UNAOJIASHIRIA: JUKUMU LA KISHAIRI NA MAIGIZO KATIKA TUNGO ZA ABDILATIF

### 2.1. Utangulizi

Sura hii inanuia kuuweka msingi wa dhana ya 'semiotiki ya ushairi'. Ushairi, kama mfumo wa mawasiliano, una kaida zake za kutekelezea mawasiliano hayo. Abdilatif, akiwa mshairi, anazizingatia mbinu hizo zinazofanikisha mawasiliano. Hivyo basi, ufahamu wetu wa tungo zake utatuhitajia kuzielewa ala mbalimbali za lugha ya kishairi ambazo mshairi huyu amezitumia.

'Semiotiki ya ushairi' ni dhana itakayoweza kutumiwa kuihukumia kazi yoyote inayoweza kuitwa 'ushairi' kwa kuizingatia lugha yake. Wazo hili halimaanishi kwamba ushairi uliotungwa kinyume na alivyotunga mshairi huyu si ushairi. Wala matilaba yetu si kutoa kijelezi cha 'nini ushairi'.

Swala kuu lililochunguzwa, na ambalo linahusiana na dhana ya 'semiotiki ya ushairi', ni zana mahsusi za lugha zinazozipatia tungo hizi hadhi ya kishairi. Ala za lugha alizozitumia mshairi huyu ndizo zilizochanganuliwa huku tukizinasibisha ala hizo na eneo letu la maigizo. Kwa kufanya hivyo, sura hii imekuwa ikilizamia jukumu la kishairi katika tungo za Abdilatif, yaani, jinsi lugha ya kisanaa inavyojiashiria na kuwa nyenzo ya maana.

### 2.2. Umuhimu wa Lugha katika Ushairi

Ushairi aghalabu umefafanuliwa kwa kuizingatia lugha yake. Waugh (1985), akimnukuu Jakobson, anaueleza ushairi kama upeo wa matumizi ya lugha ambayo huashiria kwa njia isiyokuwa ya kawaida. Kauli hii inathibitishwa, na kutiliwa nguvu zaidi, na fafanuzi

mbalimbali za 'nini ushairi' zinazotolewa na washairi wa Kiswahili. Vijelezi vyao, kwa kudokezea au kwa uwazi, vinaukiri umuhimu huu wa lugha.

Abdilatif, kama tulivyoona katika sura ya kwanza, anataja umuhimu wa lugha nyofu, tamu na laini, lugha ambayo ni tetelezi kwa ulimi wa kuitamka, lugha ambayo ina uzito wa fikra, tamu kwa mdomo wa kuisema, tumbuizi kwa masikio ya kuisikia, licha ya kuathiri moyo wa msikilizaji wa ushairi wenyewe.

Naye Mnyampala (1980) katika dibaji ya kitabu chake cha Diwani ya Mnyampala anatoa kijelezi hiki;

> Ushairi ni msingi wa maneno ya hekima tangu kale. Ndicho kitu kilicho bora sana katika maongozi ya dunia kwa kutumia maneno ya mkato na lugha nzito yenye kunata iliyopangwa kwa urari wa mizani na vina maalum kwa shairi.

Mulokozi na Kahigi (1979:25) wanaueleza ushairi kama;

> ... sanaa inayopambanuliwa kwa mpangilio maalum wa maneno fasaha yenye muwala, kwa lugha ya mkato, picha au sitiari au ishara, katika usemi, maandishi, au mahadhi ya wimbo, ili kueleza wazo au mawazo, kufunza au kueleza tukio au hisi fulani, kuhusu maisha au mazingira ya binadamu, kwa njia inayogusa moyo.

Akitoa kijelezi chake, Senkoro (1988:9) anasema;

> Ushairi ni utanzu wa fasihi utumiao mpangilio wa lugha ya mkato ya kipicha na iliyopangwa kwa njia iletayo mapigo mahsusi kufuatana na maudhui yahusikayo.

Umuhimu wa lugha unajidhihirisha katika vijelezi vya washairi na wahakiki maarufu wa ushairi wa Kiswahili. Lugha ya kishairi, kama inavyojitokeza, ni ya kipekee yenye sifa zinazoushamiri utanzu huo. Upekee huo unatokana na uwasilishaji wake wa tajriba za kila siku za wanadamu kwa njia ya kuathiri. Umuhimu huu wa lugha uliokubalika miongoni mwa washairi unaufanya ushairi kuwa

eneo maalum linalostahili kuchanganuliwa kwa kuizingatia lugha yake.

## 2.3. Semiotiki ya Ushairi

Nafasi ya lugha katika mawasiliano haiwezi ikakadirika. Umuhimu wake, kama nyenzo kuu ya kuibua maana kwa njia ya kisanaa, umedhihirishwa na wataalam tuliowanukuu. Lugha hii hujivimbisha kutokana na ala zake mbalimbali zenye uwezo wa kujiashiria. Hivyo basi, lugha ya kishairi inaweza kuangaliwa kama mfumo ambao unaweza kufumbua masuala mengi ya kijamii yaliyonakishiwa nayo. Umuhimu huu wa lugha unatuwezesha kuibuka na usomaji maalum wa kazi za kishairi.

Semiotiki ya ushairi inahusiana na jinsi lugha ya ushairi husika ilivyotumika kuibua maana. Lugha katika uchanganuzi wetu wa kisemiotiki ndiyo nyenzo ya kubebea jumla ya ishara ambazo washairi, akiwemo Abdilatif, wanazitumia katika kuwasiliana. Swala hili la mawasiliano linaturejesha kwa mfumo wa kitendo cha mawasiliano kama ulivyopendekezwa na Jakobson. Katika mfumo huo tunadhihirikiwa na jukumu la lugha ya kishairi katika tungo za Abdilatif.

Katika kitendo cha mawasiliano, Jakobson (Scholes 1974), anataja kuwepo kwa nguzo sita muhimu ambazo ni msingi wa kupatikana kwa maana ya usemi wowote. Katika shairi 'Kutendana', kwa mfano, tunapata <u>ujumbe</u> unaotoka kwa <u>mtumaji</u> wa ujumbe huo hadi kwa <u>mpokeaji</u>. Ujumbe huo unatumia <u>njia</u> (na hapa maandishi tunayoyasoma). Ujumbe huo unatumia <u>msimbo</u>, ambao katika muktadha huu ni lugha ya kifasihi. Fauka ya hayo ujumbe pia unatarajiwa urejelee <u>muktadha</u> fulani. Kipengele hiki cha

muktadha ndicho kinachobeba maana ambayo ingeelezwa kwa lugha ya kawaida. Ujumbe wenyewe, ambao unatokana na ile haja ya wanadamu kuwasiliana, yaani unaowaunganisha mtumaji na mpokeaji, unafanikishwa na nguzo nyingine sita.

Katika ujumbe wenyewe, kila nguzo ya mawasiliano hudhihirika kama jukumu linalojitahidi kuupatia maana usemi. Katika shairi 'Kutendana', kwa mfano, kuna ujumbe aina sita kutegemea nguzo husika ya mawasiliano. Ujumbe wa aina ya kwanza ni ule unaorejelea jambo lililo nje, kutegemea nguzo ya muktadha. Upo ujumbe ambao pia unatupatia fununu juu ya hisia za mtumaji (Abdilatif). Pia kuna ujumbe ambao jukumu lake ni kuivuta nadhari ya mpokeaji (msomaji). Ujumbe mwingine unahusiana na njia yenyewe ya mawasiliano (maandishi). Vilevile tunao ujumbe unaohusiana na kuutalii msimbo uliotumika kama vile ufafanuzi juu ya msamiati. Mwisho, kuna ujumbe ambao, unapotolewa hung'ang'ania kujisisitiza wenyewe. Kujisisitiza huku kwa ujumbe hulengwa kuzivuta nadhari za wasomaji kutokana na kutumikishwa kwa zana mbalimbali za lugha zikiwemo ruwaza za sauti, umbuji wa kisintaksia, taswira na ala nyinginezo. Hili ndilo jukumu la kishairi ambalo, aghalabu, limejibana na kazi za kisanaa.

Katika sura hii, tumeangalia kwa undani jinsi jukumu hilo la kishairi linavyotekelezwa na kuifanya lugha ya tungo ijiashirie na, hivyo basi, kuwa msingi wa maana. Tumeangalia uwezo wa lugha katika kutuibulia maana, kuhisi na kuipata tajriba ya maigizo katika tungo tulizozishughulikia.

## 2.4. Jukumu la Kishairi na Maigizo katika Tungo

Lugha ndicho chombo cha kimsingi cha mawasiliano katika tungo zinazoshughulikiwa. Tungo hizi ni ishara zinazoakisi mambo mbalimbali. Katika kiwango cha chini kabisa, tunazo ishara kutokana na umbo rasmi la tungo hizi ambalo mshairi amelizingatia. Kwa kuzitazama tu, tungo hizi zinamfahamisha msomaji wake kuwa anachoona mbele yake ni ushairi. Vina, urari wa mizani na vipande, vikiwa ni vipengele vya kirasmi ambavyo Abdilatif anavisisitiza katika kijelezi chake cha 'nini ushairi', vinaweza kutumika kuwa mwongozo wa kuubainisha ushairi jadi kutokana na ushairi huru. Umbo rasmi pia ndilo linalotumiwa na wanajadi kuzibagua bahari za tungo zao. Kwa mfano, kigezo cha vipande kinaweza kutumika kuitofautisha bahari ya wajiwaji yenye vipande vitatu kutokana na ile ya ushairi au utenzi. Vilevile, zipo beti ambazo washairi hawa, kwa mfano, huzitumia kutofautisha tarbia, toka kwa tasdisa.

Hata hivyo, umbo rasmi la tungo hizi si ithibati tosha ya kuiita kazi iliyotungwa kwa kuzingatia umbo hilo rasmi ushairi. Jambo hili analizumgumzia Senkoro anapotutolea utungo wenye umbo rasmi ingawa hauna mantiki yoyote. Utungo huo (Sekoro 1988: 12) unasema;

> Yakaenda na kwa rasi
> Na kukanda bila rasi
> Na mikanda kuiasi
> Hebu basi pigilia

Umbo rasmi pekee haliwezi likajenga maana ya shairi. Hili linatufanya tuangalie zana nyinginezo ambazo zinajenga kazi ya kishairi.

Abdilatif ametumia lugha ya kishairi. Lugha hii imesifika kutokana na uwezo wake wa kuzungumzia mambo mengi kwa muhtasari

kuliko lugha ya kawaida (Perrine 1990). Sifa hii si ya ushairi pekee kwani tanzu nyinginezo za fasihi kama vile riwaya na tamthilia vilevile hutofautiana na lugha ya kawaida. Uwezo huu wa ushairi katika kuzungumzia mambo mengi kwa muhtasari unatokana na matumizi ya zana mbalimbali za lugha kama vile taswira, metunumia, sitiari, tashbihi, kinaya na hata takriri. Ala hizi huupa ushairi uwezo wa kueleza kwa ufasaha masuala mbalimbali yanayoiathiri jamii.

Kutokana na sifa hii ya ushairi, ni wazi kwamba masuala mbalimbali yanayohusiana na maigizo yamesheheni katika ala hizi ambazo mshairi huyu amezitumia. Wasomaji watayamaizi masuala hayo kwa kuutafakari uzito na athari ya zana hizo katika ulimwengu wao wa maigizo. Haya yanajitokeza tunapotafakari kwa undani muumano uliopo kati ya lugha ya kishairi katika tungo hizi na uhusiano wake katika kutuhisisha maigizo.

### 2.4.1. Lugha ya Kishairi na Maigizo katika Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa

Kuhisika kwa maigizo ya utungo huu, kwa kiwango kikubwa, kumefanikishwa na zana za lugha. Abdilatif amejitokeza kama mwandishi stadi kupitia matumizi bora ya lugha. Ustadi huo unamulikwa na Chacha (1992), anaposema kwamba matumizi bora ya lugha ndiyo yaliyomwezesha mshairi huyu kuuwasilisha ujumbe wake kwa namna ya kueleweka na kuvutia. Upevu wa mwandishi huyu katika kuitumia lugha unazifanya tungo zake kuwa amali ya kijamii kama zilivyo tamthilia zote.

Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa ni thibitisho la upevu wa matumizi ya lugha katika nyanja za mawasiliano. Utenzi huu

umenakishiwa na zana mbalimbali za lugha zinazotusaidia kuyahisi maigizo kwa njia yenye mnato. Utungo huu unayapinga maoni yaliyotolewa na baadhi ya wataalam kwamba tenzi za Kiswahili huwa na lugha nyepesi. Shariff (Harrow ed. 1991), akiimulika lugha katika tenzi za Kiswahili, anasema kuwa ni nadra kwa bahari hiyo ya kiutunzi kutumia sitiari-pana au methali. Lugha ya tenzi, anaeleza, huwa sahili. Kauli hii, ingawa ina ukweli fulani kwa kuzingatia swala la methali katika <u>Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa</u>, si ya kiyakinifu tunapoangalia ala nyingine za lugha. Utenzi huu una ukwasi wa matumizi ya sitiari pana, taswira, tashbihi, kinaya, metunumia na zana nyinginezo za lugha kama vile takriri. Zana hizi zinashikilia nafasi muhimu katika maigizo na ni ishara thabiti zinazobeba maana. Wazo hili pia linaweka dhahiri nguvu za zana za lugha kama mifumo ashiriaji katika ulimwengu wa mawasiliano. Hiki ni kinyume na kauli ya Shariff inayodai kuwa tenzi huepukana na matumizi ya tamathali za usemi na badala yake kutumia lugha sahili kwa kuchelea kutatiza mawasiliano.

Lugha ya kifasihi, mbali na kutekeleza mawasiliano, hufanya hivyo kupitia lugha yenye mnato. Mawasiliano hunakishiwa, msomaji akiupokea ujumbe huku akiufurahia ustadi wa lugha ya mwandishi. Kwa kuzitumia zana mbalimbali za lugha, Abdilatif amefanikiwa kuwasiliana na hadhira yake kwa njia inayovutia zaidi; njia ya maigizo.

#### <u>2.4.1.1. Taswira</u>

Lugha ya Abdilatif inajitahidi kuziathiri hisi zetu zinazohusiana na milango ya fahamu ya kuona, kunusa, kuonja,

kugusa na kusikia. Hisi hizi ndio msingi wa taswira (Kahigi na Mulokozi 1979, Perrine 1988). Kwa kuzingatia tajriba zetu, zana hii ndiyo inayotuwezesha kuyaona maigizo kama mambo ya kiyakinifu katika maisha yetu halisi.

Katika utungo huu, Abdilatif ametilia maanani umuhimu wa mandhari ambayo hadhira yake inapasa kuiona kwenye jukwaa. Jukwaa hili si la kihalisia na linahitajia kujengwa kwa kuitumia lugha. Zana hii ya taswira inalifanikisha azimio hilo. Kwa kuitumia lugha, juhudi za Abdilatif katika kulijenga jukwaa zinathibitika. Mandhari hii katika beti zifuatazo (beti 161-168), ni sehemu ya juhudi hizo;

Nimeona mingi miti
Matundaye ni ladhati
Ulaini kitafiti
Kama siagi sikia

Tamu yake ni ya kweli
Yashinda zote asali
Alapo mtu muhali
Maisha kuona njaa

Muna na miti ya tembo
Na maziwa yaso chombo
Anywaye kijaza tumbo
Kiu hataisikia

Kadhaka muna majumba
Yenye vioo vyembamba
Sakafu zote na nyumba
Maridadi vyang'ariya

Milango na viambaza
Kwa nuru vinaangaza
Ndani yake yapendeza
Sifa imetengeneya

Kuna vitanda biyadha
Dhahabu tupu na fedha
Vyenye kuridhisha ridha
Kwa mwenye kuvilalia

Vitu vyote ni vizuri
Vimepambiwa johari
Yaliyomo majodori
Nuru njema hutokeya

Si joto wala baridi
Ilhaswili muradi
Huburudika fuadi
Mngia majumba haya

Beti nane hizi, ni mfano wa jinsi lugha ya taswira ilivyotumiwa kuyawasilisha mandhari ya peponi. Abdilatif anampeleka Hawaa matembezini: matembezi ambayo yanageuka na kuwa usimulizi wa mandhari.

Katika masimulizi haya, picha ya peponi inatujilia kwa kuwa lugha iliyotumika imelengewa baadhi ya milango ya hisi zetu. Masimulizi ya Hawaa ni juhudi za mwandishi za kuitumia lugha ya kuathiri hisia zetu ambazo, kulingana na tajriba yetu katika masuala ya kuhisi, zinatusogezea karibu zaidi picha anazojaribu kuzizalisha mwandishi.

Aghalabu kila ubeti unalengwa kuziathiri hisi zetu. Beti mbili za mwanzo, kwa mfano, zinatumia hisi za kuonja na vilevile za kuona. Tunaiona miti mingi ikinawiri huko peponi na matunda yaliyo tamu. Hisi za kuonja zinaletwa karibu zaidi na mfano wa asali, chakula ambacho tunakifahamu vyema. Beti tano zinazofuata zinatuingiza peponi kwenyewe na kuona miti ya tembo, maziwa, majumba yenye vioo vyembamba, milango na viambaza vinavyong'ara, vitanda vya dhahabu na fedha, na majodori. Tunaiona pepo iking'ara. Ubeti wa mwisho unaishirikisha hisi ya kugusa ambapo tunaihisi hali isiyokuwa ya baridi wala joto.

Katika beti nane pekee, nguvu za taswira tunaziona. Hisi za kuona, kuonja na kugusa zinatumiwa. Abdilatif anafanikiwa, kupitia kauli anazompatia Hawaa, kutuumbia ulimwengu wa peponi, kwa kuitegemea tajriba yetu ya kuhisi.

Mandhari hii, ingawa si ya kweli na ngumu kuwasilishwa kwenye jukwaa halisi, inayumkinika hivyo katika fikra zetu.

Tunaona katika fikra zetu mapambo anayozungumzia Hawaa. Lugha ya kitaswira anayoitumia Hawaa inatusawiria mandhari yote ya peponi.

Tamathali hii pia inatuonyesha jinsi baadhi ya vitendo vya maigizo vinavyotekelezwa. Msimulizi, kwa mfano, anatusawiria kwa kirefu jinsi Adamu na Hawaa wanavyolila tunda. Tunaelezwa (ubeti 368);

> Pamoja wakachutama
> Baba na mwenziwe mama
> Penye mti wa harama
> Matunda wakajilia

Baadaye (ubeti 369),

> Adamu kuja simama
> Aona kijitazama
> Asijione salama
> Uchi hana nguo moja

Katika beti hizi, Msimulizi anaeleza kuwa matunda hayo yaliliwa huku wahusika hao wakiwa wamechutama.

### 2.4.1.2. Sitiari na Tashbihi

Tumeziweka tamathali hizi pamoja kwa kuwa zinaingiliana na zote zinazingatia uhusiano wa vitu viwili ambavyo ni tofauti kimaumbile lakini vinavyounganishwa na sifa kuu kati yake (Perrine 1988).

Zana mbili hizi za lugha zimetumiwa kwa ustadi na Abdilatif katika kuyafanikisha maigizo yake. Umuhimu wao katika maigizo unatokana na sifa zao za kuruhusu kule kuwepo kwa uhusiano wa vitu viwili ambavyo ni tofauti kimaumbile na kitabia. Mvuto na hatimaye ulaji wa tunda haramu, kwa mfano, unatuelea vyema kwa kuzitafakari tashbihi ambazo mwandishi anazitumia. Tunaelezwa (ubeti 317);

Akaliona ni zuri
Ja siagi tiritiri
Jepesi kama hariri
Tunda lilivyolegea

Tunavyofahamu, tunda haramu kama linavyoelezwa kwenye misahafu ndilo linalowatoa Adamu na Hawaa peponi. Kwa hali yoyote iwayo, uamuliwaji awali wa wahusika hawa kungewaongoza katika kulila tunda. Maigizo haya, mbali na kutupasha habari, yanafanya hivyo kwa njia yenye mvuto.

Abdilatif, akiwa na ari ya kuivuta hadhira yake, anatumia tashbihi ambayo itatufanya tusiuhukumu uasi wa Adamu na Hawaa bila kuupima uzito wa ushawishi unaowakabili. Ndipo tunda likafananishwa na siagi na hariri. Siagi, kama tunavyoifahamu ni nyororo tena tamu. Hariri nayo ni nyepesi na yenye thamani. Kwa kuingizwa katika ulimwengu mpana wa mavazi na vyakula tunavyovifahamu vyema, uzuri wa tunda na ushawishi unaofuatana na tunda hilo unatufikia barabara. Hadhira, kupitia zana hii ya lugha, inayafahamu makosa ya Adamu na Hawaa; yakiwa ni matokeo yanayosababishwa na mazingira yao.

Kauli ya Shariff (1991), kuwa tenzi za Kiswahili ni nadra kutumia sitiari-pana, inakosa mashiko kwa kuzingatia maigizo haya. Sitiari-pana, zikiwemo ishara na istiari, ni miongoni mwa zana za lugha ambazo zimetumika na kuchangia kuhisika kwa maigizo. Mfano mzuri tunaupata kwa kuwazingatia wahusika katika maigizo haya.

Wahusika wametumika kama viwakilisho vya kiishara katika maigizo haya. Adamu na Ibilisi, kwa mfano, wametumika kiishara - wakiwakilisha wema na ubaya; Malaika wakisimamia utiifu; Hawaa kwa upande wake anaweza akasimamia ule ukosefu wa msimamo maalum. Kulingana na matendo yake, mhusika huyu haamini anachoambiwa na

Mungu (ubeti 151), wala Adamu. Mara tunamwona akiahidi kutozungumzia habari ya matunda ya mti wa haramu. Ishara hizi zinatokana na usanifu wa hadhira inayoshuhudia maigizo haya.

Mbali na kutumika kiishara, wahusika hawa wametumika kiistiari. Wahusika hawa ni viwakilisho vya matendo ya makundi mbalimbali katika jamii. Yupo Ibilisi, kwa mfano, ambaye uhusika wake unaranda katika dira ya kuwafarakanisha Adamu, Hawaa na Mungu. Vitendo vyake ni fumbo la maisha katika jamii halisi zilizokithiri fitina. Akina Ibilisi ni wengi hadi leo. Wao daima wamo mbioni kuwavunjia wengine unyumba wao, urafiki na wakachukia lolote ambalo litawapa ufanisi wanadamu wengine. Adamu naye ametumiwa kusawiri kaumu ya watu waadilifu ambao huwa na kasoro zao. Pamoja na kujitokeza kama mtu anayemcha Mungu, uanadamu unamwandama na kumtia doa. Ukamilifu wa waja unatiliwa shaka na uhusika wa Adamu. Binadamu katika urazini wake, ni kiumbe anayezingirwa na kasoro mbalimbali. Adamu anawakilisha baadhi ya mambo muhimu katika jamii, hususani makosa ambayo kila binadamu anayatenda. Wafuasi, kutokana na swala hili, hawastahili kuyaajabikia baadhi ya makosa yanayotendwa na viongozi wao kwani kila binadamu ana kasoro. Ukamilifu ni wa Mungu pekee.

Kunajitokeza pia dhana ya uhuru wa kimawazo ambao mhusika Hawaa anajaribu kuuwasilisha. Hawaa ndiye anayekuwa mwanadamu wa kwanza kudadisi mambo ambayo hayamwelei vyema. Haoni haja ya kufuata amri ambazo hazijui hekima zake. Msimamo wa Hawaa wa kutafiti zaidi katazo la kula matunda ya mti wa haramu ni kiwakilisho cha uhuru wa kudadisi mambo ulioenea kila pembe hapa duniani. Mbali na hilo, Hawaa anakuwa mwanadamu wa kwanza

anayejaribu kuzingatia masuala ya kiujumisia, kwa kuukana ulimwengu wa wanaume na kufanya lile analoona ni bora kwake. Juhudi hizi za suala la uana zinaendelezwa hadi leo.

Mungu, hasa kwa kuyazingatia matendo yake, ni kiwakilisho cha nguvu za kisiasa. Aghalabu kila serikali, huweka katiba ambayo, inatarajia itakuwa mwongozo wa utawala wake. Wananchi wanatakiwa wazitii katiba zao. Matendo ambayo ni kinyume na matarajio ya katiba husika hukutana na nguvu za kisiasa. Mungu, akiwa ndiye bwana wa viumbe wote, hasiti kuweka wazi mikatale yake. Adamu na Hawaa wanapoiasi wanakutana na anguko lao. Hatima kama hiyo ya kuivunja amri ya Mungu inamkuta Kabili anapomwua Habili. Ndugu hawa wawili pia ni kiwakilisho cha uhasama sio tu baina ya ndugu na ndugu bali hata ukoo na ukoo, kabila na kabila, nchi na nchi na uhusiano mwingine unaoambatana na mgawo kama huu.

Sitiari pana hizi, tunapozichungua kwa makini, tunaziona kama mifumo ashiriaji ambayo inatusaidia kuelewa ujumbe wa mwandishi. Kwa kufahamikiwa na ujumbe, maigizo haya tunayahisi yakijadili masuala nyeti katika jamii zetu. Mawanda ya fikra zetu yanapanuliwa kwa kuzitafakari sitiari hizi. Mungu, Adamu, Hawaa, Ibilisi na wahusika wengineo kama vile Kabili na Habili tunawahisi wakiwa wahusika wa kimataifa badala ya kuwatazama katika ufinyu wao wa maigizoni.

#### 2.4.1.3. Metunumia

Metunumia ni dhana ambayo kwayo sehemu fulani ya kitu hufanywa isimamie kitu kizima chenye uhusiano nacho. Katika muktadha huu neno 'kitambi' linaweza likasimamia utajiri (Kahigi

na Mulokozi 1979).

Kwa kuzingatia suala la mapenzi na wivu unaoandamana na mapenzi kati ya Adamu na Hawaa, tunamwona kila mmoja akitumia mbinu yoyote kuhakikisha mapenzi ya mwenziwe. Adamu anafahamu barabara kuwa mkewe ni mzuri wa sura. Abdilatif anampa Adamu kauli ya kimetunumia kuueleza uzuri huo. Adamu (ubeti 323) anasema;

Ewe siti wa masiti
Usidhani nacha mti
Namuhofu Jabaruti
Yake aloniusiya

Hawaa anakuwa 'siti wa masiti' tamko ambalo Adamu analitumia kama heshima kwa Hawaa. Kauli hii inasimamia dhana ya uzuri kama unavyomdhihirikia Adamu. Tamko hili ni kichocheo kwa wasomaji kuutafakari uzuri wa kiupeo alionao Hawaa. Adamu anatufungulia moyo wake pia juu ya penzi lake kwa mkewe. Kinachotutanza ni iwapo Adamu tayari alikuwa amefahamu wanawake wengine humo peponi hadi akafikia uamuzi kuwa Hawaa alikuwa '...siti wa masiti'. Pengine alikuwa akiupima uzuri wa Hawaa na mahurulaini waliokuwa wakimea mtini.

2.4.1.4. Takriri

Umuhimu wa ala hii ya lugha unaelezewa na Kuhenga (1977) kuwa una azma ya kutia nanga jambo fulani ili liweze kumwingia msikilizaji moyoni apate kulidhibiti vizuri. Abdilatif, akiwa na haja ya kuyanawirisha maigizo haya, anafanikiwa kulifikia lengo hili kupitia lugha ya kishairi ambayo ina sifa mbalimbali za matumizi ya takriri. Takriri hizo ni pamoja na takriri vina na takriri neno.

### 2.4.1.4.1. Takriri Vina

Hii ni ala ya kishairi ambayo inatumiwa kuzivuta hisi zetu tunapousoma utungo huu. Zana hii inaibua mahadhi fulani hususani ya kimziki kulingana na hali iliyopo. Kipengele hiki kinamwezesha msomaji azingatie ujumbe wa utungo wenyewe huku akistaladhi ushairi. Vina vya utenzi huu vinabadilika isipokuwa katika beti chache. Lengo kuu ni kumfanya msomaji asichoshwe, hasa kwa kuuzingatia urefu wa utenzi huu.

Wakati mwingine, mshairi anaendeleza maneno kwa namna ambayo yataingiliana na utaratibu wa vina bila ya kuipotosha maana iliyokusudiwa. Kwa mfano, Msimulizi (ubeti 64) anasema;

> Tena sio <u>wakinzano</u>
> Kwa Mungu hawana neno
> Yake huunga mkono
> Kwa mtakaso wa niya
>
> (Msisitizo ni wetu)

Neno 'wakinzano' limechukua mahala pa neno 'wakinzani'. Mshairi ameutumia mwendelezo huu ili adumishe kina husika.

### 2.4.1.4.2. Takriri Neno

Katika maigizo haya, tamathali hii inajitokeza vizuri zaidi katika majadiliano ya Hawaa na Ibilisi. Wakati huu, Hawaa anakutana na 'shoga' huyu ambaye anataka kufahamu iwapo Hawaa alifanikiwa kumshawishi Adamu kula matunda ya mti wa haramu. Hawaa (ubeti 263) anajibu;

> Hataki thama hataki
> Hataki kuniafiki
> Hata kwa kutarazaki
> Mti ameususiya.

Kauli hii inasheheni matumizi ya neno 'hataki' kuashiria ugumu wa Adamu katika kuikiuka amri ya Mungu. Msisitizo huu kwa msomaji unatoa mwanga na kumtilia nanga maono ya Adamu kuhusiana

na mti huo. Tamathali hii vilevile inatujengea taharuki ya kutaka kufahamu iwapo njama zinazopangwa katika mkutano huu wa Hawaa na Ibilisi zitaambulia lolote hapo baadaye.

Ibilisi anapozipata habari hizo anaitumia takriri hiyo hiyo. Anasema (beti 264-265);

Kwani mumeo ujuzi
Hataki muwe walezi
Ili muwe na kizazi
Jamaa kuendeleya?

Au mumeo Adamu
Yeye hataki kudumu
Kwa mti wenye elimu
Na anasa maridhiya?

'Hataki' hiyo hiyo ndiyo inayotumiwa na Ibilisi kumlainishia Hawaa kuendeleza mapambano ya kulifikia lengo lao. Msisitizo anaoutumia Hawaa ndio unaoutumiwa na Ibilisi kumsisitizia haja ya kutia migati ili Adamu alile tunda.

Neno 'hataki' linatumiwa kutuandalia mapambano makali yatakayojiri kati ya Adamu na Hawaa ambayo yanajitokeza katika kitendo kinachofuata.

### 2.4.1.5. Uteuzi wa Maneno katika Mishororo

Mbinu hii ya kishairi inahusiana na jinsi mshairi alivyoyateuwa maneno yake katika baadhi ya mishororo. Abdilatif ameyateuwa maneno ya utenzi huu kwa namna ambayo inaikweleza hali iliyopo ya drama. Katika uteuzi wake wa maneno, mshairi anachagua neno moja kutokana na jumla ya msamiati uliopo unaoeleza dhana moja. Hoja hii inaelezwa vyema na Msimulizi (ubeti 44) anaposema;

Kwa Mola yake karama
Uhai aliosema
Adamu kumgandama
Kweli ukamueneya (Msisitizo ni wetu)

Uteuzi wa maneno haya uliofanywa na mshairi unaupatia utenzi huu sifa ya kuwa drama. Mshairi alikuwa na mwanda mzima wa maneno, kama vile 'kumjilia', 'kumthubutikia' na hata 'kumzukia', ambayo yangetumika mahala pa 'kumgandama'. Neno hili linasadifu vyema hali iliyopo ya uhai kumjilia Adamu mara moja. Uhai unafanywa uwe mfano wa kitu ambacho hakimpatii Adamu nafasi ya kupumua. Baada ya uhai kumgandama, tunaelezwa kuwa '...Kweli ukamueneya'. Neno 'ukamueneya' limeteuliwa kwa minajili hiyo hiyo, ya kueleza tukio hilo kidrama. Maneno kama vile 'kila mahali' na 'ukawa mote' yangetumika. Hata hivyo, kufanya hivyo kungeupunguza utamu wa kishairi. Ni lazima tufahamu kuwa Abdilatif anatumia ushairi jadi ambao lazima uhifadhi vina. Neno 'kumgandama' linatimiza, sio lengo la vina pekee, bali pia kueleza hali iliyopo kidrama.

2.1.4.6. Mpangilio wa Maneno katika Mishororo

Ala hii ya lugha imetumika kuuwasilisha utenzi kwa njia ya kimaigizo. Mshairi ameitumia mbinu hii kwa kuuzingatia uhusiano wa mfululizo wa maneno (horizontal relationship). Mpangilio wake haufuati kanuni zinazokubalika za kisintaksia, isipokuwa katika maandishi ya kisanaa tu. Kwa mfano, hutokea mshairi akatanguliza kiarifa kielezi, au kivumishi kabla ya kitenzi. Msimulizi (ubeti 103) anatudokezea kutoka kwa Ibilisi peponi;

> Ibilisi kwa kinyongo
> Atoke upande shingo
> Amefutika kijongo
> Huyo akatokomea
>
> (Msisitizo ni wetu)

Mshairi hapa anatumia mpangilio ambao, mbali na kutimiza matakwa ya urari wa vina na mizani, unajaribu pia kuwasilisha hali

iliyopo kidrama. Hali hiyo ya kidrama inajiri kutokana na msisitizo unaotokana na mpangilio huo wa kisintaksia usiokuwa wa kawaida. Laiti angetumia 'Atoke shingo upande' mshororo huu ungeshindwa, sio katika kutimiza vina tu, bali pia ungepoteza udrama wake.

Kipengele hiki cha lugha tunakiona pia akikitumia Adamu anapombembeleza Hawaa. Anapokabiliwa na madai ya kutaka kujiolea mke mwengine, Adamu (ubeti 183) anasema;

> Muhibu usishituke
> <u>Sina mwenginewe mke</u>
> Hawaa sidhalilike
> Poa moyo kutulia
> (Msisitizo ni wetu)

Mshororo huu unatuvutia zaidi kwani tunauhisi uzito wake wa kubembeleza. Badala ya 'Sina mke mwenginewe', mshairi anautumia mpangilio huu ili aiendeleze hali ya udrama katika utenzi wake.

<u>2.4.2. Lugha ya Kishairi na Maigizo katika 'Kutendana'</u>

Katika maigizo haya, zana mbalimbali za lugha zimetumika kuikweleza athari inayoistahili kazi ya kidrama.

<u>2.4.2.1. Taswira</u>

Miongoni mwa taswira zinazojitokeza katika maigizo haya ni ile inayomhusu Mwanamke. Aghalabu Mwanamke huwa anapewa nafasi duni katika jamii. Picha ya Mwanamke wa maigizo haya ni tofauti. Maigizo haya yanayohusiana na kutendana yanamchukua Mwanamke kama nguli wake, yaani mtendaji.

Kitendo cha mchezo huu, kama tutakavyoeleza hapo chini, kinajitokeza katika viwango viwili. Kiwango cha kwanza ni kitendo kilichowahi kutokea. Katika kiwango hiki, Mwanamke ndiye

aliyekuwa mtendwa: akiichukua nafasi ya mume na mke nyumbani huku Mwanamume akiwa ameridhika na kumnyonya mwenzake. Ilimbidi Mwanamke ajikakamue kuzikidhi haja za Mwanamume hadi yakamfika ya kuziuza nguo, licha ya madeni yaliyomkodolea macho. Tija ya yote hayo ikawa ni kutorokwa.

Kiwango cha pili, na ambacho ni kitendo kilichopo cha 'Kutendana', Mwanamume anarudi tena baada ya miezi. Anachotarajia Mwanamume ni kutimiziwa haja yake huku akijilizia mapenzi. Hoja kwamba aliwahi kuishi na huyu bibi inakuwa sababu ya kuamini kwamba ataupata mradi wake. Matarajio yake hayafani. Mwanamke aliyemjua si huyu tena.

Mabadiliko haya ya kisilika yanakuwa nyenzo ya kutueleza mwelekeo mpya ambao Abdilatif anatuelezea. Nyakati hazipo tena za kuafiki kila wanaume wanachotaka. Hayo ni mambo ya zamani ambayo tajriba ya Mwanamke inajaribu kutueleweshа. Idhilali na mateso yaliyomsibu yameugeuza moyo wake na kuuona mwanga. Mwanamume ameingia mashakani kwa kumfumbua macho aliyemdhania bado amelala. Chambilecho Mwanamke mwenyewe / Mato unnifumbuwa, ya wazi sasa yaona.../.

Taswira hii, kwa ujumla, inadokezea pia uwanja mzima wa maonevu ambayo hutendewa watu hadi ikafika muda ikawa maovu hayo yamewachachukia wanaoonewa. Taswira hii inaweza kuwa onyo kwa viongozi ambao huamini kuwa wanafahamu zaidi kuliko mtu yeyote katika jamii. Ipo siku ambapo maonevu yao yatawafikia kooni wafuasi wao. Siku hiyo itakuwa ya viongozi hao kutiwa hekahekani wawe waombaji kama alivyo Mwanamume katika maigizo haya. Vilevile, wafuasi, ambao wanaonekana kama watu wa 'ndiyo bwana', watachoka na kuamua kuwa mawazo yao yana haki ya kuheshimiwa kama

ya mtu yeyote katika jamii.

2.4.2.2. Sitiari

Mgongano katika maigizo haya una misingi yake katika uchu uliokithiri wa Mwanamume. Uchu huu ni wa kiupeo. Dhana hii ya uchu uliokithiri inabidi ielezwe kwa mbinu ambayo itaipeleka hadhira kuutafakari upeo wa uchu huo. Hivyo basi, tunaona matumizi ya msamiati ambao umetapakaa katika shughuli zetu za kila siku. Hata hivyo, tajriba yetu ya maneno hayo inatupelekea kuihamisha maana yake kulingana na muktadha unaozungumziwa. Kwa kuyateuwa maneno hayo, mwandishi anajaribu kutufanya tuuingie kwa uketo ulimwengu wa maigizo yetu na kumwona Mwanamume akifadhaika kutokana na uchu wake.

'Pepo', 'dawa' na 'mwako', ni baadhi ya sitiari ambazo mwandishi amezitumia kuipanua dhana yake ya uchu. Taaluma ya uganga inatumiwa kulifikia lengo hilo. 'Pepo', ambao tunawafahamu kama viumbe wanaowafanya watu wapagawe aula wapungwe, wanatumika kutuelezea kiwango cha uchu uliomsibu Mwanamume. Ilivyo, ni kukirimiwa tu ambako kungeufanya uchu huo kupungua.

Mbali na sitiari ya 'pepo', kunaingizwa pia 'dawa' ambayo ndilo tumaini la mgonjwa. Aghalabu ni 'dawa' ambayo inatumika katika kuwatibu wagonjwa. Kuwanyima wagonjwa dawa ni sawa na kuwauwa polepole. Kwa kujiweka katika kundi la wagonjwa ambao kifo kinawasubiri iwapo itakuwa muhali kuipata dawa, Mwanamume anaitoa kikamilifu picha ya uhitaji wake kwa muda huu.

Vilevile, dhana ya 'mwako' ina nguvu za kimawasiliano hasa tunapozingatia kwamba uchu unafananishwa na moto unaounguza ndani

kwa ndani. Uzito wa ujumbe unaobebwa na dhana hizi haufui dafu kwa Mwanamke ambaye bado anayakumbuka mateso aliyoyapata hapo awali.

Zana hii ya lugha, hususani kwa kuizingatia mifano tuliyoitoa, inathibitisha uwezo wake wa kuizamisha hadhira na kuutafakari ujumbe unaowasilishwa.

<u>2.4.2.3. Takriri</u>

Zana hii ya lugha inajitokeza pindi tu maigizo yanapoanza na kuifanya hadhira waitafakari umuhimu wake. Mbali na takriri vina, tuna takriri za maneno na vilevile takriri za kibwagizo.

<u>2.4.2.3.1. Takriri Neno</u>

Hali iliyopo ni ya mkinzano. Pande mbili zinazokinzana, yaani Mwanamke na Mwanamume, ni sharti zidhihirishe hilo. Takriri hizi zinakuwa nyenzo ya kuvipandisha viwango vya mkinzano na vilevile kuyapatia uhai maigizo hasa kwa kuzingatia ule udrama ambao zana hii inauzalisha. Miongoni mwa takriri hizo, takriri 'sina' inatia fora. Neno 'sina', kwa mfano, linakuwa neno linalozua hisia masikioni mwa Mwanamke. Neno hilo linamuathiri kiasi cha kulirudiarudia mara nne katika ubeti mmoja pekee. Takriri hii inatufanya tuwaze lile ambalo mhusika Mwanamke ametendewa kiasi cha kukirihiwa na neno kama hili. Makini ya hadhira inanolewa na kufanywa iwe chonjo kuona lile litakalojiri.

Baadhi ya mambo yanayotufungukia kutokana na takriri hii ni hoja kwamba 'sina' kwa Mwanamume imekuwa wimbo aliokuwa akiuimba kwa muda mrefu hadi ukawa hauna thamani kwa Mwanamke. Takriri hii, hivyo basi, ni kidokezo cha silika ya Mwanamume ambayo

hadhira inaingoja ijidhihirishe malumbano yao yanaponoga.

Takriri ya 'sina' inafuatilizwa na takriri nyinginezo. Hadhira haitashindwa kugundua kwamba takriri hizi zina ruwaza maalum. Ruwaza hiyo inatokana na Mwanamume kutamka neno ambalo linatumiwa kumpwaguzia. Maneno kama vile 'mwako', 'pepo' na 'dawa' anayoyatumia Mwanamume kuelezea shida iliyomkaba, yanakutanishwa na maelezo yaliyojaa kebehi toka kwa Mwanamke. 'Pepo' aliyemo kichwani anayemzungumzia Mwanamume amegeuzwa na kufafanuliwa kama 'pepo' duni ambaye Mwanamke hawezi kumpunga. Matumizi ya takriri hizi yanaupa nguvu ujumbe wa kidrama ambao mshairi huyu amekusudia kuuwasilisha.

Matumizi ya takriri, vilevile, yanaashiria udhati wa nafsi kwa upande wa Mwanamke. Suala la kumkatalia mbali Mwanamume si jambo la kufanyiwa masihara. Mwanamke keshaamua kwamba hataki tena kujiingiza katika uhusiano wowote na huyu bwana. Zana hii inakuwa njia aula ya kuelezea msimamo huo. /...Nnatoka nitokako.../ ya Mwanamume inageuzwa na bibi huyu na kuwa /...Rudi kuko utokako.../. Jawabu hii inakuwa na makali yanayozidishwa na muambatano wa kukaririwa kwa neno 'nitokako' dhidi ya 'utokako'. Fauka ya hilo, kuna pia takriri ya silabi '-ko' ambayo vilevile inauchangia uzito uhusika wa Mwanamke usioafiki upuuzi katika jawabu yake.

#### 2.4.2.3.2. Takriri Kibwagizo

Mwanamume anawahi kutamka kuwa Mwanamke kashikwa na tamaa. Hili, anavyosema, ndilo linalomfanya Mwanamke ageuze nia ya kurudiana na Mwanamume. Shtaka hili linamtia uchungu Mwanamke. Anaorodhesha masumbufu mbalimbali yaliyomsibu; ya kumlisha na

kumstarehesha Mwanamume, kumpa pesa za matumizi, na ya kuuza nguo zake ili alipe madeni wakati bwana huyo alipomtoroka. Uchungu wote huu unasisitizwa na swali, ambalo pia ni kibwagizo: /...Vipi wanambiya kisha, tamaa innishika? /. Mwanamke analikariri hili katika beti tisa (uk. 95-96).

### 2.4.2.4. Mahadhi (Ridhimu)

Mahadhi hapa yanarejelea mapigo ya sauti ambayo yanajitokeza kwa mpango maalum. Mahadhi huenda yakawa ya kasi au ya polepole (Hall 1987, Kahigi na Mulokozi 1979). Lengo kuu la kuitumikisha mbinu hii huwa ni kueleza hali iliyopo; ya woga, wasiwasi, hali ya kufurahi. Mahadhi sharti yafungamane na maudhui husika. Katika maigizo haya, mshairi ameitumia mbinu hii kwa madhumuni mbalimbali. Kwa mfano, Maelezo (uk. 103) yanatufahamisha;

> Zilikuwa zishapita, saa tano za usiku
> Ni hapo alipokata, shauri la kuja huku
> Dirisha akaligota, Ku! Ku! Ku! Ku! Ku! Ku! Ku! Ku!
> Ili bibiye kumwita, kwa kubwa mno shauku

Tunaona kuwa kipande kizima cha mshororo wa tatu kimejengwa na silabi moja tu. Hili si jambo la kisadfa kwani mshairi ana lengo fulani la kufanya hivyo. Mahadhi yaliyopo yamezidishwa kasi. Kama wasomaji, tunahisishwa ugongwaji wa dirisha kwa nguvu na silabi / Ku /. Mahadhi haya yanahisika, sio kwetu wasomaji tu, bali hata kwa Mwanamke ambaye tunaelezwa (Maelezo uk. 104);

> Ndipo hapo kusikiya, dirishale la chumbani
> Hakuwa yakimweleya, aligotaye ni nani
> Papale akabakiya, hakutukutika sini
> Wala kusema ngojeya, au hivyo mathalani

Hali hii ya wasiwasi imemsibu Mwanamke. Hisia kama hiyo imekuzwa kwa hadhira ya wasomaji kupitia mahadhi yanayoibuliwa na kipande cha mshororo huu.

### 2.4.3. Lugha ya Kishairi na Maigizo katika 'Mnazi: Vuta N'kuvute'

Katika maigizo haya, lugha iliyotumika inajikita katika malumbano ya wahusika tu. Wahusika hawa wanavutana; kila upande kati ya Alii na Badi ukijaribu kuupiku mwingine. Lugha yao, vilevile, inaufuata mkondo huu wa vuta nikuvute iliyopo. Abdilatif ametumia zana mbalimbali za lugha zinazojaribu kutumulikia kiini cha mzozo kati ya kaka hawa wawili.

#### 2.4.3.1. Nafasi ya Tashibihi

Tashibihi zinazojitokeza katika maigizo haya zina lengo la kuweka wazi zaidi dhana na athari ya mvutano uliopo kati ya Alii na Badi. Kwa kuitumia tamathali hii, Abdilatif anaunakshi na kuupatia mgongano wa wahusika hawa mvuto wa kisanaa. Hadhira, kwa mfano, inaingizwa katika mgogoro uliopo kuhusiana na mnazi. Mnazi huu, tunaelezwa na wahusika wenyewe Alii na Badi, kuwa hapo mwanzoni ulikuwa wa shirika. Ushirika huo uliendelea hadi Alii alipoona hangeweza kuvumilia kupunjwa pato lake la mnazi. Badi pekee alikuwa akiufaidi mnazi kwa kulichukua fungu kubwa. Badi anakiri alimgawia Alii /...dogo fungu.../ ambalo analaumu /...uliona ni vizuri, kichache kutokubali.../.

'Ukubwa' na 'udogo' wa fungu ni mambo yanayoiacha hadhira gizani. Fungu analopewa Alii, kwa mfano, halifahamiki udogo wake uliomfanya Alii kuukatalia mbali ushirika wao. Fauka ya hilo, usemi wa Badi kuwa /...Ni heri nusu, kuliko shari kamili/ unatutia mushkili juu ya kile alichokuwa akipata Alii. Mkururo wa maswali yakiwemo ya 'fungu dogo ni lipi' na 'linafanana na nini' yanapitia kwenye bongo zetu. Kitu cha kufananisha fungu

dogo kinahitajika. Kwa ustadi, Alii anajaribu kutueleza fungu alilokuwa akipewa;

Fungu ulo ukinipa, wakati unapogawa
Sababu iliyonipa, hakataa kutukuwa
Ulikuwa kinikopa, ukinipa kama dawa
Hali tuna haki sawa
(Msisitizo ni Wetu)

Dawa, katika tajriba zetu ni kifaa cha kuponyea maradhi. Kifaa hiki aghalabu hutolewa kwa kipimo kidogo na tabibu. Mathalani, tunaposhikwa na homa, vidonge vinne vya malaria, ambavyo hupungua na kuwa viwili, hutosheleza kupambana na viini vya maradhi hayo. Tajriba ya hadhira kuhusiana na dawa inatumiwa kuutafakari uonevu aliotendewa Alii. Fungu la Alii ni mwengo wa mfano wetu na dawa; vikianza na vidonge vinne na kupungua kufikia viwili. Alichogawiwa Alii kilikuwa kichache mno ambacho, kwa sasa, ni nusu ya kichache hicho alichokuwa akipata kuzikidhi haja zake.

Ghadhabu za Alii anapoikumbuka dhuluma hii inaeleweka kwa hadhira. Kupewa fungu dogo kwa kile ambacho ni haki kwake si jambo la kuridhisha. Ndipo Alii anapotamka kuwa atatumia nguvu zake /...japo kwa ya ghali bei.../. Alii amefikia kikomo na stahamala zimejibari.

Kulingana na Badi, Alii ni mbobokwaji, kwani anamuona akitoa mambo ambayo kwake yangestahili kuhifadhiwa moyoni. Badi anaeleza kuwa mtendaji huwa haupotezi muda wake kueleza dhamira ya kitendo chake. Upangaji wa mambo ya kihujuma kwa maoni ya Badi si mambo ya kutangazwa hadharani. Mambo hayo ni ya kuzimwa - hadi siku ya kuanguka kwa zani lenyewe. Wakati wote, mtendaji /...Hutuliya kama maji, yaliyomo mtungini.../. Tashibihi hii inatuwekea bayana maana kwa kuufananisha ukimya na maji yaliyomo mtungini. Mtungi ni kifaa kinachofahamika barabara miongoni mwa

jamii za kiafrika. Shughuli zake za kuhifadhia maji na kuyafanya baridi si ngeni. Mtungi, hivyo basi, unakuwa nyenzo ya mawasiliano inayoeleza jinsi shughuli za kiunyama zinavyotekelezwa.

Kulingana na Alii, ufumbataji wa dukuduku linalomsakama mtu ni ishara ya uoga. Matumizi ya nguvu anayoahidi ni suala litakalomwathiri Badi. Anachotekeleza ni ada ya kibinadamu tu ili waja wengine wasije wakamlaumu kwa kutomtahadharisha mapema Badi. Kwa kufanya hivyo anatarajia Badi atakaa akifahamu kwamba /...iko siku...kujulikane bayana/. Kuoteana, kwa maoni ya Alii, si jambo mwafaka. Picha hiyo ya kuoteana inawekwa wazi kwa hadhira na usemi kuwa;

> Ni ya woga tabia, hiyo usemayo wewe
> Shujaa humwambia, mvita wake ajuwe
> <u>Hendi kumuoteya, ja kifaranga na mwewe</u>
> Kama usemavyo wewe
> (Msisitizo ni wetu)

Kifaranga anapolinganishwa na mwewe hatimii kamwe sudusi ya nduli huyu. Lakini mwewe, kutokana na maumbile yao, huamua kujinyakulia, tena kwa kuotea, vifaranga wasiotuhumu hatari. Mwewe hushuka kwa kasi ya kufumba na kufumbua na hivyo basi kuwanyima fursa vifaranga hao kujitafutia maficho. Ghafla, vifaranga hujikuta katika makucha ya nduli hawa ambao bila huruma huwararua miili yao kwa azma ya kuwala.

Tashibihi ya kuoteana kama kifaranga na mwewe inaeleza kwa uwazi hulka za baadhi ya watu madhalimu, wakiwemo viongozi, wanavyowatendea watu wasiokuwa na hatia. Alii hapendelei hilo kwa mhiniwa wake. Anajitokeza wazi, akionyesha ghamidha na kariha iliyomsukuma kujidaia kilicho chake.

Tashibihi hizi, kwa namna tulivyozitolea maelezo, ni nyenzo

mwafaka za jinsi zana hii ya lugha inavyoufumbata uwezo wa kumpa msomaji hisi ya maigizo. Wahusika, kwa kutumia tashibihi zinazoeleweka kwa hadhira, wanayafanya maelezo haya kuhisika zaidi.

### 2.4.3.2. Sitiari

Nguvu za sitiari, kama ala ya lugha inayoweza kufumbata dhana pana kwa kutumia neno moja, inajitokeza katika maigizo ya 'Mnazi: Vuta N'kuvute'. Mnazi, kwa jinsi ulivyotumiwa kisitiari, unakuwa mhimili wa maigizo haya yanayotendwa na Alii na Badi.

Umuhimu wa mnazi katika dira ya maisha ya wakazi wa eneo la upwa si suala la kimjadala. Nassir (1974) anatoa baadhi ya matumizi mbalimbali ya mnazi, yakiranda katika maeneo ya uchumi, kijamii na hata kitamaduni. Katika mti huo kunapatikana vyakula, dawa, pato la kifedha na hata vifaa vya michezo kwa watoto. Muhimu zaidi katika mti huu ni nazi; matunda ya mnazi ambayo Badi na Alii wanayang'ang'ania.

Uteuzi wa mnazi kama kifaa cha mvutano uliopo kati ya wahusika hawa wawili unafahamika katika misingi ya umuhimu wake maishani. Picha inayozushwa na 'vuta nikuvute' iliyopo inausawiri mnazi kama kitovu cha uhai. Sitiari hii ya mnazi inazichemsha bongo zetu na kuudadisi umuhimu wake hasa tunapotafakari historia na faida za matunda ya mnazi kwa wakazi wa pwani. Hata kwa yule asiyeufahamu mnazi, taswira hii inampa mshawasha wa kutaka kufahamu iwapo ni matunda ya mti tu yanayogombaniwa.

Alii hagombanii kuukwea mnazi, kwa ajili ya kukwea tu. Ni juu mnazini ambako kunaliliwa kutokana na natija ya kuwa huko.

Anamhimiza Badi (uk.19) ashuke;

> Sababu ya kukwambiya, ushuke tini haraka
> Mke na wanangu piya, wana ndaa mewashika
> Nami nataka kukweya, nitunde nazi hakika
> 'Kauze wapate pika

Mnazi huu ndio unaoweza kumnufaisha na kumpa mtu uhai katika maisha. Alii (uk. 19) anasimanga;

> Mwerevu ulijidai, fungu kubwa ukitwaa
> Wanayo wala miyai, na vyakula vya kufaa
> Wala hata hukinai, kwa mitumbo kuwajaa
> Na nguo njema wavaa

Sambamba na kujitononokea kwa kina Badi ni hali ya uhitaji inayowakabili kina Alii. Alii anatudokezea uhitaji huo kwa kulalama (uk. 20);

> Hali kuwa wangu wana, wadhii mno kwa ndaa
> Ndiyani ukiwaona, ni mitambara 'mevaa
> Ni kwa kuwa kitu sina, kuwapa nilowazaa
> Kwa wewe changu kutukuwa

Mikabala hii miwili ya maisha inatokana na tofauti za aliye juu dhidi ya aliye chini ya mnazi. Yanayojadiliwa si masuala ya kutunda nazi tunazozifahamu. Chacha (1992:75) anauona mvutano huu wa mnazi ukiwa ni uhusiano uliokuwepo kati ya vyama vya K.P.U. na K.A.N.U. ambavyo viongozi wao waliokuwa wameshirikiana kumtimua mkoloni walijikuta wakikorogana baada ya viongozi wa K.A.N.U. kukiuka mikataba ya kiuongozi. K.A.N.U., kama inavyodaiwa, ilijinyakulia na kuyafaidi matunda ya uhuru pekee na kuvitupa vyama vyengine.

Mbali na kusawiri mvutano huu wa kisiasa, mnazi huu kwa upana zaidi, unatumulikia pia mivutano kati ya wanyonge na wenye nguvu. Mvutano huo si lazima uwe wa kisiasa bali unaweza ukamulika jumla ya maonevu yote wanayotendewa wanyonge na wenye nguvu. Chacha anatutolea tafsiri yake kutokana na ushuhuda wa matokeo ya mwandishi mwenyewe kama anavyoeleza katika utangulizi

wa kitabu chake cha Sauti ya Dhiki. Kwa ambaye hajawahi kufahamu yale yaliyotokea na alisome shairi hili, picha ya mivutano itamdhihirikia vilevile.

Mnazi kwa jinsi ulivyotumiwa kisitiari unakuwa nyenzo ya kuyamulika maigizo haya ya Abdilatif.

### 2.4.3.3. Methali na Misemo

'Mnazi: Vuta N'kuvute', tukilinganisha na maigizo mengine tunayoyashughulikia, ndiyo maigizo ya kipekee yanayotumia kwa wingi ala hizi za lugha. Ala hizi ni semi zinazobeba hekima na mawazo ya kiupeo ambayo jamii ya Waswahili imekuwa ikiyashikilia tangu jadi. Methali na misemo, kama vile sitiari, tashibihi, na zana nyinginezo za lugha, zinatuwezesha kuibuka na hisi na maana ya maigizo haya, kwa jinsi ala hizi zinavyoweka wazi mawazo na maana kwa njia yenye mguso.

Alii na Badi wamo katika 'vuta nikuvute' yao. Badi anajiona akikabiliwa na tisho la kutolewa tonge mdomoni. Alii, kwa upande wake, anajiona akiipigania haki. Pande mbili hizi zinavutana. Vitisho, kutiana hofu na hata kupigana milaza kunatumiwa na wahusika hawa kwa ajili ya kuupata ushindi.

Inasadifu katika maigizo haya kwamba ala hizi za lugha zinatumiwa na Badi pekee. Kwa sasa, mhusika huyu ni jabari asiyehofu lolote. Ala hizi za lugha zinaweka wazi silika na mchemu wa udhalimu unaomwenda katika damu yake. Badi hasiti kumsimanga Alii kwa mkururo wa methali na misemo kama /...Mpiga ngumi ukuta huumiza mkonowe.../, /...Ni heri nusu shari, kuliko shari kamili.../ na /...Alobwia ndiye mwenye, alowata uzuzuwe.../.

Methali na misemo yote hii ni masimango na kebehi zinazofanyiwa mtu ambaye ana haki na kile Badi anachokiona kuwa ni chake. Badi anajiona ni mwerevu na aliyepevuka zaidi kimawazo kuliko Alii. Kujitoa shirikani kwa Alii, kulingana na kakake, kilikuwa kitu cha kipumbavu. Kwa Badi, Alii alikuwa 'akiupiga ngumi ukuta'. Mhusika huyu tunamwona akiuhalalisha udhalimu wake kwa kujiona akimfanyia hisani Alii kwa kile ambacho kwa hakika ni haki yake.

2.4.4. Lugha ya Kishairi na Maigizo katika 'Usiniuwe'

Katika maigizo haya, ni 'nofu la nyama' au mtoto aliyemo tumboni ambaye anasuhubiana na wahusika Mama, Uhai, Haki na Mauti. Wahusika hawa ni bubu lakini mengi yanayohusiana na maigizo haya yanaibuka kutokana na ustadi wa matumizi ya lugha. Zana za lugha zilizotumiwa katika maigizo haya zina nafasi muhimu ya kutuelewesha maigizo hayo.

2.4.4.1. Nafasi ya Taswira

Taswira inayotufuma zaidi ni ile ya mtoto aliyemo tumboni mwa mama. Mtoto huyu, kama kauli zake zinavyoeleza, yumo katika heka heka za kuunusuru uhai wake ambao mama ameazimia kuuchukua. Usalama na uhai wake umo mikononi mwa mtu ambaye badala ya kuwa mfariji wake amegeuka kuwa nduli.

Tumboni mwa mama, kama tunavyoelewa, ni mahali tunapopatarajia pawe salama kwa watoto kwa muda wa takribani miezi tisa. Hewa, chakula na mahitaji ya watoto hawa huwa ni jukumu la mama wanaowabeba. Hali inayotuthibitikia imekuwa hivyo kwa muda tu. Mama huyu amelighairi jukumu lake. Himaya ya tumbo

lake hapendelei ikaliwe na mtoto. Kulitekeleza hilo si jambo gumu kwani vidonge tu vinatosha kumtimua mtoto huyo tumboni mwake.

Taswira hii inakuwa mwenge unaotumulikia ugumu wa hali aliyomo mtoto huyu. Kwa kuitumia taswira hii, Abdilatif anatarajia kuonyesha hali ya kutotegemeeka kwa baadhi ya watu ambao tungekuwa na yakini nao kuwa ni wafadhili wetu. Hali ya uvunjifu inayomkabili mama inalipiziwa mtoto, kiumbe dhaifu asiyekuwa na hatia. Kadhalika, ndivyo hali ya maisha ilivyo ambapo watu wenye uwezo wanawanyanyasa watu ambao wanatarajia mapenzi na ulinzi toka kwao.

2.4.4.2. Tashihisi

Jambo moja la kuajabikiwa na linalozivuta nadhari zetu katika maigizo haya ni kuthibitikiwa na kiumbe kinachoongea kikiwa kingali tumboni. Huyu ni mhusika Mtoto au 'nofu la nyama' kama anavyojiita yeye mwenyewe. Mtoto huyu amepewa uhai kwa minajili ya kuwasiliana na maamake.

Athari ya zana hii ya lugha inatokana na tahadhari yake inayotushauri tupatafakari mahali alipo mtoto huyu. Baadhi ya hadhira ambayo imeshawahi kuziona picha za watoto wakiwa bado wangali tumboni mwa mama zao, picha kama hiyo inawajia bila pingamizi. Kitoto hicho tunachokiona ndicho kilichopewa uwezo wa kuongea na mamaake ambaye anasikia na kumwona mtoto huyu anapoongea.

Mbali na mbinu hii kuwa mbinu ya kimsaada inayotufanya tuyafikirie makazi ya mtoto, na vilevile uhai aliopewa, tunapata pia ujumbe wa kiyakinifu. Kitendo cha kuwaavya watoto ni tokeo

la kiyakinifu hapa duniani. Suala hili limezungumziwa kwa marefu na mapana na asasi mbalimbali za kijamii. Maigizo haya ni tamko juu ya suala hilo katika uwanja wa sanaa andishi.

Athari ya maigizo haya kwa hadhira inatokana na hali ya kiyakinifu ambayo mtetezi wake ni miongoni mwa madhulumu wa kitendo hicho cha kuavywa. Hapa tunauona ulalamishi wa mtu ambaye ukatili huu unamsibu. Utetezi wake haumlengi mamaake tu, bali ni maoni yake kwa mama wengineo wanaowauwa watoto wasiokuwa na hatia. Ni kupitia uhai huu ambapo Mtoto huyu anapata fursa ya kuushutumu uzinifu ambao husababisha mimba zisizotakikana.

Mbali na zana hii ya lugha kuwa tamko juu ya swala la uavyaji mimba, tunadhihirikiwa pia, na ukatili wa viongozi wa kisiasa kwa wafuasi wao. Wananchi, ambao wanawategemea viongozi wao, huishilia kunyanyaswa wanapotarajia faraja kutoka kwa viongozi hao. Wananchi ni mfano wa Mtoto huyu ambaye uhai ni haki yake. Hili ni onyo kwa viongozi wasiwanyanyase wanaowaongoza kwa kuwaona kama mizigo badala ya wanadamu wenye haki sawa.

Mtoto huyu pia, anakuwa nyenzo ya tashihisi nyinginezo za wahusika Mama, Uhai, Haki na Mauti. Mama anadhihirika kama mhusika katili ambaye haelekei kuyumbishwa kuliacha azimio lake. Mtoto anapoona hivyo anawahadhiria kesi yake wahusika wengine. Hadhira inafahamu na kuuelewa uhusika wa wahusika wengine kupitia kuhisiwa kwao na Mtoto. Uhai na sifa zao za kibinadamu zinazoidhihirikia hadhira ni zao la zana ya tashihisi iliyotumiwa kumsawiria mtoto.

#### 2.4.4.3. Takriri Neno

Beti za kumi na nane hadi ishirini zinakariri maneno mawili- 'sitakosa' na 'sikosi'. Maneno haya yanatokana na mzizi wa neno '-kos-'. Takriri hii inatumiwa na Mtoto kuusisitiza umuhimu wa maisha ambayo ni haki kwa kila kiumbe. Kauli hizi za kiutetezi zinamkanya mama kuwa si yeye pekee tu ambaye ana haki ya kuufaidi uhai.

Takriri hii inajitokeza mwishoni mwa maigizo haya. Beti za ishirini na saba hadi ishirini na tisa zina maneno 'Uhai', 'Haki' na 'Mauti' ambayo yanakaririwa. Maneno haya yanaisisitizia hadhira hali ya uvunjifu ambayo mtoto anaikabili kwa wakati huu. Mama anaamua kukidhulumu kiumbe ambacho amekuwa akikibeba kwa hiari tumboni mwake.

#### 2.4.4.4. Mahadhi (Ridhimu)

Mahadhi ya maigizo haya kwa jumla yanapanda na kushuka. Uzungumzi nafsia wa Mtoto ni masimango yanayoelekezewa Mama. Utetezi anaoutoa Mtoto unalengwa kumwelimisha Mama kuwa analonuia kulitenda si jambo murua. Wakati huu wa kutoa utetezi wake, Mama anatarajiwa asikilize kwa makini. Kwa kuwa yanayotolewa ni maelezo mahadhi ni ya maigizo ni ya mtiririko na ya polepole. Beti za kwanza hadi kumi na nne, kwa mfano, ni maelezo ya kumwelimisha Mama. Mahadhi yake ni ya polepole.

Kama inavyojitokeza, Mama ameazimia kumwua Mtoto. Anapojaribu kutenda hivyo, Mtoto anashtuka na hivyo basi kuathiri mahadhi ya maigizo. Hali hii inajitokeza zaidi katika beti tatu za mwisho. Beti hizi zinasomeka upesi upesi kutokana na alama za uwakifishaji kama vile mshangao, za kuuliza na mkato. Mbali

na hilo, kuna pia takriri za kama vile 'uhai', 'mauti', 'haki' na 'mamangu'.

Mbinu hii ya kishairi inamjulisha msomaji hali mbalimbali zilizopo. Kwenda kasi kwa mahadhi kunatumika kumfahamisha msomaji kuwa hali iliyopo si ya kutegemeeka.

## 2.5. Kimalizio

Lugha ya kishairi, kama tulivyoona, ina ukwasi wa kuibua maana na tajriba mbalimbali ambazo mshairi huyu anaziwasilisha. Zana tofauti tofauti za lugha alizozitumia Abdilatif, zinajaribu kueleza kwa ufasaha dhana ya maigizo katika tungo zake.

Lugha ya tungo hizi, mbali na kutufahamisha kwamba imetungwa kishairi, inazidi kuashiria kwa namna isiyokuwa ya kishairi. Kupitia lugha, tunaziona tungo hizi zikidai zisomwe kitamthilia. Ni kana kwamba mshairi huyu anasema 'huu si ushairi tu bali vilevile ni tamthilia'.

Tumeizingatia hoja kwamba tungo hizi pia zimewahi kuitwa tamthilia badalia (Chacha 1992). Tofauti na ushairi, tamthilia hutumia zana zake mahsusi za mawasiliano. Sura zinazofuata zimejaribu kuonyesha jinsi Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa unavyoweza kusomeka kitamthilia. Mbinu mbalimbali za kimaigizo alizozitumia Abdilatif kuwasiliana na hadhira yake zimejadiliwa. Mbinu muhimu zilizofafanuliwa katika sura ya tatu, na pia ya nne, ni lugha, kaida za kimaigizo, ploti, kitendo, wahusika na mandhari. Mbinu nyingine zilizoshughulikiwa ni kinaya drama na maleba. Mbinu hizi zinafafanua uwezo wa tungo hizi kuigizika.

# SURA YA TATU

## MBINU ZA KIMAIGIZO KATIKA UTENZI WA MAISHA YA ADAMU NA HAWAA

### 3.1. Utangulizi

Katika sura hii, tuliuangalia kwa undani ushairi wa Abdilatif, kama makala ya kimaigizo. Tuliangalia, hususani, njia maalum ambayo msomaji anaweza akazielewa tungo zinazoshughulikiwa kama maigizo.

Tungo zinazopatikana katika Sauti ya Dhiki na Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa hazikuandikwa kwa lengo la kuigizwa hadharani. Hata hivyo, tumeshuhudia mashairi au tungo mbalimbali zikikaririwa mbele ya hadhira. Jambo hili, kama tulivyodokeza katika sura ya kwanza, si geni miongoni mwa Waswahili wenyewe. Tungo tulizozishughulikia, mbali na kuwa hazikutungwa kwa minajili ya kutendwa mbele ya hadhira, zina sifa za michezo ya kuigiza. Hivyo basi, msomaji ana uwezo wa kuibuka na hisi ya maigizo hayo, kwa kuziweka tungo za mshairi huyu wa kijukwaa katika jukwaa la bongo lake.

Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa, 'Kutendana', 'Mnazi: Vuta N'Kuvute' na 'Usiniuwe', kwa jinsi zilivyotungwa, zinaweza zikaigizwa hadharani. Mazungumzo ya Adamu, kama yanavyojitokeza, yameandikwa kana kwamba yazungumzwe na mwigizaji kwenye jukwaa. Mfumo huu unaambatana, vilevile, na semi za wahusika wengineo kama vile Ibilisi, Hawaa, Habili, Kabili na wahusika wengineo.

Wazo hili kwamba tungo hizi zinaweza kuigizwa kwenye jukwaa, ndilo linalokuwa changamoto ya kujaribu kuibuka na aina ya semiotiki ya usomaji wa kimaigizo, ambao unaziona tungo hizi kama kivuli cha uigizaji unaotokana na utendaji wenyewe.

Yapo mambo ya kimsingi ambayo sharti yazingatiwe tunapolizungumzia suala la maigizo. Mambo haya ni pamoja na

kuutilia maanani mzunguko wa utatu. Kwanza ni waigizaji, ambao katika maigizo haya, watawakilishwa na wahusika wa tungo hizi. Wasomaji watasoma sehemu za wahusika kana kwamba ni waigizaji wanaojitayarisha kwa sehemu za Adamu, Hawaa, au hata Mwanamke. Pili ni watazamaji, ambao wanachukuliwa mahala pao na wasomaji. Tatu, ni lazima pawepo na jukwaa ambalo kwalo shughuli za nipa nikupe kati ya hadhira na waigizaji zitatekelezewa. Kwa kuyazingatia mambo haya matatu, maigizo yatakuwa yamekamilika.

Mbinu mbalimbali za kimaigizo tulizoabiri kuzichunguza, yaani lugha, kaida za kijukwaa, ploti, kitendo, wahusika, mandhari na hata kinaya drama sharti zizingatie mzunguko huo wa utatu.

### 3.3.2. Lugha ya Kimaigizo katika <u>Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa</u>

Sifa mojawapo ya lugha ya kimaigizo ni ule uwezo wake wa kutendwa. Kupitia lugha hii, wahusika wanaozicheza sehemu zao wanaweza kufahamu sehemu za maungo yao ambazo wanaweza kuzitumia kusisitizia yale wanayoyasema. Jambo hili linazingatiwa kwa kikamilifu na Abdilatif, ambaye anaitumia lugha inayoweza kutendwa. Lugha hii inajitokeza sio katika mbinu ya 'Maelezo' tu bali pia kupitia wahusika wenyewe. Mfano mzuri unatolewa na lugha ya wahusika Adamu na Hawaa ambao, wakiwa peponi, wanaingia katika mjadala mpevu kuhusu tunda. Hapa tuna mpiko wa 'Maelezo' na kauli za wahusika hawa zinazoumulika uwezo wa kutendwa kwa lugha na wahusika hao. Adamu (ubeti 357), anaanza kwa kumwambia Hawaa;

Kaamba waliliani
Machozi yako yakini
Yanikata langu ini
Likulizalo nambiya

Usemi huu unabeba ujumbe wa kile ambacho mhusika Hawaa anakitenda wakati mjadala unapoendelea. Kulia ni kitendo kinachoweza kutendeka; jambo ambalo linaupa utenzi huu uwezo wa kuigizwa kwenye jukwaa.

Tamko la Adamu, ambalo linamhakikishia mapenzi Hawaa, linakabiliwa na usemi wa mkewe ambaye pia, anatupatia fununu juu ya uwezo wa kutendwa kwa lugha iliyotumiwa na mwandishi. Hawaa (ubeti 360) anajibu;

Lau wewe wanipenda
Huwezi na kunikinda
Niwachie hili tunda
Mdomoni kukutiya

Uteuzi wa maneno haya yanamwezesha Hawaa kulichukua tunda lililomo mkononi mwake na kulipeleka mdomoni mwa mumewe. 'Maelezo' nayo yanawaongoza wahusika hawa; yakiwaelekeza namna ya ulaji wa tunda hilo, kwa kuchutama.

Sambamba na kutendwa kwa lugha ya utungo huu, tuna pia uwezo wake, wa kuiendeleza ploti ya maigizo haya. Ghadhabu na ari ya kujilipizia kisasi inayomchemka Ibilisi anapofukuzwa peponi, ni mfano wa jinsi lugha ya mhusika huyu inavyoweza kueleleza hoja hii. Ibilisi (ubeti 94) anasema;

Uchungu nina kisasi
Wa Adamu wafuasi
<u>Niwabadili nafusi</u>
<u>Wakithiri kupoteya</u>
(Msisitizo ni wetu)

Kauli hii inatudokezea yote ambayo Ibilisi anaazimia kuyatenda. Vituko vya mhusika huyu vinabebwa na kauli hii ambayo kwa hakika inatimizwa hapo baadaye. Ibilisi, anawahi kumkabili Hawaa, na kumpa undani wa kiuzushi unaowasababishia Adamu na mkewe anguko lao.

Mvuto wa tungo za mshairi huyu wa kimaigizo, umewezeshwa pia

na lugha yake ambayo ina uwezo wa kutuonyesha mambo mbalimbali ambayo wakati mwingine ni muhali kuwekwa kwenye jukwaa halisi. Kwa kuitumia lugha, Abdilatif, kwa mfano, anatupaisha mbinguni na kushuhudia vitendo vya kufikirika vya mbinguni ambavyo tunafahamu haviwezi vikaonekana katika ulimwengu halisi. Kupitia lugha, tunaona jinsi mshairi huyu anavyotufanya mashahidi wa kuuona umbuji wa Mungu anapomuumba Adamu. Mungu (beti 38-41) tunaelezwa;

Akaumba kwa udongo
Taratibu kwa utungo
Kiungo penye kiungo
Mtu akatengeneya.

Umbo bora kwa mfano
Kichwa shingo na mikono
Sehemu mbili kiuno
Mwili umegawanyika.

Mdomo wa kutamka
Mikono ni ya kushika
Namna alivyotaka
Miguu ni ya kwendeya.

Kadhalika masikio
Sauti zote ziweo
Yawe ni kiingilio
Ya neno jema na baya.

Shughuli hii ya Mungu, inatudhihirikia barabara na kwa ukamilifu kwenye bongo zetu. Vitendo vyote, tunaweza tukaviona katika akili zetu na kuvihisi, ingawa tunafahamu kwa yakini kuwa mambo yote yanayotekelezwa hatuwezi tukayaona katika maisha yetu licha kuwekwa kwenye jukwaa halisi.

Lugha hiyo hiyo, wakati mwingine, inatumiwa kuweka bayana vitendo halisi vya kimaigizo ambavyo vinakosa kauli za kueleza vitendo na hali hizo. Adamu, kwa mfano, kama tunavyoelezwa, aliumbiwa Hawaa ikiwa ni tokeo la tamanio lake mwenyewe kwani Adamu tunaelezwa (ubeti 136);

Moyoni akatamani
Akaamba laitani
Mtu kanami Peponi
Mola angeniumbia.

Analala, na anapoamka, anamkuta Hawaa mbele yake. Mwanamke anayemwona ni (ubeti 139);

Mtanashati wa umbo
Mwenye sifa ya urembo
Suraye mithili pambo
Yavuta kuangaliya.

Adamu anapatwa na mshangao; mshangao unaomfanya akose la kusema. Ikawa sasa (ubeti 140);

Adamu ende karibu
Ilhali aajabu
Kuona alo sahibu
Mwanamke shamsiya.

Anapozinduka, Adamu anabakia tu kushukuru Mungu kama njia pekee ya kueleza hisia zake, hadi anapoamrishwa amchukue Hawaa kama mkewe (beti 142-4).

Abdilatif anaitumia lugha ambayo si ya kimaelezo tu bali inathibitisha vitendo halisi vya kimaigizo pia. Kwa kuitumia lugha, mshairi huyu wa kimaigizo anajizatiti kuonyesha picha mbalimbali kwa jicho letu la nje na kutuhisisha, kama vile Adamu, katika fikra zetu. Mirengo hii ya kuonyesha kwa jicho la nje na kuona kwenye akili, haijitokezi mbalimbali katika maigizo haya. Wakati mwingine, mshairi huyu anatumia mirengo yote kwa pamoja. Hata pale ambapo inajitokeza pekee, ni lugha ambayo inalibeba jukumu hilo.

Katika jitihada zake za kuifanya hadhira yake iyahisi maigizo haya, Abdilatif ameitomelea lugha yake kwa zana mbalimbali za lugha ya kishairi. Lugha hii, kama tulivyoona katika sura ya pili, ina uwezo wa kufumbata dhana pana ambazo zingechukua maneno mengi kuzielezea kinathari. Kupitia lugha

hiyo, hadhira ya mwandishi imewashuhudia wahusika katika kitendo, mandhari waliyomo na hata kaida za kijukwaa zilizotumika.

### 3.3. Kaida za Kimaigizo

Kaida za kimaigizo ndicho chombo kinachotuwezesha tuwe weledi wa kitendo katika ulimwengu bunifu wa maigizo (Reinert 1970:xvii). Wazo hili linaashiria kwamba ili kuwepo na uwezekano wowote wa mawasiliano baina ya hadhira na mtunzi, ni sharti hadhira iwe na fununu juu ya kaida mbalimbali zilizotumiwa na mtunzi. Nafasi ya kaida za kimaigizo katika michezo ya kuigiza huwa ni kubwa.

#### 3.3.1. Kaida za Kimaigizo katika Utenzi

Mshairi Abdilatif hajapungiwa mkono na uwanja wa matumizi ya kaida za kimaigizo katika tungo zake. Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa, kwa jinsi ulivyotungwa, unaweza ukamtanza msomaji wake iwapo baadhi ya mambo yanayojitokeza hayataeleweka katika muktadha wa kaida za kijukwaa. Jambo hilo huenda likaathiri maigizo yanayojitokeza katika utungo huu. Kitengo hiki kinatoa mapendekezo ya mambo mawili muhimu ambayo yanastahili kuonekaniwa katika mkumbo huo wa kaida za kijukwaa ili kuibuka na maigizo yatakayofana. Haya ni pamoja na kaida ya Msimulizi na matumizi ya lugha ya kishairi.

#### 3.3.2. Msimulizi

Msomaji wa utenzi huu hatashindwa kugundua uchangamano wa sauti mbili - moja ya msimulizi na nyingine ikiwa majadiliano ya wahusika Hawaa, Adamu, Kabili, Mungu, Habili, Malaika na Ibilisi.

Chacha (1992:119), akiigusia hoja hii ya kuwepo kwa sauti mbili, anasema;

> ... lugha inayotumika hapa ina nafasi za aina mbili. Kuna kauli za maelezo ambazo ni usemi wa mtunzi na vilevile kuna kauli za wahusika ambao mtunzi amewatumia. Ni muhimu katika usomaji kuzingatia tofauti iliyoko kati ya lugha hizi mbili.

Lugha anazozizungumzia Chacha, kwa hakika, zinahitaji kutofautishwa ili maigizo katika mchezo yaweze kufahamika vyema. Lakini tutakuwa na tatizo gumu iwapo tutamfuata Chacha kwa kuiita 'lugha' mojawapo 'kauli za mtunzi', kama anavyoibainisha mtaalam huyo. Maigizo yetu yatakuwa chapwa kwa kuwa nafasi ya masimulizi yanayotolewa na usimulizi huo, yatamwendea zaidi Abdilatif mwenyewe. Ndipo tunapotoa pendekezo kuwa 'lugha' hiyo ichukuliwe kama kaida ya kijukwaa, ambayo kwayo, mshairi huyu anatuumbia mhusika aliyejitenga na wahusika wengine wanaotekeleza vitendo vya ndani, vya maigizo. 'Lugha' hii, hivyo basi, tunaieleza katika utungo huu kama ile ya Msimulizi.

Msimulizi huyu aliyetumika kikaida ambaye anatusimulia kisa cha Adamu na Hawaa, si kaida ngeni, kwani tunaweza tukamnasibisha na Arkadi Tscheisde, yule mwimbaji stadi toka Tiflis katika The Caucasian Chalk Circle. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa na mhusika anayeutamba mchezo wa Adamu na Hawaa. Visa mbalimbali, kama vile vya Adamu na Hawaa peponi, Hawaa na Ibilisi, na hata kisa cha ndugu wawili Habili na Kabili, vitakuwa mikononi mwa msimulizi huyu. Usimulizi huo unakuwa kiungo muhimu cha kuwatayarisha wahusika wa sehemu mbalimbali zilizomo katika utungo huu. Matokeo ya kaida hii, ni kudhihirikiwa na mchezo katika mchezo.

Msimulizi anakuwa mhusika ambaye, mbali na kuutamba mchezo wenyewe, vilevile, anakuwa mshuhudiaji wa matukio tofauti tofauti

yanayotendwa kwenye jukwaa. Athari kuu ya kuwepo kwa Msimulizi, kwa wasomaji wa mchezo huu, ni kuwa wanakiona kitendo cha ndani cha mchezo kupitia Msimulizi. Umuhimu wa mhusika huyu hauwezi ukakadirika. Tutaona, kwa undani, uamilifu wake hapo baadaye. Kwa sasa, ni muhimu kutaja kwamba ufahamu wetu wa kitendo cha mchezo huu, unahusisha uhusika wa Msimulizi huyu.

### 3.3.3. Lugha ya Kishairi

Mbali na kaida ya Msimulizi, tunaona pia matumizi ya lugha ya kishairi. Katika mazungumzo yetu ya kila siku, ni nadra sana kuzungumza kishairi. Hata hivyo, tunawaona Msimulizi, Adamu, Ibilisi na wahusika wengineo wanavyozungumza katika mchezo huu. Abdilatif anaitaka hadhira iyaone matumizi ya lugha ya kishairi kama jambo la kawaida katika utungo huu. Kaida hii inasaidia, hususani tukitilia maanani kwamba, ushairi ni lugha inayosema mambo mengi kwa muhtasari.

## 3.4. Ploti

Kipengele cha ploti ni miongoni mwa mbinu ambazo Abdilatif amezitumia ili kuifanya hadhira yake kuwa na hisi kamili ya tungo zake kama maigizo. Maoni ya wataalam mbalimbali walioidurusu na kuitolea maelezo dhana hii ya ploti yalichanganuliwa. Kwisha kufanya hivyo, tulichukua mwelekeo ambao ulituwezesha kuona jinsi tunavyoweza kuieleza ploti aliyoitumia Abdilatif. Aidha, tuliangalia jinsi mbinu hii ilivyotumika, na athari yake katika kumfanya msomaji au hadhira kuibuka na hisi ya maigizo ya tungo hizi. Katika tasnifu hii, tumeifafanua ploti kama ule mpangilio na mtiririko wa vitushi kama vilivyowasilishwa na mtunzi.

3.4.1. Ploti katika Maigizo ya Utenzi

Hiki ni kipengele ambacho kimetumika kuyawasilisha maigizo katika utenzi huu. Faslu ya kwanza ni onyesho linalotendeka mbinguni. Mungu na malaika wapo katika mjadala. Mjadala huo unahusiana na pendekezo la Mungu la kumuumba mwanadamu ambaye atamfanya khalifa kwenye ardhi. Mpango au ratiba ya maisha ya mwanadamu huko ardhini unaogofya. Mwanadamu anabashiriwa kuwa mtu mlaghai, atakayepuuza ibada na kuimwaga damu. Haya ni mambo ya kuogofya yanayotufanya tuutilie shaka uamuzi huu wa Mungu. Malaika anaowaeleza haya, vilevile, wanaingiwa na hofu. Kauli ya Mungu (ubeti 36) kuwa

Mimi ni mola adhima
Ni mjuzi wa hikima
Kadiri ninavyosema
Najua msoyajuwa

inalengwa kuifanya hadhira kuwa na hamu ya kujua litakalotokea. Kauli hii inabeba hekima fulani ambayo, kwa kiwango kikubwa, inachangia maudhui ya mchezo. Inaikuza pia taharuki, kile kipengele ambacho huipa hadhira mshawasha wa kujua jambo litakalotendwa au litakalotokea, hadi Mungu adhihirishe hekima na kujua kwake.

Faslu ya pili inatuingiza katika shughuli za kiungu anazotekeleza Mungu. Hapa Mungu, kwa kutumia udongo, anamuumba mwanadamu. Mwanadamu anafunzwa na Mungu mwenyewe. Anatayarishwa kuwapiku malaika, ikiwa ni njia ya kufanywa bora. Hilo linatekelezwa na kuishia na amri ya kusujudu. Malaika wote wanasujudu isipokuwa Ibilisi. Kukataa kusujudu kwa Ibilisi na majisifu yake, ni sehemu ya hekima za Mungu. Tukio hili ni muhimu katika maigizo haya kwa mambo mawili muhimu.

(a) Ufahamu wa Mungu

Ibilisi, kama anavyosimulia Msimulizi, ni kiumbe mwovu. Asili yake, anatueleza, ni shetani /Alokuzwa na Mannani... Alipokinyenyekeya/ (ubeti 71). Tunakumbushwa zaidi na Msimulizi kuwa /Muasi yake asili... Mwisho humrejeleya/ (ubeti 69).

Kwa hadhira, hili ni tukio la kwanza ambalo linatupasa kuutafakari ujuzi wa Mungu. Ibilisi kumbe ni shetani aliyepata makao miongoni mwa malaika. Kuumbwa kwa Adamu, na jaribio la kumsujudia, ndiyo inayokuwa njia ya kumtimua Ibilisi peponi. Mungu anafahamu kwamba Ibilisi ni kiumbe mwenye kiburi. Kukataa kumsujudia Adamu ni sababu tosha, na ya kihekima anayoitumia Mungu kumtolea Ibilisi peponi.

(b) Uhusika wa Ibilisi

Ibilisi anapotimuliwa peponi, anamsihi Mungu, muweza wa kila jambo, uwezo wa kuwapoteza wanaadamu. Kwa kukubaliwa ombi lake, Ibilisi anakuwa mhusika anayejitokeza, na vilevile kuhisika katika mchezo. Uhusika wa Ibilisi, pamoja na baraka za kuwapoteza watu alizotunukiwa na Mungu, unawafanya washuhudiaji wa tukio hili kuvingojea kwa hamu vituko na fujo za Ibilisi. Ibilisi anajiona ameangamia kwa sababu ya kuumbwa kwa Adamu. Anaabiri kujilipizia kisasi miongoni mwa wanaadamu. Hadhira inatayarishwa kuwaona Ibilisi na Mungu wakiingia katika kinyang'anyiro cha kuwania wafuasi. Ubabe wa pande hizi mbili unathibitika katika maigizo yote.

Onyesho la Adamu na Hawaa tunaweza tukasema ni ile sehemu ya kati ya maigizo. Ni katika onyesho hili anapojitokeza Hawaa katika maigizo. Tukumbuke kwamba Hawaa ni tokeo la matamanio ya

mwenzi, la Adamu. Tukio la Hawaa kwenda matembezini pekee ni njia ambayo mwandishi ameitumia kwenda kumkutanisha Hawaa na Ibilisi. Katika mkutano huo, Hawaa anawahi kuelezwa faida za matunda ya mti wa haramu; faida ambazo matokeo yake si yale anayoelezewa. Katika onyesho hili, tunajikuta kama vile Hawaa, tukitaka tuifahamu siri iliyogubikwa katika tunda. Vilevile, kunatokea mvutano kati ya Hawaa na Adamu, kila mmoja kati yao akiuona mwelekeo wake wa tunda kuwa ndio sahihi zaidi. Kutokana na mvutano huu, wasomaji wanaingia hamu ya kutaka kufahamu mshindi na mshinde baina ya wahusika hao wawili. Mashindano haya pia yanaingia katika kiwango cha pili; Mungu dhidi ya Ibilisi.

Mkutano wa Hawaa na Ibilisi ndilo tukio muhimu linalojitokeza katika onyesho hili la peponi. Kukutana huku kunaipatia ploti msukumo wa kuona jinsi Ibilisi atakavyofanikiwa au kushindwa kumshawishi Hawaa, kumwezesha Adamu kuyatumia matunda ya mti wa haramu. Vilevile, shauku ya kuviona vituko vya Ibilisi, ambaye wakati wote tumekuwa tukimsikia, inafikia kilele na kujitokeza kwake jukwaani. Tunachoshuhudia katika mkutano huu ni uwongo uliokithiri ambao kwa bahati mbaya unamwingiza Hawaa mtegoni. Hawaa anarubuniwa kwa maneno na kukubaliana na maoni ya Ibilisi. Ibilisi anafanikiwa kumzaini Hawaa, kwanza kwa kujidaia umalaika. Kama ilivyo ada ya malaika, ni wasema kweli na hupendelea watu heri. Pili anamtisha Hawaa kuwa Adamu angejiolea hurulaini waliomo peponi iwapo hatajizatiti kupata kizazi. Ulaji wa tunda anashauri ndilo tegemeo lake tu.

Ni katika mkutano huu huu, ambapo mipango ya kumshawishi Adamu inapangwa. Ibilisi anajitolea kutoa mwongozo wa jinsi ya kumkabili Adamu. Anashauri (ubeti 304);

Tumia yako madaha
Maneno ya ufasaha
Iwe kwako ni silaha
Ya kike kuitumia

Kisha inapobidi (ubeti 306);

Kwake ulie kipenzi
Tone moja la machozi
Litamtia majonzi
Na kukusikitikiya

Mpango huu unatarajiwa uifanye hadhira iutamani kwa hamu na ghamu, ustadi wa Hawaa wa kutekeleza yale ambayo anashauriwa na Ibilisi. Haya yanadhihirika katika onyesho linalofuata.

Tukio kuu linalofuata, ni lile la kuliwa kwa tunda haramu na wahusika Hawaa na Adamu. Yote ambayo Ibilisi alimfunza Hawaa yanafuatwa kimsahafu. Hawaa anaanza kwa kumbembeleza Adamu na faida za kulila tunda hilo. 'Madaha ya kike' ya Hawaa hayafui dafu: jambo ambalo linasababisha ulazima wa 'tone la machozi'. Adamu, kama alivyobashiri Ibilisi, anashindwa kuuzuia moyo wake. Anakubali kulila tunda. Hilo linapotendeka, Mungu anawaamuru Adamu, Hawaa na Ibilisi watoke peponi washuke kwenda ardhini. Sehemu hii ya ploti ni kilele cha maigizo haya. Adamu, pamoja na kuhisi kuwa analotenda si sawa, anaona hana budi ila kumfuata Hawaa. Anajikuta katika njia panda: kumfuata Mungu ambaye alimfanyia hisani kubwa ya kumuumba na kumweka peponi, au kumfuata Hawaa; mke na mwenzi katika kila jambo, na pia mwanadamu kama yeye. Adamu anachagua kumfuata Hawaa. Anguko lao linajiri.

Maonyesho ya ardhini yamepangwa kwa namna ya kutuelewesha juu ya shughuli mbalimbali wanazotekeleza Adamu na Hawaa katika kukabiliana na ulimwengu wao. Ploti hapa, inakuwa nyenzo ya kuonyesha juhudi za wanadamu hawa wa kwanza wanavyojitahidi kuyamiliki mazingira yao mapya. Shughuli tunazoonyeshwa

wakizitenda ni pamoja na ufugaji, ukulima na hata uchumaji wa matunda mwitu. Adamu, mbali na kuyakabili mazingira yake, pia anajaribu kuutafuta uhusiano mwema na Mungu wake, kwa kumshauri mkewe watubie madhambi yao. Hawaa bado anabishana.

Katika maonyesho haya, tunaingizwa katika ploti ndogo ya kaka wawili, Habili na Kabili. Kaka hawa, ambao wanakiendeleza kitendo cha 'uzazi', wanajikuta wakipigania dada mmoja wamuoe. Ugomvi huu unaishilia katika kifo cha kwanza; cha Habili. Kaka hawa ni sehemu ya maigizo ya utungo huu. Uhusika wao una uhusiano na ploti kuu ya kisa hiki kwa kujaribu kumpa Hawaa na hadhira pia, usuli na kuendelea kwa kifo hapa duniani.

Ni katika sehemu hii hii, ambapo Adamu na Hawaa, wanajiona wakosa na kumwomba Mungu msamaha. Hili ni suala la kiugunduzi miongoni mwa wahusika na inaashiria hatima ya ploti ya maigizo haya. Kupitia dua hiyo, kuna hali ya kusawazishwa kwa mambo. Mungu, kwa upande mmoja, na binadamu, kwa upande mwingine, wanaridhiana na kuuimarisha uhusiano wao wa hapo awali. Yote yaliyopita yamekwisha pita. Sehemu hii, mbali na kuwa hitimisho la ploti na vilevile maigizo yenyewe, inampa fursa msomaji kuirudia hali yake ya kawaida ambayo kwa muda wote ilikuwa imezama katika visa mbalimbali katika maigizo.

## 3.5. Kitendo

Aristotle (Kernan 1963), mwananadharia maarufu wa drama, katika kitabu chake <u>Poetics</u>, anaieleza tanzia kama mwigo wa kitendo chenye uzito, kilichokamilika na cha kiasi fulani. Kulingana na Aristotle, dhana hii ya kitendo ni dhana pana, ambayo mchezo mzima unaazimia kukitimiza. Maoni haya yanatufanya

tukione kitendo katika misingi ya kidhahania.

Dhana hii ya Aristotle kuwa kitendo ni kile kilichokamilika si ya kuridhisha hasa tunapozingatia kwamba kupatikana kwa kitendo hicho kikamilifu ni tokeo la mkusanyiko wa vitendo vidogo vidogo katika maigizo. Katika utafiti huu, dhana hii ya kitendo ilifafanuliwa na vitendo vidogo vidogo katika tungo ambavyo vinaunda kitendo kikuu anachozungumzia Aristotle. Kitendo ni ule uzi unaoshikiliwa, kwa maneno na vitendo vya kimwili, tangu mwanzo hadi tamati ya maigizo yetu. Kwa kufanya hivyo, udhahania wa kitendo, mahala pake, ulichukuliwa na kitendo halisi kilichotokana na vitendo vidogo.

### 3.5.1. Kitendo katika Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa

Kitendo cha maigizo haya kimegawanyika mara mbili. Kwanza ni kitendo cha nje, na pili, kitendo cha ndani. Katika kuvitofautisha vitendo hivi, kitendo cha nje kinahimiliwa na mhusika Msimulizi, ilhali kile cha ndani kinatendwa na wahusika Mungu, Adamu, Hawaa, Ibilisi, Kabili na Habili. Mbali na wahusika kuwa kigezo cha kimsingi katika kuvibainisha vitendo hivi, tuna pia mgongano wa kiwakati unaothibitishwa na kauli za wahusika hawa. Wakati ambapo Msimulizi anasimulia kwa wakati uliopita, wahusika wa kitendo cha ndani wanazungumza kwa wakati uliopo. Hali hii inampa Msimulizi hadhi ya kuwa mshuhudiaji wa yale yanayotendwa na kina Adamu. Msimulizi, kwa upande wake, anatoa ufafanuzi wa yale ambayo wahusika hao wangeyatenda au waliyowahi kuyatekeleza.

Kuwepo kwa kitendo katika daraja mbili, hakumaanishi kwamba maigizo ya utungo huu yametingwa. Kitendo cha nje na kile cha

ndani vinathibitisha muumano, sio kimasafa tu bali hata kimaudhui.

### 3.5.1.1. Kitendo katika Faslu ya Kwanza na ya Pili

Faslu ya kwanza na ya pili, takribani zote, zimo mikononi mwa Msimulizi, na hivyo basi kitendo cha nje. Mahali panapotekelezewa kitendo hiki ni mbinguni. Kupitia Msimulizi, habari za kiufunuzi na msingi wa maigizo unaandaliwa. Msimulizi huyo anakuwa kiungo muhimu cha hadhira katika kukiona kitendo cha nje cha maigizo haya. Msimulizi anatupatia muhtasari wa baadhi ya vitendo muhimu vilivyotokea kabla ya kujitokeza kwa wahusika wa kitendo cha ndani katika faslu ya tatu.

Katika faslu ya kwanza kitendo kinajengwa kutokana na uhusiano uliopo kati ya Mungu na Malaika. Uhusiano huu ni wa muumba na viumbe wake wanaomtumikia. Uhusiano uliopo ni wa wahusika wanaotangamana na kuelewana. Faslu hii inaanza na sifa za Mungu ambazo, kutokana na Msimulizi, zinatupatia vuguvugu la ukuu wake. Semi hizo pia ni maelekezo ya kijukwaa, zinazotuwezesha kuwaona malaika walioko mbinguni wakisujudu na kumtukuza Mungu. Katika ufalme wake, ambao unaelezwa na miongoni mwa mengineyo 'kiti cha enzi', Mungu anaitamka nia yake ya kumuumba halifa au mfalme wa aridhini. Kauli hii inayotoka kwa Mungu, mara moja, inazichemsha hisia za malaika ambao wanaingia hofu. Malaika hao wanaingia hofu kutokana na sifa za kibadhirifu zinazomshamiri kiumbe ambaye Mungu ananuia kumuumba. Hadhira pia, bila shaka, inaingiwa na uoga fulani kwa kusikia sifa za kiuharibifu ambazo zinatajwa kama sifa zitakazomshamiri kiumbe huyo mpya.

Malumbano, au vitendo vya kiusimulizi, ndivyo vinavyojitokeza katika faslu hii. Mkinzano kati ya Mungu na Malaika hasa ndio unaojitokeza. Hatima ya malumbano hayo ni kauli ya Mungu ambayo inaweza ikachukuliwa kama kitendo kikuu cha mchezo. Mungu (Ubeti 36) anasema;

Mimi ni mola adhama
Ni mjuzi wa hikima
Kadiri ninavyosema
Najua msoyajuwa
(Msisitizo ni wetu)

Kauli hii ya kuwa yeye Mungu kama muumba anafahamu kila lisilojulikana ni kauli inayotufanya, kila mara, tuwe macho kuona jinsi weledi huo wa Mungu utakavyojitokeza. Mungu amekwisha kutueleza kuwa kiumbe anayemweka aridhini atawahi kumwaga damu, na hata kuukwepa wajibu wa kumwabudu yeye kama muumba wake. Mambo yote hayo, na maovu mengineyo, hayamtii shughuli. Badala yake, anamuumba mwanadamu kwani 'anajua yasiyojulikana'. Kitendo cha mchezo huu ndipo tukapendekeza kuwa kinaingilia suala la kudhihirisha mipango ya Mungu. Pendekezo hili limeangaliwa sambamba na ushahidi wa vitendo vinavyofuata na kuangalia iwapo mipango ya Mungu kwa kweli ni ya kipekee.

Vitendo vya uungu, hasa kuumbwa kwa Adamu, vinatekelezewa katika faslu ya pili. Kufikia faslu ya tatu, wahusika Adamu na Hawaa wameandaliwa jukwaa huku hadhira ikiwa tayari imetilia maanani matukio muhimu yaliyotokea. Matokeo hayo ni pamoja na kuumbwa kwao, kutokea kwa mgogoro kati ya Adamu na Ibilisi, kuharamishiwa kwa Adamu na Hawaa matunda na mti uliomo katikati ya bustani, na vilevile, dhamira ya Ibilisi ya kuwapoteza wanadamu. Ni katika faslu hii ambapo Msimulizi anatupatia fursa ya kuona kitendo cha ndani cha maigizo haya. Adamu na Hawaa

wanajidhihirisha wenyewe, usimulizi ukiwa na nafasi ndogo kuliko hapo awali. Hili ndilo onyesho la kwanza la kitendo cha ndani.

### 3.5.1.2. Faslu ya Tatu

Katika faslu hii, kuna maonyesho mawili. Onyesho la kwanza ni la 'Adamu na Hawaa'. Pili, ni onyesho la 'Hawaa na Ibilisi'. Maonyesho haya mawili yanatokea huko peponi.

#### 3.5.1.2.1. Adamu na Hawaa

Onyesho la kwanza linapoanza, tunaelezwa na Msimulizi kiasi cha muda ambao wahusika hawa hawajaonana. Maelezo haya yanaitayarisha hadhira na hali ya wasiwasi iliyopo. Tayari tunaelezwa wasiwasi uliomsakama Adamu; kitendo kinachokubalika na chenye uyakinifu kwani hili ndilo linalojiri pindi mtu anapotowekewa na mwandani wake. Hawaa anapotokezea, Adamu anapata wasaa wa kuipumzisha nafsi yake na kumuuliza Hawaa alikokuwa. Hawaa anaeleza kuwa alikuwa ameenda matembezi. Kitendo hiki cha kuitwalii bustani anachosimulia Hawaa hakikutumiwa kisadfa na mwandishi bali kina uamilifu wake katika kukiendeleza kitendo kikuu cha mchezo. Utalii huu unamfikisha kwenye 'mti wa neema' ambao ndio chanzo cha anguko lao na Adamu. Matembezi haya tunakisia, kutokana na kitendo kinachofuata, kwamba yamemkutanisha Hawaa na Ibilisi. Fursa anayoipata Ibilisi kutokana na matembezi hayo inampa nafasi ya kumghuri Hawaa juu ya 'uzuri' wa matunda ya mti haramu.

Matembezi ya Hawaa, kama tulivyodokeza, si ya kisadfa. Matembezi hayo yanakuwa changamoto ya kitendo cha onyesho hili la Adamu na Hawaa. Hili linadhihirishwa na umbeya aliokuja nao

Hawaa juu ya matunda ya mti. Vumbuo la umbeya alilokuja nalo Hawaa linamfanya adai;

Nasikia ule mti
Tulofanyiwa sharuti
Ndio wenye neemati
Kushinda ilobakiya

Naambwa mna ujuzi
Na ya milele makazi
Na thamma mna uzazi
Vijana vya fahariya

Hawaa, bila shaka, amekutana na mtu ambaye ameipuliza sumu hii. Kulingana na yamini aliyokula Ibilisi mbele ya Mungu pindi alipomuomba

Kwa hilo bwana naomba
Nidiriki kuwapemba
Wa Adamu kila nyumba
Njia kuwapotezea

na kutakabaliwa dua yake, tuna imani kuwa huyu si mwingine ila ni yule shetani aliyefukuzwa mbinguni. Kitendo chote katika onyesho hili kinaishilia kuwa 'nasikia' na 'nambwa' tupu. Hawaa anasaili hoja mbalimbali, moja baada ya nyingine na kwa mantiki. Hoja zote anazotoa ni rubuni tupu za maneno alizopata toka kwa Ibilisi.

Hawaa anasaili mantiki iliyopo ya Mungu kuwakubalia wale chochote isipokuwa matunda ya mti huo mmoja tu. Fauka ya hayo, haoni sababu ya Mungu kuweka peponi kitu ambacho anaona ni udhia kwa viumbe wake kukila (beti 248-49). Anaukashifu ufuataji wa amri kimbumbumbu bila kusaili hekima ya amri hizo. Hawaa anaona hawana tofauti na wanyama. Anasema (ubeti 195);

Mfano wetu wanyama
Hatuna akili tama
Twaona na kutazama
Hatuna tunalojuwa

Kulingana na Hawaa, kukatazwa kula tunda si jingine ila ni njama

ya kuwanyima fursa wanadamu kuwa wengi, kama walivyo malaika. Anamuasa Adamu wajitahidi wawezavyo waweze kuwa wengi kuliko malaika. Hawaa anazidi kuusimanga utupu wa maisha kwa mwenye shibe kuwa ni mpungufu wa akili kwani haijui shida.

Ni matembezi haya haya yanayomfanya Adamu amuulize mpenziwe iwapo ameuona mti wa hurulaini. Hawaa, inavyojitokeza, haufahamu. Adamu anapoueleza mti huo kwa tafsili, Hawaa anajiinamia, akihofu kupokwa mwandani wake. Wivu unamfanya Hawaa kusihi mti huo usitajwe tena mbele yake. Hiki ni kitendo cha kutiliwa maanani kwani, Ibilisi baadaye, anakitumia kama kitisho kimojawapo cha kumfanya Hawaa kukubaliana naye kuwa ipo haja ya kulila tunda. Ibilisi (ubeti 274) anasema;

Hatari ilo usoni
Adamu humu peponi
Ataoa hurulaini
Na wewe kukukimbiya

Kitisho hiki cha ukewenza, kama tunavyoona baadaye, kinafanikisha mipango ya Ibilisi ya kumtia Hawaa katika hatia.

Adamu, kwa jinsi anavyokabwa na tetesi za Hawaa, anatuhumu kuwa ni Ibilisi anayezua kutoelewana kwake na mkewe. Hili linamfanya Adamu kuuliza shina la habari alizokuja nazo mkewe. Jibu linakuwa;

Hii taarifa yangu
Mepata kwa shoga yangu
Peponi mwenye kitangu
Ndimo tumekutaniya

Adamu anang'amua kuwa huyo ni Ibilisi. Anatoa maelezo kuhusu sifa za Ibilisi, na jinsi zinavyofarikiana na za Malaika. Maelezo haya hayamfumi Hawaa. Kitendo cha onyesho hili kinaisha ikiwa bado Hawaa hajaridhika kuwa Adamu anamweleza ukweli. Kitendo kinanoga zaidi kutokana na pande mbili alizozivaa

Ibilisi. Kwa maoni ya Adamu, Ibilisi ni kiumbe mlaghai na mwovu, ambaye lengo lake kuu ni kujilipizia kisasi cha kutolewa kwake peponi (beti 94-5). Hawaa, kwa upande wake, anamwona Ibilisi kama mtu anayemtakia heri. Siri ya mti wa neema anayodokolewa ni hisani kubwa aliyofanyiwa na 'Malaika wa Mungu'. Dukuduku la Hawaa, kinyume na weledi wa Adamu anaoutumia mwandishi, linakuwa msingi imara wa kukifanikisha kitendo cha onyesho hili.

3.5.1.2.2. Hawaa na Ibilisi

Katika onyesho hili, kitendo cha mchezo kinafanikishwa chini ya mti. Mti huo ndio unaokuwa mhimili wa kitendo kilichoisha na kinachofuata. Mti huu umejawa na shari. Tunatarajia kuwa kitendo kinachotendeka kinahusiana na kutiwa mushkeli na kughafilishwa kwa Hawaa. Mhusika huyu anakuwa madhulumu wa nafsi yake mwenyewe. Onyesho hili linapoanza, kauli zinazotolewa zinaifahamisha hadhira kuwa huu si mkutano wa kwanza kati ya wahusika hawa. Ibilisi anauliza iwapo Hawaa alifanikiwa kumbembeleza mumewe kulila tunda. Jawabu anayoipata Ibilisi si ya kuridhisha. Hawaa anaeleza ukakamavu na uthabiti wa mumewe katika kumcha Mungu. Kitendo cha onyesho hili kinachukua mkondo wa upangaji wa hujuma mpya. Kwa kuwa haonyeshi msimamo thabiti, Hawaa anatishwa na Ibilisi, ikiwa ni njia ya kumbana aweze kuwa mtekelezaji wa hujuma hizo. Hili linafanikishwa kupitia kutajwa kwa mti wa hurulaini ambao unatupatia picha ya mwanamke jamali kuliko Hawaa. Hawaa anaaminishwa kuwa ni tunda tu litakalomwepusha na janga linaloelekea kumsibu. Hawaa tunamwona akibabaika, akimsihi 'sahibu' yake, amweleze la kufanya. Jawabu inakuwa kulila tunda.

Ushiriki wa Hawaa unahakikishwa. Ibilisi anamhimiza afanye hima mumewe alile tunda. Anamshauri Hawaa atumie silaha ya kike, yaani kilio, kama njia ya kumfanya Adamu kutekeleza kile kisichotakikana.

3.5.1.3. Faslu ya Nne: Adamu na Hawaa Tena

Faslu hii ina onyesho moja linalotendeka peponi. Wahusika wakuu, Adamu na Hawaa ndio washiriki wa kitendo cha onyesho hili. Msimulizi anatoa maelekezo ambayo tungestahili kuyaona kama vitendo wanavyofanya wahusika Adamu, Hawaa na Ibilisi. Kutokana na maelekezo yaliyotolewa, pamoja na ushuhuda wetu wa njama yenyewe, tunatarajia tuone kwa ukamilifu kiwango cha kufanikiwa kwa mpango wa Hawaa na Ibilisi. Onyesho hili linapoanza, hatushangai kuona vitendo vya kilaghai ambavyo vinatokea bila Adamu kufahamu.

Hawaa anapotokeza, tunamwona akiwa na uso wenye bashasha. Kwa jumla, anaonekana mtu mwenye furaha. Anamchukua Adamu kwenda matembezini. Kikomo cha matembezi yao ni palepale chini ya mti. Hili halitokei kisadfa, kwani ni hapo hapo kwenye mti, ambapo tunamwona Ibilisi akinyapanyapa na kuukwea mti. Maelezo ya jinsi Ibilisi alivyoukwea mti hayatolewi lakini tunapaswa kufahamu kuwa hiki ni kitendo cha haraka haraka. Ukweaji wenyewe si wa pupa, hasa tunapofahamishwa kwamba mhusika huyu alikuwa akinyapanyapa, /...pasina kuuvunja unyasi/ (ubeti 311). Tunamwona Ibilisi akichagua tunda zuri, la kuvutia, ambalo analiangusha mbele ya Adamu na Hawaa. Hawaa anayaona yote yanayotendeka kama anavyoeleza Msimulizi (ubeti 315);

> Yote haya yakijiri
> Yali ya kisiri

Adamu hana habari
Wala kumfumaniya

Maelezo ya tunda lenyewe yanatufanya tulione pindi tu tunapofikiria wororo wa siagi, wepesi wa hariri na ulegevu wake pia. Hisi zetu za maonjo, kama hadhira ya maigizo haya, zinachemshwa. Hata hivyo, hofu ya kuvunjwa kwa miiko ya Mungu sharti iwe nasi.

Hawaa analichukua tunda hilo. Adamu naye ndiyo mwanzo anamwona Hawaa na tunda haramu mkononi. Yanayofuata ni cheche za makemeo, ambayo kwa kuyatafakari, tunaweza tukayahisi yakiambatana na makali ya sauti ya Adamu. Adamu anaona hawako salama, mradi tu wangeendelea kubakia kwenye mti. Anatoa amri watoweke haraka iwezekanavyo chini ya mti. Kulingana na msimamo wake kwa Mungu, kitendo aula kwa wakati huu kingekuwa kile cha kulibakura tunda, lidondoke mikononi mwa Hawaa. Laiti hilo lingejiri, mwandishi hangeweza kukielekeza kitendo kama kilivyo. Kitendo kingechukua mkondo tofauti kabisa. Abdilatif hamfanyi Adamu kutekeleza hilo. Badala yake, Adamu anamwacha Hawaa na tunda hilo mkononi, na hivyo basi, kumpatia fursa ya kumshawishi kulila tunda.

Hawaa hasiti kumshawishi Adamu. Anaanza kwa kushangaa jinsi mwanamume anavyoweza kushindwa kujasirisha kuukaribia mti na mazao yake kuliko mwanamke (ubeti 322). Anazitaja pia faida za mti huo, ikiwemo siri ya pato la kizazi. Hawaa anatekeleza kitendo cha haramu kwa kuliuma tunda huku akisifia utamu wake. Adamu habanduki na anaelekea kutotingishika. Hawaa sasa anaitumia silaha yake ya kike.

Hawaa anaanza kwa kuyasingizia mapenzi; kuwa mumewe anamkatalia kila jambo kwa kuwa hampendi. Baadaye kidogo, Hawaa

analia, kitendo ambacho kinamtinga Adamu. Tunamwona Adamu akihuzunika kwa kumwona mwenzake akilia. Adamu anakiri penzi lake kwa mkewe, na hapo ndipo anapotiwa tunda mdomoni.

Kitendo cha kutiwa tunda mdomoni kinamaanisha kukaribiana kwa wahusika hawa wawili. Hakuna maelezo ya kuonyesha jinsi kukaribiana huku kulivyotekelezwa. Pia hatufahamu jinsi Adamu alivyotiwa tunda mdomoni. Utendwaji halisi wa kitendo hiki kwenye jukwaa utakuwa umo mikononi mwa mwigizaji stadi ambaye ataujua wakati mwafaka wa kumkaribia Adamu na hatimaye kuifahamu njia bora ya kumlisha Adamu tunda hilo. Wasomaji, wakiwa hadhira ya maigizo haya, hawana nafasi hiyo ya kuona vitendo hivyo kwenye jukwaa halisi. Usomaji wa kimaigizo unatarajiwa umsaidie msomaji kufahamu wakati aula ambao vitendo hivi vinatekelezwa. Kwa kufanya hivyo, msomaji atakuwa ametekeleza wajibu wake kama hadhira ya mwandishi, ambaye katika maigizo haya, anatarajia vitendo hivyo vifanyike. Hili linaweza kutekelezwa, lakini sio bila ya fununu fulani inayotokana na semi za wahusika.

Katika kuyajibu masuala haya, tunawajibika kuangalia kauli za wahusika wenyewe. Kauli anayoitoa Adamu, na ambayo inampasa awe karibu na mpenzi wake, ni ile inayosema (ubeti 357);

> Kaamba waliliani
> Machozi yako yakini
> Yanikata langu ini
> Likulizalo nambiya

Bila shaka, Adamu ameshtushwa na kilio cha Hawaa. Hivyo basi, haiyumkiniki, kumuuliza swali kama hili akiwa yu mbali na Hawaa. Hata ikiwa yuko mbali, basi kuyapunguza masafa kati yao, ndilo jambo la kimantiki. Kitendo cha kumkaribia Hawaa, ambaye bado kalishikilia tunda lake, kinatokea hapa. Ukuruba huu wa kimasafa ndio unamwezesha Hawaa kuipata fursa ya kulitia tunda mdomoni mwa

Adamu.

Msimulizi anatoa maelekezo ya kutekelezwa kwa ulaji wa tunda. Hawaa, kwa hila, anaufikisha mkono mdomoni mwa Adamu huku akimkamulia maji ya tunda. Kitendo kinakuwa cha kimwili; tukiuona mkono wa Hawaa ukitekeleza jambo ambalo lina hatima mbaya. Maelezo ya Msimulizi yanaeleza jinsi Hawaa anavyofanikiwa kumlisha mumewe tunda. Hawaa, kwa hila, anampemba Adamu na kumtia tunda mdomoni. Kinachorejelewa hapa, ni kutekelezwa kwa kitendo, kwa njia ya madaha na ya kimapenzi, kusudi Adamu apotewe na akili zake tambuzi. Kitendo hiki, ingawa kibaya kwa Adamu, hakikutani na pingamizi yoyote kutoka kwake kutokana na kukolea kwa mapenzi. Jambo hili pia linatilia nguvu hoja kwamba, fanaka ya kitendo cha mchezo, hutegemea sana ushirikiano kati ya wahusika wa mchezoni. Adamu anahiari kulishwa tunda ambalo wakati wote amekuwa akijizatiti kuliepuka.

Utamu wa tunda unamkolea Adamu kiasi cha kutomaizi linalotokea. Swali la Hawaa, analomuuliza mumewe iwapo tunda alilojililia ni tamu au la, ndilo linalotuzindua na lile lililojiri. Baba na mama kufikia hapa wametenda walilokatazwa na Mungu. Adamu anakiri utamu wa tunda ingawa bado ananung'unika kuwa Hawaa amemchongea kwa Muumba wake. Baadaye, wanaafikiana na kwa pamoja wanachutama kula matunda ya mti wa haramu. Ghafla wanajikuta uchi. Kinachotokea ni mfadhaiko wa nafsi zao. Uchi katika uhalisi wake, hasa wa watu wanaowekeana heshima, si kitu cha kupendeza machoni mwao. Pengine baadhi yetu tutadai kwamba hawa walikuwa watu waliooana, na kwa hivyo, hawakuwa na sababu ya kubabaika. Mfadhaiko huu tunaweza tukauhisi athari yake kwa kujiweka katika muktadha ambao sisi na watu tunaoheshimiana kama

vile wazazi wetu ghafla tuonane tupu zetu. Kukimbiana, na kutumia njia yoyote ya kujisitiri, kama kule kutumia majani walikofanya Adamu na Hawaa, ni mambo ambayo tutayakubali kama vitendo vinavyofaa kwa wakati huo.

Kitendo cha kulila tunda ndicho kinachotekeleza hatima ya Adamu na mkewe iliyobashiriwa toka mwanzo. Wao walikuwa ni viumbe ambao makazi yao yalikuwa duniani. Peponi palikuwa ni mahali pa kupitia tu. Kwa namna yoyote, Adamu na Hawaa wangetolewa peponi. Matunda wanayokula yanatoa fursa ya kutolewa kwao badala ya Mungu kuibeba lawama ya kuwatoa peponi pasi na sababu.

### 3.5.1.4. Faslu ya Tano na ya Sita

Katika maonyesho yanayopatikana katika faslu hizi za utungo, kitendo cha maigizo kinaelekea kuzisawiri juhudi za mapambano ya binadamu na mazingira yao. Adamu na Hawaa, wakiwa binadamu wa kwanza, wanavumilia mateso aina mbalimbali ili kuweza kuumiliki ulimwengu wao. Kwa namna nyingine, wahusika hawa pia, wanaitekeleza ahadi ya Mungu ya kumweka mfalme au mwakilishi wake kwenye ardhi. Maonyesho hayo ni 'Adamu na Hawaa Duniani' na 'Uzazi'.

#### 3.5.1.4.1. 'Adamu na Hawaa Duniani'

Onyesho la 'Adamu na Hawaa Duniani' linafunguliwa na maelezo ya Msimulizi kuhusiana na mandhari iliyopo kwenye jukwaa. Mandhari hiyo si ya kuridhisha kutokana na ukosefu wa yale yaliyopatikana peponi. Dunia inayoonekana haina mimea, ina mito ya maji ya kawaida, wanyama wote ni wanyama mwitu na mawe yamejaa

kila mahali. Mandhari hii si ya kuridhisha na inakuwa changamoto ya kitendo cha kusukumiana lawama ambacho Adamu na Hawaa wanakiingilia.

Kitendo kinaanza na manung'uniko ya Adamu ambaye anadai kuwa Hawaa ndiye chanzo cha dhiki wanazozikabili. Hawaa, kwa upande wake, anashangaa jinsi machozi yake yalivyoweza kuwa sababu tosha ya uasi wa Adamu. Fauka ya hayo, Adamu, kulingana na Hawaa, ni mtume ambaye anastahili kufahamu vyema ubaya na uovu. Mazungumzo haya yanafikia kilele wakati wahusika wanapomwomba Mungu awarehemu wote ingawa kila upande haukubali makosa. Kitendo hiki cha dua tunakiona kama mwanzo wa kuishi katika dunia kwa kuziomba baraka za Mungu kwanza.

Katika faslu ya sita, Msimulizi anaeleza shughuli mbalimbali walizotekeleza Adamu na Hawaa wakiwa hapa duniani. Shughuli hizi, kikaida, ni mambo ambayo wahusika hao wanayatenda kwenye jukwaa na kuthibitika machoni mwetu. Hivyo basi, tunawaona Adamu na Hawaa wakitekeleza shughuli mbalimbali za kilimo, kuchuma matunda mwitu, na hatimaye kujipumzikia pangoni. Shughuli zote hizi tunaziona zikifanywa kiuanagenzi. Hapa tunaweza tukamfikiria mtu yeyote ambaye hajawahi kulima maishani mwake ili kujizalishia picha kamili ya uanagenzi wa wahusika hawa. Vitendo hivi vinafanywa kila mara hadi wakati ambapo wahusika hawa wanaonyesha kuzimiliki shughuli hizi. Kupitia majaribio ya kila mara, ndipo wanapoweza kuzibainisha nafaka mwafaka kutokana na mbaya. Pia wanaanza kuwaweka nyumbani wanyama ambao muda wote walikuwa wakiishi mwituni. Majaribio haya, tunaweza tukayanasibisha na kule kusujudu kwa Binadamu mbele ya Shetani katika <u>Mashetani</u>, ambapo Binadamu anasujudu kama inavyopasa baada

ya majaribio ya muda. Tofauti ni kwamba, wakati ambapo Binadamu anafanikiwa kusujudu vizuri kupitia amri za Shetani, Adamu na Hawaa wanafanikiwa kutimiza vitendo mbalimbali kupitia uigizaji bubu kwenye jukwaa, huku maelekezo yakitolewa na Msimulizi.

### 3.5.1.4.2. 'Uzazi'

'Uzazi' ni onyesho linalotuingiza katika mazungumzo kati ya Adamu na Hawaa. Katika onyesho hili, kitendo kikuu kinazingatia usuli wa uzazi, na hatima yake katika kifo. Kauli ya Hawaa kuhusiana na wasiwasi wake juu ya kitu kinachotembea tumboni mwake kinaashiria hali ya ujauzito inayomkabili. Tunamwona Hawaa akiwa kama mama yeyote mja mzito, ambaye tayari tumbo lake limeanza kuvimba. Adamu anamjulisha kuwa ana mimba. Usuli wa mimba hiyo, umo katika hamu ya Hawaa, ya kutaka kujizalia watoto. Kubeba mimba, na hatimaye kuzaa kwa uchungu miongoni mwa wanawake, kunahalalishwa kama adhabu ya Hawaa ya kulila tunda.

Msimulizi anatuandaa kuwaona wahusika wawili, Habili na Kabili, watoto wa Adamu na Hawaa kwenye jukwaa. Muda uliopo ni baada ya siku nyingi. Habili na Kabili wanaijenga ploti ndogo ya maigizo haya na kuchangia maudhui yake. Wanahusika katika kutekeleza kifo cha kwanza hapa duniani. Vilevile, wanakuwa uelelezo wa mipango yake Mungu. Tunakumbuka barabara, kuwa Mungu alikuwa ameubashiri umwagaji damu utakaofanywa na wanadamu kwenye ardhi (ubeti 28). Wahusika hawa wanapojitokeza, tunawaona wakiteta vikali, Kabili akidai kuwa ana haki ya kumwoa dadaake wa pacha moja. Habili, hata baada ya kuibuka na ushindi baada ya kukubaliwa kwa sadaka yake na Mungu, anauwawa na Kabili. Baada ya kumwua kakaake, tunamwona Kabili akishikwa na mfadhaiko.

Anahangaika na maiti ya kakaake hadi wanapotokeza kurabu wawili wanaomzindua kuwa wafu hupaswa kuzikwa.

Baada ya kifo cha Habili, kitendo kinachukua mrengo wa kufikia hali ya usawazishano. Hawaa anaonekana amejifunza kutokana na visa vingi alivyovishuhudia. Anakiri kuwa Ibilisi ndiye mwovu aliyewakosesha rehema ya Mungu. Kitendo kinamalizika na dua; baba na mama wakiwa na yakini kuwa wamesamehewa madhambi yao. Ukurasa mpya wa Maisha unafunguliwa.

### 3.6. Wahusika

#### 3.6.1. Utangulizi

Tunapousoma mchezo wa kuigiza, wahusika wa mchezo huo ndio wanaozivuta nadhari zetu zaidi. Jambo hili hutokea kwa kuwa mwanatamthilia hutupambanisha na mazungumzo yanayoambatana na vitendo vya wahusika wake. Nafasi ya mtunzi wa tamthilia huwa imetoweka. Mwanatamthilia, tofauti na mwanariwaya, hana uhuru wa kutuelezea fikra na hisia za wahusika wake. Mazungumzo na vitendo vya wahusika wake ndivyo vinavyotupatia vuguvugu la hisia na fikra za wahusika wenyewe. Mwanatamthilia, kwa mfano, hana uhuru wa kueleza kuwa mhusika fulani 'amesakamwa na biwi la simanzi'. Hali mbalimbali wanazojikuta wahusika wake si matilaba yake kuzifafanua, bali ni wahusika wenyewe wanaotarajiwa wazieleze hali hizo.

Kutokana na dhana kwamba wahusika katika tamthilia wana jukumu la kujifafanua wenyewe, tunaibukiwa na hoja ya kuwaona wahusika hao kama watendaji. Sifa hii ya utendaji inatokana na maumbile yanayowashamiri wahusika hao. Miongoni mwa sifa hizo za kimaumbile, ni pamoja na uhai uliokithiri ule wa watu wa

kawaida. Uhai huo hudhihirika katika mambo ambayo ni msingi wa maisha, kukiwemo ule uwezo wa kujieleza kilugha na vitendo, fikra tambuzi, wingi wa hisia, na kuingia mbioni ili kuyatimiza baadhi ya malengo wanayonuia kuyatekeleza.

Wahusika katika michezo ya kuigiza wanapojitokeza kwetu, hutenda mambo ambayo kwayo, tunafungukiwa na undani wao. Machoni mwetu, tunawaona mwanzo wakiwa wametanda ukungu. Ni kutokana na wanayosema na wanayotenda, ambapo, tunaenda mbele na kuufahamu uhusika wao.

Katika sehemu hii ya wahusika, azma yetu ni kuwaangalia wahusika kama watendaji katika maigizo ya utungo huu. Tumeitumia istilahi ya wahusika, kwani ni kupitia wahusika hao ambapo tunaingilia dhana ya waigizaji. Hata hivyo, dhana hii ya waigizaji inapasa ieleweke katika misingi ya mtunzi wa tungo hizi. Haistahili, kwa mfano, kuwaona Adamu na Hawaa kama sehemu zinazoigizwa na mtu mwingine asiyekuwa Adamu au Hawaa wa mwandishi.

Tunapousoma utungo huu, itabidi tuwaone Adamu, Hawaa, Habili na wahusika wengineo kama watendaji wa nafasi zao. Maigizo haya yanahitajia kwamba wahusika wanaobainika wawe ni wale ambao mwandishi mwenyewe anawatarajia watekeleze mambo aliyowapangia. Usomaji wetu tunatarajia utuongoze katika kuona jinsi wahusika wa Abdilatif wanavyozitekeleza sehemu zao. Kwa ufupi, usomaji wetu wa kimaigizo unatuelekeza katika kuheshimu jukwaa la mwandishi kama alivyoliwasilisha na kutudhihirikia katika utungo.

### 3.6.2. Kudhihirishwa kwa wahusika katika utungo

Katika maigizo haya, kuna njia kadhaa ambazo Abdilatif

amezitumia kuwafahamu vyema wahusika. Njia hizo humwezesha msomaji kujipatia picha toshelezi za kuwafasiri wahusika anaowaona. Kwanza, njia kuu ambayo ni muhimu kuzingatia ni yale wanayotenda na wanayofanya wahusika. Njia hii inaturudisha hadi kwa Abdilatif ambaye amewasawiri wahusika wake kama watendaji wa nafasi zao husika.

Kulingana na njia hii, usomaji wetu utahitaji kunolewa-ukiona kila jambo ambalo mhusika analisema au kulitenda. Wahusika, wakiwa watekelezaji wa sehemu zao walizopewa, huwa wanatoa kauli ambazo zinalifikia lengo hilo. Ibilisi, kwa mfano, kupitia kwa Msimulizi, tunamwona akimuomba Mungu haja ya kutunukiwa kuzusha uhasama miongoni mwa binadamu. Ombi hilo linakubaliwa. Ibilisi pamoja na wenziwe ikawa tangu siku hiyo wamo mbioni kuwafanyisha watu maovu (beti 104-5). Ibilisi anapojitokeza, hatuoni akifafanuliwa tena na mtu mwingine bali tunamwona akiwa katika harakati za kuwaangamiza wanaadamu kupitia kauli na vitendo vyake. Kitendo cha 'Hawaa na Ibilisi', kwa mfano, kinatuonyesha Ibilisi akiicheza sehemu yake ya kuwapoteza wanadamu. Kauli anazotoa zinalengwa kuwafarakanisha Adamu, Hawaa na Mungu.

Pili, tunawajibika kuziangalia kwa makini kauli zinazotolewa na wahusika wengine kuhusiana na wahusika fulani. Abdilatif ameitumia mbinu hii katika maigizo yake. Katika maigizo haya, njia hii ya kuwadhihirisha wahusika kupitia wahusika wengine inaelezeka vizuri kwa kuuzingatia uhusika wa Ibilisi. Kitendo cha 'Adamu na Hawaa', kwa mfano, kinatuonyesha mhusika Hawaa akiusimulia wema wa 'shoga yake' ambaye pia ni 'malaika wa Mungu'. Maelezo ya Hawaa kuhusu shoga huyo yanatuandaa katika

kumwona Ibilisi na vituko vyake. Hawaa, anavyoonekana katika kitendo hiki, amerovyeka rojo uongo aliosimuliwa hadi akawa ni mwakilishi wa Ibilisi katika kumkabili Adamu. Kitendo kinachofuata cha 'Hawaa na Ibilisi' ni dhihiriko la uharibifu wake ambao Hawaa tayari alikuwa ameudokezea.

Njia hizo mbili pia zimetomelewa na njia nyinginezo, zikiwemo zile za 'Maelezo' na 'Msimulizi'. Maelezo, kwa mfano, yanatupatia habari za kiufunuo kuhusiana na usuli wa uasi wa Ibilisi. Maelezo yanarudi nyuma kiwakati na kutueleza kuwepo kwa Ibilisi miongoni mwa malaika wakati yeye, kiasili, ni shetani. Maelezo hayo ndiyo yanayotoa mwanga wa jinsi Ibilisi atakavyoicheza nafasi yake katika maigizo haya. Msimulizi naye, kwa upande wake, anatoa habari zinazohusiana na wahusika na jinsi wanavyokitekeleza kitendo cha ndani cha maigizo.

### 3.6.3. Wahusika katika Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa

Katika maigizo haya, wahusika wamegawanyika katika makundi mawili kulingana na kitendo cha mchezo. Kundi la kwanza linamilikiwa na Msimulizi ambaye, kama tulivyotaja katika kitengo cha kitendo hapo juu, ni mhusika wa kikaida. Kundi la pili linajumuisha Adamu, Hawaa, Ibilisi, Habili na Kabili. Wahusika wa kikundi cha pili wanazitenda nafasi za kitendo cha ndani, ilhali Msimulizi anashughulikia kitendo cha nje cha mchezo. Tutaanza na mhusika huyu wa kitendo cha nje, yaani Msimulizi, kabla ya kuwaingilia wale wahusika wa kitendo cha ndani.

#### 3.6.3.1. Msimulizi

Mhusika huyu, kama anavyojitokeza, ni mshuhudiaji wa matokeo

kwenye jukwaa la kina Adamu, Hawaa, Ibilisi na wahusika wengineo wa kitendo cha ndani cha mchezo. Tukiwa hadhira ya maigizo haya, tunamwona Msimulizi, akiwa amejitenga na wahusika wengineo kimasafa huku akisimulia na kushuhudia matokeo kwenye jukwaa la ndani. Kutokana na kauli zake, tunahisi kule kujitenga kwake katika maigizo haya. Msimulizi anaicheza nafasi yenye majukumu mengi.

Awali, ni nafasi yake kama kiunganishi kati ya hadhira na wale wahusika wa kitendo cha ndani cha mchezo. Ingawa upo mgawo katika kitendo, ni muhimu kutaja kwamba kitendo cha nje na cha ndani vinahusiana na kujengana. Kitendo cha ndani ni kile kinachotendwa na kina Adamu. Msimulizi, kutokana na ustadi wake wa kusimulia, anatubainishia mambo muhimu ambayo wahusika wengine wanapasa kuyasema au kuyatenda kwa viungo vyao. Hadhira, kupitia Msimulizi, inapata fursa ya kuandaliwa mapema katika kufahamu jinsi kitendo kitakavyotekelezwa na wahusika wengine. Nafasi yake ya uunganishi inajitokeza tunapoitazama kauli kama hii;

Kunena maneno hayo
Akachafukwa na moyo
Akaanguwa kiliyo
Bibi Hawaa kuliya

Katika kauli hii, Msimulizi haijulishi tu hadhira yake mkondo ambao kitendo kiliuchukua baada ya majadiliano kati ya Adamu na Hawaa, bali pia ni maelekezo yanayonuiwa kutuonyesha jinsi Hawaa anavyoitenda nafasi hiyo kwa wakati uliopo. Mbali na kuwa ni masimulizi ya jinsi Hawaa alivyofanya, wakati huohuo tunamwona mhusika huyo akifanya kitendo hicho hicho kwenye jukwaa la ndani ya mchezo.

Sambamba na suala la kuwa kiunganishi kati ya hadhira na wahusika, ni mazingatio ya wakati kwenye jukwaa. Msimulizi,

anaposimulia kisa chake, anafanya hivyo katika wakati uliopita. Usimulizi wake unachochewa na uonyeshaji wa papo kwa papo kwa kuwaacha wahusika wajitokeze wenyewe. Beti za 260 na 261 zinaeleza mabadiliko ya kiwakati;

Mpaka alipofika
Ibilisi mpotoka
Ndipo akachangamka
Hawaa kuchekeleya.

/ Mpaka alipofika ... Hawaa kuchekeleya/ za Msimulizi, ghafla zinabadilika na kuwa

Bi Hawaa nijulisha
Kama umemuwezesha
Adamu kwa mshawasha
Ule mti kutumiya.

za mhusika Ibilisi. Msimulizi, ndiye anayekatiza vitendo vinavyotokea kwenye jukwaa na kutukumbusha kuwa, tunayoshuhudia ni sehemu ya maigizo katika usimulizi wake. Kitendo cha kula tunda kinapotokea, Hawaa anashauri;

Usifanye wasiwasi
Mpenzi kaa upesi
Ujiburudi nafusi
Matunda kujishibiya

Usemi huu, ghafla unakatizwa na Msimulizi, na kututanabahisha kuwa kitendo hicho kiliwahi kutokea hapo zamani. Anasema;

Pamoja wakachutama
Baba na mwenziwe mama
Penye mti wa harama
Matunda wakajiliya

/Mpenzi kaa upesi/, ya Hawaa inakinzana kiwakati na /Pamoja wakachutama/, ya Msimulizi. Wakati Hawaa anapotenda kwa wakati uliopo, Msimulizi anatufahamisha kuwa haya ni mambo yaliyokwishatendeka. Mabadiliko haya ya wakati hayamaanishi kupotoshwa kwa mshikamano wa maigizo haya. Msimulizi, au mhusika kama Hawaa anapotokeza, hadhira huwa imeandaliwa ipasavyo,

kuwaona au kutoweka kwa wahusika hao.

Tunapochunguza kwa makini, Msimulizi anajivalia nyuso tofauti tofauti anaposimulia kisa hiki. Mhusika huyu mara ni Mungu ambaye wakati huo huo anajibizana na Ibilisi. Jambo hili lisipoangaliwa kwa uangalifu huenda likawatanza baadhi ya wasomaji hasa kwa kutafakari uzungumzi wa nafsi ya kwanza wa Mungu na Ibilisi. Huu ni aina ya usimulizi ambao una mizizi yake katika fasihi simulizi ya Kiafrika ambayo kwayo mtambaji hutamba hadithi huku akionyesha vitendo vyenyewe (Matteru (1983). Mbinu hii, anayoitumia Msimulizi, inatuwezesha kuuhisi zaidi ukuruba wetu katika kushuhudia matukio ya mbinguni.

Aidha, Msimulizi amesahilisha zaidi mawasiliano ya mwandishi, katika kuyawasilisha matukio ya mbinguni. Suala kuu hapa ni mantiki iliyopo ya kuyaweka majadiliano ya mbinguni katika himaya ya Msimulizi, wakati Msimulizi huyo huyo anapowaacha baadhi ya wahusika kama vile Adamu, Hawaa na wengineo kujitokeza dede kwenye jukwaa. Hali hiyo huenda ikawa ilijiri kwa kuwa dhana ya Mungu ni ngumu kuelezeka hasa kwa kuzingatia onyo la <u>The Holy Qur'an</u> la kumfananisha Mungu na kitu chochote. Kumweka Mungu katika medani sawa, yaani kujitokeza kwenye jukwaa sawa na wahusika wengine, kungewafanya wasomaji kumdhania Mungu kuwa yuko hivi au vile jambo linalokatazwa katika misingi ya dini ya Kiislamu. Hivyo basi, Msimulizi pekee ndiye tunayemwona akitamka kauli za nafsi ya kwanza ambazo tayari zimo katika misahafu.

### <u>3.6.3.2. Adamu</u>

Aristotle (Kernan 1963), katika kitabu chake <u>Poetics</u>,

anamfafanua shujaa wa kitanzia kama mtu ambaye ni mwadilifu, mwema, na anayestahili kupewa uzito fulani katika tanzia. Alichomaanisha Aristotle ni kwamba, shujaa huyo anapojitokeza katika tanzia ana haki tummulike katika misingi ya kimaadili. Shujaa huyo, huwa ni mhusika anayejitoa kafara ili kuwa tambiko la tata zinazomkumba kwenye mchezo. Hali hii anayoielezea Aristotle ndiyo inayomsibu Adamu katika maigizo haya.

Katika maigizo haya, Adamu anathibitisha uhusika wa kitanzia. Vitushi mbalimbali, kabla na baada ya kumbwa kwake, vinamsawiri kama mtu mwadilifu. Msimulizi anatumulikia kuumbwa kwake kama tokeo la ari ya Mungu, ya kumuumba mtu atakayekuwa mfalme kwenye ardhi. Hilo linamfanya Mungu kuwakusanya malaika mbele yake kuwajulisha dhamira yake. Malaika wanapinga. Lakini Mungu anaendelea na dhamira yake.

Baada ya kuumbwa kwa Adamu, Mungu analichukua jukumu la kumwelimisha Adamu. Elimu anayoipata haikadiriki: Anathibitisha hilo kwa kuwataja malaika wote kwa majina, nafaka zote humu duniani na hata nyota. Mungu, pamoja na sifa zake za ukubwa katika kila kitu, anatufanya tuione elimu ya Adamu kuwa upeo wa elimu. Kuelimishwa huko na Mungu, kwa mfano, kunatupatia hisia kuwa Adamu, ingawa ni mwanadamu kama wanadamu wengine, kidogo ana sifa za kipekee zinazostahili kumweka katika ngazi tofauti na wanadamu wengine. Adamu, kwa hilo, anakuwa kama wahusika wa kitanzia, kama vile Hamlet, ambao wamekiuka daraja za maisha ya kawaida za kibinadamu (Bradley 1992). Likaja shindano kuu kati ya Adamu na Malaika. Adamu akaibuka mshindi. Hili ni tukio moja ambalo ni muhimu kutuonyesha upevu wa Adamu kwa kutunukiwa bongo chapu chapu na Mungu. Mashindano hayo yanampandisha daraja ya

juu kuliko malaika, kama kitendo cha kusujudiwa kinavyoashiria. Kusujudu kwa malaika (ubeti 50) ni ishara ya viumbe kupigwa mafungu kulingana na ubora wao; kila anayemsujudia mwenzake akiwa daraja ya chini. Ni kitendo hicho hicho cha kusujudu ambacho Adamu anakitekelezea Mungu wake anapoumbwa (ubeti 48). Kwa kulizingatia tukio hilo, ubora na uzito wa mhusika huyu unajengeka.

Baada ya kuumbwa kwake, Adamu anawekwa peponi. Pepo hiyo, kama Msimulizi anavyotuelezea, ilimsababishia upweke. Upweke huo ukamfanya atamani mwenzi. Mungu haoni matamanio hayo yakiwa na ubaya wowote kwani yana mwelekeo wa kisawasawa. Anampatia Hawaa kumwondolea upweke. Adamu, pamoja na Hawaa, wanaamriwa waishi humo, wastarehe kwa lolote, isipokuwa kula matunda ya mti wa haramu.

Adamu anapotokeza katika maonyesho ya peponi, tayari wameishi na Hawaa kwa muda. Ni katika maonyesho haya, na baadaye yale ya ardhini, ambapo tunaweza tukauhukumu uhusika halisi wa Adamu kama anavyofanya na kutenda mambo mbalimbali.

Wakiwa wamepoteana kwa muda mrefu, Adamu tunamwona akiwa ametaharuki. Anakabiliwa na mkewe na masuala ya kipotofu yanayohusiana na matunda ya mti. Hawaa anazua mjadala wa siri iliyofichwa katika mti huo - akidai ni nyenzo ya uzazi, elimu na anasa mbalimbali. Mjadala huu unatufunulia umbuji wa Adamu katika taaluma ya uchanganuzi wa silika za watu. Kwa Hawaa, Ibilisi ni malaika wa Mungu. Adamu anatoa ufafanuzi wa hila za Ibilisi zikiwemo ule uwezo wa kujigeuza umbo anapotaka kuleta husuda na fitina. Maelezo hayo ni miongoni mwa hekima za Adamu za kutaka kuihifadhi hali ya kihafidhina ya kuzifuata amri za

Mungu. Na hasiti kukumbusha (ubeti 245) kuwa;

Mungu ametukataza
Mti ungatupendeza
Matunda tukiyameza
Itakuwa maasia

Kwa kila njia, Adamu anaonekana akiwa na ari ya kumfurahisha Mungu kwa kuyafuata yale aliyoamrisha.

Kupatikana kwa hisia katika nafsi ya Adamu ni nembo mojawapo muhimu ya kusababisha anguko lake. Ni hisia hizo ambazo zinajitokeza kama msingi wa udhaifu wake - udhaifu wa kibinadamu ukiwa ndiyo njia kuu ya kuwaangusha mashujaa wa kitanzia (Carpenter 1975). Hisia hizo, hususani zile za kimapenzi, zimegawanyika mara mbili. Kwanza ni mapenzi yake kwa Mungu ambayo tumekwisha yagusia hapo juu. Pili ni mapenzi kwa Hawaa, ambayo ni kifaa cha kusababisha anguko lake na mkewe. Katika mapenzi hayo, chembechembe za uasi wa kibinadamu zinajidhihirisha.

Adamu, akiwa mwanadamu na mume wa Hawaa, ana majukumu ya kutekeleza. Kwanza ni kuonyesha mapenzi yake kwa dhati. Hili linajitokeza katika maigizo haya pindi wahusika hawa wanapokutana. Mti wa hurulaini unakuwa kielelezo cha mapenzi hayo ambapo Adamu anaapa kutoutaja mti huo kwa kuchelea kumuudhi mkewe. Mapenzi yaliyotiwa katika moyo wa Adamu yamekithiri mno. Mapenzi haya yanaishilia kuwa kitanzi anachojinyongea mwenyewe.

Ukamilifu ni jambo la kufikirika miongoni mwa waja. Adamu, vilevile, si kiumbe aliyekamilika, ijapokuwa anaonyesha hekima iliyovuka mipaka ya uanadamu. Hawaa anajaribu kila njia kuona kwamba mumewe ametimiza lile analotaka. Vishawishi vya maneno havifai kitu kwani Adamu anashikilia lile aliloamrishwa na Mungu. Ushauri wa Ibilisi kwa Hawaa, ndio pekee unaomyumbisha Adamu.

Ibilisi anafahamu vyema hisia za kibinadamu; kuwa huhuzunika pindi wanadamu wenziwao wanaposhikwa na huzuni. 'Tone moja la machozi' analomsisitizia Hawaa linakuwa jawabu aula ya kumtia Adamu mtegoni. Adamu anashindwa kumwona Hawaa akilia huku akisingizia kuwa anatendewa hivyo kwa kuwa hapendwi. Adamu anajikuta akitarazaki haramu kama ishara ya upendo wake kwa Hawaa. Ni sifa hii ya kibinadamu, yaani kukithiri kwa hisia za kimapenzi, ambayo inamkutanisha Adamu na anguko lake.

Baadhi ya wasomaji hawatasita kusaili iwapo ulaji wa tunda haramu ni kitendo kilichofungamana na uamuliwaji awali wa maisha ya Adamu. Usomaji huo hautalaumika kwani Mungu, kupitia Msimulizi (beti 17-8) ameeleza;

> Napendekeza kuumba
> Kiumbe ambacho kwamba
> Nchini ajenge nyumba
> Na mashamba kulimiya
>
> Kadhalika afuge nyama
> Na ndege kuwatazama
> Katika yangu rehema
> Wapate kufurahiya

Kwa wasomaji wanaomtetea Adamu, hasa na ulaji wa tunda, wanamwona kama mtekelezaji wa uamuaji awali wa Mungu wa kumweka kwenye ardhi. Lakini ingefaa tusisahau kwamba binadamu si malaika ambao hawamuasi Mungu na wakatenda yale wanayoamrishwa bila pingamizi (beti 62-4).

Binadamu, tofauti na malaika ambao hawawezi kujichagulia la kutenda, alipewa uhuru wa kiuteuzi. Jambo hili linajitokeza kwani Adamu anakumbana na vitu viwili vya kuchagua - kula au kuliacha tunda. Adamu, akiwa anafahamu anachotenda, anaamua kula tunda. Kwa maoni yetu, Adamu ndiye wa kulaumiwa kutokana na majaaliwa yake kama inavyojitokeza katika maigizo.

Baada ya anguko lao, Adamu anajikuta ardhini. Anakuwa mwepesi wa kupambana na mazingira yake pamoja na mkewe. Kila jambo analotenda linanuiwa kutoa mwanga juu ya mambo ya kimsingi katika maisha. Adamu anaingia katika shughuli za kilimo, ufugaji na hata hifadhi ya nafaka zitakazotumiwa kama mbegu. Pia tunatajiwa watoto wake ambao kisa chao ni uelelezo wa malezi kwa watoto na hukumu kwa watu wanaoteta.

Hali ya usawazisho inayotokea mwisho wa maigizo, ambayo kwayo Adamu, na baadaye Hawaa, wanarudi kwa mola wao, inaradidi utegemeaji na umuhimu wa Mungu katika maisha ya mtu. Picha tunayoipata ni ile ya kusisitizwa kwa unyoofu wa Adamu katika masuala ya kiroho; kwa kuomba msamaha, maigizo haya yanaisha kwa kuonyesha kuwepo kwa utuvu katika akili ya Adamu.

<u>3.6.3.3. Ibilisi</u>

Sifa za malaika, kama zinavyosimuliwa na Msimulizi, zinaiweka wazi sifa na nafasi ya Ibilisi katika maigizo haya. Malaika, tunaelezwa na Msimulizi (beti 62-4),

> Nyoyo ni zao ambazo
> Kuasi hawana wezo
> Safi ni yao mawazo
> Mola hushukuria
>
> Si wake wala waume
> Kwa mola wao niseme
> Hawendi naye kinyume
> Kuasi wamuhofiya
>
> Tena sio wakinzano
> Kwa Mungu hawana neno
> Yake huunga mkono
> Kwa mtakaso wa nia

Sifa hizi zinamtenga Ibilisi, ambaye tunafafanuliwa kuwa, ni shetani (ubeti 71). Maelezo haya yanamfanya Ibilisi kuonekana kwenye jukwaa kama kiwakilisho au picha ya uovu, kinyume na picha

ya unyenyekevu inayowasilishwa na malaika.

Mbali na maelezo kuwa ni kiumbe mwovu, tunamwona pia katika umbo lake lisilopendeza. Sehemu ya Maelezo inalidokezea umbo lake wakati Ibilisi anapofukuzwa peponi. Maelezo (ubeti 103) yanatueleza;

> Ibilisi kwa kinyongo
> Atoke upande shingo
> Amefutika kijongo
> Huyo akatokomea.

Mbali na kuwa mwovu, kiumbe huyu pia ana kibyongo. Hii ni kasoro ya kimaumbile ambayo inasisitiza uovu wa Ibilisi.

Mhusika huyu, kama usuli wake wa ushetani ulivyobainishwa, ndiye hasidi wa maigizo haya. Uhasidi wake ni tokeo la kuyakataa maagizo ya Mungu ya kumsujudia Adamu. Kitendo hicho kinalisababisha anguko lake. Makazi na upendeleo aliokuwa ametunukiwa na Mungu unamdondoka. Kuona hivyo, Ibilisi anaazimia kujilipiza kisasi dhidi ya wanadamu. Anaiona satuwa katika kuwapoteza wanadamu kwani ni Adamu, yule binadamu wa kwanza, aliyemkosanisha na Mungu.

Azma ya kumwangusha Adamu ni jambo pekee linalomshughulisha Ibilisi. Katika maigizo haya, kila hatua ya Ibilisi imelengwa kujilipizia kisasi cha kutolewa peponi. Mhusika huyu anatafuta kila nyenzo itakayomkidhia haja yake. Katazo la Mungu kwa Adamu na mkewe, la kuyala matunda ya mti wa haramu, linakuwa nafasi aula kwake. Inayumkinika kuwa, wakati huo ambao Mungu alikuwa akitoa amri hiyo, Ibilisi alikuwa amejibanza mahali asipoonekana na kina Adamu. Mti huu anautumia kama chombo cha kuzushia mafarakano kati ya Mungu na waja wake. Anaupamba mti kwa sifa za kuwa mhimili wa uzazi, anasa mbalimbali, elimu na mambo mengineyo ya kuutamanisha moyo.

Athari ya Ibilisi katika maigizo haya ni kubwa sana. Ingawa anajitokeza mara moja tu kwenye jukwaa, mhusika huyu ana umuhimu wa kulisababisha anguko la Adamu na Hawaa. Anguko hilo linafanikishwa na mbinu pevu anazotumia Ibilisi kulifikia lengo lake. Kwanza, Ibilisi anafahamu barabara kuwa Adamu, si mtu mwafaka wa kukabiliana naye. Pili, imani ya Adamu kwa Mungu wake ni thabiti. Mbali na hilo, Adamu pia ndiye aliyesababisha kufukuzwa kwake peponi. Hivyo basi, haingekuwa vigumu kwa Adamu kumtambua Ibilisi pindi angemzushia vituko vyake. Adamu, kwa namna yoyote, ilibidi aepukwe. Na hata Hawaa anapotoa shauri wakamkabili Adamu wampeleke mtini, Ibilisi (beti 302-3) anajibu;

Hawaa tuza akili
Nia hiyo si halali
Tutapokutwa wawili
Adamu tafikiriya

Dhana atadhani hivi
Twamfanyia vitimvi
Nami sitaki ugomvi
Yenu kuwachafulia

Ibilisi anatoa maelezo ambayo ni ya kuridhisha kwa Hawaa. Maneno hayo, hata hivyo, hayana tija anayoisema Ibilisi. Anachonuia kwa hakika ni kuyavuruga maisha ya Adamu na Hawaa, ingawa Ibilisi anadai kuwa hilo ndilo analoliepuka. Ibilisi anajaribu kila awezavyo asikutane ana kwa ana na Adamu. Hawaa ndiye tumaini lake.

Uteuzi wa Hawaa kama mtu wa kuhujumu, unamfaa Ibilisi kutokana na faida zinazoandamana na uteuzi huo. Jambo hili linamfanya Ibilisi kuwa mhusika aliyekithiri fikra zinazomwezesha kuupata mradi wake. Kwanza, kuumbwa kwa Hawaa kama jambo la kimatokeo, kunaurahisisha ulaghai na uendelezaji wa fitina zake. Analitumia dukuduku la Hawaa la kujua vilivyomo peponi kupuliza

sumu iliyokuwa imemsakama kwa muda mrefu. Baadhi ya mambo anayoyaotelea bahati ni kuwa Hawaa hakushuhudia yote yaliyojiri peponi, ukiwemo ugomvi kati yake na Mungu. Vilevile, anafahamu kuwa Hawaa hangeweza kuwatofautisha malaika na mashetani. Fauka ya hayo, Ibilisi anaielewa barabara sumu ya mwanamke ya kumfanya mumewe amtendee analotaka.

Matembezi ya Hawaa ndiyo yanayompatia nafasi Ibilisi ya kulitimiza lengo lake. Kauli za Hawaa, baada ya matembezi yake, ni umbeya mtupu. Hawaa anadhihirika kuwa mwakilishi wa Ibilisi katika kumkabili Adamu. Ibilisi anahisika, kupitia Hawaa, akimkabili Adamu. Hivyo basi, mhusika huyu ana uwili; kwanza akiwa na umbo na urazini wake, na pili akiwa amemteka Hawaa kifikira. Hawaa anaupoteza urazini wake na kuwa kivuli cha Ibilisi. Hata hivyo, hafaulu katika duru yake ya kwanza ya kumshawishi Adamu; jambo linalomfanya arudi kwa Ibilisi, ambaye kwa wakati huu ni rafiki mwenzi, kutafuta mbinu nyingine.

Ibilisi, akiwa amefanikiwa kidogo katika kumteka Hawaa, anajaribu kutumia mbinu zaidi za kuhakikisha kushiriki kikamilifu kwa Hawaa. Wanapokutana mara ya pili, Ibilisi anadokezewa na Hawaa tuhuma ya Adamu kuwa si mwingine anayehimiza kuliwa kwa tunda isipokuwa ni shetani. Jambo hili linamfanya Ibilisi adai kuwa ni malaika. Anautumia umalaika kama fimbo, kwani hili lingempa moyo Hawaa, kuwa na hakika ya lile analotenda. Mbali na hilo, Ibilisi anatumia vitisho vya mti wa hurulaini, akifahamu barabara kuwa ukewenza kwa Hawaa ni suala linalomchukiza. Kutajwa kwa hurulaini kunauhakikisha ushiriki wake. Mbali na kuuhakikisha uhusika wa Hawaa, yeye mwenyewe pia anaingia mbioni kuona kwamba mpango wake utafanikiwa. Ndipo anaponyapa pasi na

kuvunja unyasi, kupanda mti na kuliangusha tunda zuri mbele ya Adamu na Hawaa (beti 311-12).

Juhudi za Ibilisi zinakamilika wakati Hawaa anapofanikiwa kumshawishi Adamu kulila tunda. Farka kati ya Mungu na wanadamu inakuwa jambo la kiyakinifu. Hivyo basi, si ajabu kuona kwamba uhusika wa Ibilisi kwenye jukwaa unaishia na mawaidha ya mwisho aliyompatia Hawaa.

### 3.6.3.4. Hawaa

Msimulizi katika maigizo haya anatupatia fununu juu ya nafasi anayoicheza Hawaa. Kuumbwa kwake, tunajulishwa, ni tukio la Adamu kutamani mtu wa kumliwaza (beti 136-37). Tamanio hilo linatimizwa na Mungu. Adamu anapolala, anaamka na kumkuta mwanamke ambaye ni;

> Mtanashati wa umbo
> Mwenye sifa ya urembo
> Suraye mithili pambo
> Yavuta kuangaliya

Mhusika huyu, anavyofafanuliwa, ni mzuri sana. Katika bongo zetu, uzuri huu tunaweza tukaumithilisha na mwanamke mzuri ambaye tumewahi kumwona maishani mwetu. Ni uzuri huu ambao ndio unamstaajabisha Adamu. Adamu haamini anachokiona mbele yake. Ndipo;

> Adamu ende karibu
> ilihali aajabu
> Kuona alo sahibu
> Mwanamke alo shamsiya

Adamu haamini anachoona,

> Mno kwa kumtalii
> Awene bie yu hai
> Akamba huyu Hawai
> Mola amenileteya

Uzuri huu ni sharti tuuhifadhi katika bongo zetu kila mhusika

huyu anapotokea kwenye jukwaa. Ni uzuri huu, unaomfanya Adamu arovye rojo mapenzi ya Hawaa hadi ikawa vigumu kwake kumvunja. Si ajabu kwetu kumwona Adamu akimwita mkewe 'siti wa masiti' (ubeti 323); ishara ya kuukiri uzuri wake.

Uzuri wa Hawaa si jambo aliloumbiwa kulitekeleza katika maigizo haya. Uzuri huo ni nyenzo inayokuwa nyongeza ya nafasi ya mhusika huyu. Vilevile, Adamu anapewa mwenzi ambaye si wa kumliwaza tu, bali pia wa kusababisha anguko lake.

Katika maigizo haya, kuna jambo moja muhimu la kuzingatiwa katika kuuelewa uhusika wa Hawaa na jinsi anavyostahili kujitokeza katika maigizo haya. Tofauti na Adamu, Hawaa hakuwahi kufunzwa na Mungu, licha ya kushuhudia matukio muhimu, ukiwemo mchuano wa Adamu na Malaika. Mhusika huyu anajitokeza kama tukio la tamanio la Adamu la kuwa na mwenzi. Ulimwengu aliouingia haufahamu barabara; jambo ambalo linamfanya kuwa windo bora kwa Ibilisi ambaye ameapa kuwatenganisha wanaadamu na Mungu wao. Ibilisi anafahamu yote yaliyotokea peponi, kwani yaliyojiri huko yanamuathiri moja kwa moja.

Anapoumbwa, Hawaa anaenda matembezini. Tendo hili si la kisadfa, kwani kama tulivyotaja, mhusika huyu hafahamu vyema mazingira anayojikuta. Matembezi ya Hawaa, yanaificha siri ndani yake, ambayo ni murua kwa hadhira kuifahamu. Kwanza, matembezi hayo yanakuwa kipoza dukuduku kwa mhusika huyu wa hivi karibuni. Kila kitu anachokiona ni kipya, na hivyo basi, haja ya kuitalii bustani. Azimio hili linatuingiza katika sababu ya pili; Hawaa kuwa windo kwa Ibilisi ambaye ingemuwia vigumu kumkabili Hawaa akiwa karibu na Adamu. Ibilisi anakuwa mwalimu wa kwanza wa Hawaa kuhusiana na mazingira yake. Anaporudi, Hawaa anarudi na

hadithi nyingi zinazohusiana na matembezi yake. Yote anayoyaona hayamshangazi Adamu. Adamu anaelekea kuwa mweledi zaidi wa yale yaliyomo peponi. Ni Adamu anayemuuliza iwapo ameuona mti wa hurulaini (ubeti 171).

Ukembe wa Hawaa katika pepo ndio unatufanya tuelewe milaza anayopigwa na Ibilisi. Hii ni hali ya kimantiki katika kuuona uhusika wa Hawaa. Katika matembezi yake, Hawaa anakutana na Ibilisi anayedai ni Malaika wa Mungu. Dai hilo linamfanya amwite Ibilisi 'shoga' (ubeti 203). Huko matembezini, ndiko anakomweleza Hawaa, 'faida' za matunda ya mti wa haramu.

Hawaa anaonyesha kuwa na yakini kuwa mti ulioharamishwa, ndio wenye funguo za neema katika maisha yao. Hoja anazotoa mbele ya Adamu ni mawazo yanayotokana na 'elimu' mpya aliyoipata huko matembezini. Elimu hiyo inamshangaza Adamu, ambaye anamwona mkewe tofauti na vile alivyomwacha. Adamu (ubeti 202) anasema;

> Mno umebadilika
> Fikira zako zawaka
> Hebu neleza hakika
> Wapi umezipatiya

Dai hili la Adamu linatumulikia uafikiano uliokuwepo kati yake na Hawaa. Maelewano hayo tunayaona yakiyumba na kuhatarishwa kama Adamu anavyotumulikia. Vilevile, kauli hii ya Adamu ni tamko kwa hadhira juu ya uhusika wa Hawaa. Hawaa tunayemfahamu siye tena. Ni katika kujiendea matembezini ambapo Hawaa amekuja na mambo mapya. Anatoa kauli zinazohimiza kuutumia mti wa haramu ambao una uzazi, ujuzi na makazi ya milele (ubeti 191).

Shauku ya Hawaa kuhusiana na mti inamkolea. Wazo hili linatufanya tumwone akikosa satuwa. Ana yakini kuwa, katika mti huu, ndimo mlimofichwa siri kubwa na Mungu. Uzazi ndilo jambo analolitamani zaidi. Nia yake ya kuwa na watoto wengi

watakaoshinda wingi wa malaika inamshinda. Duru ya kwanza ya kumshawishi Adamu alile tunda haileti mafanikio. Hujuma zaidi zinahitajika.

Hawaa, katika mapatano yake na Ibilisi, alikuwa arudi chini ya mti ili waelezane matokeo ya mkutano wake na Adamu. Katika kitendo cha 'Hawaa na Ibilisi', Hawaa tunamwona akiukosa utulivu. Hawaa anashehenezwa uongo zaidi. Ibilisi anahakikisha kuwa yeye ni malaika wa Mungu. Anamshauri Hawaa alile tunda kama njia ya kuitetea nafsi yake na ya kizazi kitakachofuata. Mitego anayoiweka Ibilisi inafana kwa kuizingatia saikolojia ya Hawaa. Anamtisha kwa kumtajia hurulaini waliomo peponi: Ibilisi akiwa anafahamu barabara wivu alionao Hawaa. Tukumbuke kuwa ni mti huo wa hurulaini uliomfanya Hawaa atete kuwa Adamu ana njama za kujiolea mke mwingine (ubeti 177). Ibilisi anawatumia hurulaini kama kitanzi atakachojinyongea Hawaa.

Kutajwa kwa hurulaini kunaisahilisha kazi ya Ibilisi. Hawaa tunamwona akiwa kalitega sikio huku akisihi afundishwe mbinu za kumzuia Adamu na 'uovu' wake. Anamshauri kuwa ulaji wa tunda ndiyo njia pekee itakayomnusuru na janga litakalomsibu. Kwa Hawaa, shoga huyu anamfanyia hisani kubwa. Hawaa anasihi apewe ushauri juu ya kumkabili mumewe; jambo ambalo Ibilisi analifurahia. Ibilisi anamshauri autumie uana wake kama silaha; kwanza kwa ufasaha wa maneno na, atakaposhindwa, amlilie mumewe.

Ibilisi anashinda. Hawaa, kutokana na kutofahamu kwake, anadai kutekelezwa kwa mambo yatakayomtoa yeye na mumewe katika rehema ya Mungu. Kama alivyoagizwa, anauthibitisha ustadi wake katika malumbano mbele ya Adamu. Ubishani wa Adamu, kuwa mti ni jaribu la Mungu kwao, hauwi sababu yenye msingi (beti 323-25).

Hawaa anaanza na faida anazofikiria zinaushamiri mti. Adamu anapoonyesha kutobanduka, Hawaa anasingizia kutopendwa. Anayafungamanisha mapenzi na kula tunda; kwake yakiwa ni mamoja (ubeti 353). Hawaa anafuatilizia na kilio ambacho kinamuathiri Adamu vilivyo. Kwa kufanya hivyo, Hawaa anapata wasaa wa kumtia Adamu tunda mdomoni.

Ulimwenguni ndipo pahala panapomzindua Hawaa na ukweli wa maisha. Pamoja na Adamu wanaihimili misukosuko ya dunia. Wanalima na kufuga wanyama mwitu. Uzuri wake pia unatoweka - hali ambayo inajaribu kutueleweshа kumwona kwetu akiwa duniani. Pia anafahamu kuwa uzazi unamkabili, ikiwa ni lile tamanio lake lilomtoa peponi. Vilevile, anashuhudia kifo cha mwanawe na kustahamili uchungu. Kwa namna iwayo, misukosuko hiyo inamfanya awe mhusika mwenye saburi na upevu wa fikra kuliko yule Hawaa wa peponi ambaye muda wote amekuwa kizuu cha Ibilisi. Unyoofu wa silika yake unafikia kilele na dua anayomwomba Mungu. Msingi mpya wa maisha unawekwa na dua hiyo.

### 3.5.3.5. Kabili na Habili

Hawa ni wahusika wanaopatikana katika ploti ndogo ya uzazi. Uhusika wao unaendeleza kisa kikuu cha Adamu na Hawaa wakiwa duniani. Wahusika hawa wametumiwa kuendeleza mapambano ya wanadamu wa kwanza katika jitihada zao za kukabiliana na maisha yao hapa duniani.

Msimulizi anatueleza kuzaliwa kwa watoto mapacha wa Adamu na Hawaa. Kwa kuwa mapacha walihitajiwa kuoana, Mungu aliutoa mpango wa utekelezwaji wa ndoa kati ya watoto hao. Ikawa kila mtoto wa pacha fulani aowe toka kwa pacha nyingine. Watoto hao

ni wengi lakini ni wahusika hawa wanaopewa uzito zaidi kwa kutajwa majina yao katika maigizo. Mbali na kutajwa huko, matendo yao na athari yake katika kuisukuma mbele ploti ya maigizo haya ni kubwa.

Wahusika hawa wanapotokeza kwenye jukwaa, tayari kuna mgongano kati yao ambao unaendelea, licha ya juhudi za Adamu na vijana hawa kuonyeshwa dalili za kumbainisha mwenye haki kwa Mungu (beti 486-501). Kabili, kwa kuathiriwa na uzuri wa dadaake aliyezaliwa naye pacha moja, anapinga kuolewa kwake na Habili.

3.6.3.5.1. Kabili

Kabili anajitokeza kuwa mhusika hasidi. Kabla ya kujitokeza kwa mhusika huyu, Msimulizi anatufunulia uhasidi wa Kabili, kutokana na visa vilivyojiri. Hukumu ya Mungu kuhusiana na mkweli kati yake na Habili anaipinga. Sadaka yake ya nafaka inasalia wakati moto unaotoka mbinguni unapoteremshwa kuzichukua sadaka zao. Msimulizi pia anatuingiza katika nafsi yake na kuonyeshwa ari ya umwagaji damu inayomchemka Kabili. Kabili tunaelezwa (ubeti 502);

> Na mwishowe katamani
> Kuwa Habili ahuni
> Aondoke duniani
> Kwa kifo kumfikiya.

Kitendo cha kuuwa, kwa Kabili, ndio njia pekee ya kulinusuru baa hilo ambalo Habili amelileta.

Matamanio yanageuka kuwa azma ya kutekelezwa. Kile tulichokiona kama fikra kinadhihirishwa na Kabili mwenyewe. Kwanza anaurudisha kwa mara nyingine ugomvi ambao Habili aliuona umefikia ukingoni. Kwa Habili, sadaka zao tayari zilikuwa zimeshawaamua. Kwa Kabili, ndugu yake ni mkaidi na

anatahadharisha kuwa (ubeti 513);

Uzidipo ukaidi
Nakuapia Wadudi
Sina budi kukurudi
Kwa kipigo kukuuwa.

Kile tulichoonyeshwa kama fikra hatimaye kinatamkwa kama azimio la Kabili. Kuuwa kwake si jambo gumu kwa wakati huu iwapo itabidi almuradi kwa kauli yake /...Ila yangu nitakayo dadangu kuniwachia/ (ubeti 516).

Baada ya majibizano yao makali, Msimulizi anatuelezea yaliyotokea kati yao. Kabili, kweli anamwuuwa ndugu yake. Anafadhaishwa na hilo. Kutembea na maiti ya ndugu yake inapasa tukione kama kitendo cha siku nyingi. Maiti inaoza hadi anapotokea kurabu ambapo Kabili anapata fikra ya kumzika Habili. Mfadhaiko huu unaompata Kabili unatupitikia kwenye fikra zetu; tukimwona waziwazi mhusika huyu akihangaika baada ya kitendo chake cha kiukatili.

3.6.3.5.2. Habili

Habili, kabla ya kumwona kwenye jukwaa, anasawiriwa kama mhusika mwadilifu. Kuliwa kwa sadaka yake na moto toka mbinguni ni ishara ya kuwa katika misingi ya haki. Uhusika wake vilevile unathibitisha uadilifu huo. Ni kupitia uhusika wake ambapo tunadhihirikiwa waziwazi na ukatili wa Kabili.

Anapotishwa na maangamizi, Habili hasiti kukumbusha uamuzi wa Mungu ambao ulikwisha pitishwa na sadaka zao. Anazidi kukumbusha kuwa mauti hayamtishi kwani ni Mungu tu anayemhofu (ubeti 515). Kwa Habili, Mungu tu ndiye wa kutegemewa hata wakati mtu anapokabiliwa na maafa. Habili anakuwa kielelezo cha uchaji Mungu kwa wasomaji wa utungo huu. Na hata Kabili

anapotisha kumuuwa, jawabu ya Habili (ubeti 514) ni;

Iwapo wapenda mno
Mimi nawe mapigano
Kinyosha wako mkono
Wangu sitakunyoshea

Kwa Habili, Mungu tu ndiye atakayemuamulia kwani tayari ameshatangazwa kuwa mshindi.

Habili anakutana na hatima yake. Anauwawa na kakaake. Hatuelezwi iwapo mhusika huyu aliwahi kujihami baada ya majibizano yao. Inavyoonekana, ni Kabili ambaye alikuwa akimuuwa mtu ambaye hakuwahi kujitetea. Msimulizi (ubeti 520) anasema;

Kwisha hayo kutamka
Kabili kaghadhibika
Nduguye akambika
Magongo na kumuuwa.

Inavyodhihirika, Habili ni mhusika anayeamini lile analolisema. Kuuwawa kwake kwa kinyama kunatimizwa bila ya 'kuuinua mkono wake'.

## 3.7. Mandhari

### 3.7.1. Utangulizi

Mandhari ni moja kati ya nembo za maigizo ambayo hutumiwa ili kuzalisha picha kamili ya tajriba ya sanaa za kijukwaa. Wanatamthilia, vilevile, wakiwa na wazo hili katika fikra zao, kwamba tamthilia zao ni maigizo pia, hutumia mandhari ili kuwazalishia wasomaji au watazamaji wao hisi ya maigizo yao ya akilini.

Mandhari, anavyoeleza Kernan (1963), ni ule upenu unaowazingira wahusika na jinsi mwanatamthilia anavyoutumikisha upenu huo hadi ukafikia kuwa kiwakilishi cha ulimwengu ambao wahusika hao wanauishi. Upenu huo hufanikisha usomaji, na

hatimaye kuihisi tamthilia kama maigizo, pindi msomaji anapotafakari na kuidadisi maana ya mandhari inayomkabili (Kelsall 1985).

Wasomaji wa utungo tunaoushughulikia katika muktadha huu wanakuwa hadhira ambayo inashughulishwa na kile kinachothibitika kwenye jukwaa, wakiwa na jicho pekuzi la kufahamu umuhimu wa kila kifaa wanachokiona.

Tunapozisoma tamthilia, aghalabu ni wahusika ambao wanazivuta nadhari zetu zaidi kuliko mandhari. Kupuuzilia mbali kwa mandhari husika hutokana na imani yetu kwamba ni sharti kuwepo na vifaa vya kuutekelezea uigizaji wa mchezo huo. Kwa bahati mbaya, tunayafungia macho masuala nyeti yanayoibuliwa na vifaa vinavyoonekana kwenye jukwaa (Kernan 1963).

Mandhari, ikitangamana na ishara nyinginezo kama vile kitendo na wahusika, inao uwezo sawa wa kuangazia masuala mbalimbali ambayo mwanatamthilia ananuia kuyawasilisha. Katika kitengo hiki, matilaba yetu ni kuangazia jinsi Abdilatif, alivyotumia mandhari au vifaa mbalimbali kwenye jukwaa, hadi vikafikia kuwa viwakilishi vya ulimwengu wa wahusika wake. Wazo hili linamaanisha kwamba, tunalizamia suala la jinsi mandhari inavyofanikiwa kutangamana, na miongoni mwa mengineyo wahusika, na kuweza kutuwezesha kuiona mandhari akilini mwetu. Tuliiangalia mandhari kwa jicho pekuzi, na kuangalia uhusiano wake na maudhui ya maigizo.

### 3.7.2. Mandhari katika Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa

Kupitia lugha, mandhari inayodhihirika katika maigizo haya ni ya aina mbili; mandhari ya ulimwengu wa pili na ile ya

duniani. Mandhari ya ulimwengu wa pili inajumuisha maonyesho yote yanayopatikana kati ya faslu ya kwanza hadi ya nne. Mandhari inayojitokeza si ya kiyakinifu ingawa inaweza ikafananishwa na vitu mbalimbali alivyowahi kuviona msomaji katika maisha yake. Mazingira yanayorejelewa ni ya mbinguni na peponi; yote yakiwa maeneo ambayo binadamu wa siku hizi hawajawahi kuyaona. Mandhari hii, ikiwa ya kidhahania, inatoa fursa kwa wahusika kuwa na ulimwengu mpana zaidi wa kuigizia kuliko ule ulimwengu wa kihalisia wa hapa duniani.

Hadhira inapousoma utenzi huu kimaigizo, inadhihirikiwa na vifaa vinavyopatikana katika ulimwengu wetu wa kawaida. Hii ni mandhari ya ulimwengu tunaoishi. Shamba kubwa la Adamu na mkewe Hawaa (ubeti 432) lenye miti, kwa mfano, ni rahisi kufikirika na kuonekana kwa msomaji, kuliko kiti cha enzi cha Mungu (ubeti 16).

<u>3.7.2.1. Mandhari ya Mbinguni na Peponi</u>

Kama tulivyotangulıza, mandhari ya maonyesho yanayotendeka katika ulimwengu wa pili, hususani ile ya mbinguni, imesheheni mawazo ya kidhahania. Mandhari ya mbinguni, ambayo imo katika usimulizi wa Msimulizi, imetandwa na mazingaombwe. Mazingaombwe hayo, yanazalisha picha ya mandhari changamano, inayowapatia nafasi Mungu, Ibilisi, Malaika na baadaye Adamu kutamba katika ulimwengu mpana zaidi kuliko Adamu na Hawaa au Habili na Kabili hapa duniani. Mandhari hii, inamwezesha Mungu kuwa na uwezo wa kuufikia ulimwengu, na kuvitumia vilivyomo duniani katika kumuumba mwanadamu wa kwanza.

Mbingu, kama anavyotufahamisha Msimulizi, iko juu mkabala na ardhi. Hivyo basi, maonyesho ya mbinguni, tunatarajiwa

tuyaone yakitendeka fikrani mwetu. Huko ndiko aliko Mungu, ambaye yuko juu ya kiti chake cha enzi.

Kiti cha enzi ambacho kinatajwa na kuonekana kwetu kama kiti cha kawaida inapasa tukichunguze zaidi. Ni lazima tuwe na jicho la kudadisi ili kufahamikiwa barabara na kile tunachokiona kwenye jukwaa. Ni kwenye kiti hiki ambapo Mungu anatoa mawazo yake ya kuiimarisha nchi (ubeti 16). Kiti hiki kinaashiria nguvu na uwezo alionao Mungu kwa viumbe wake. Uteuzi wa mandhari hii ambao umetumika kitaswira unazidi kuyahuisha maigizo hususani kuonekana kwake pindi msomaji anapotafakari yote yanayotokea mchezoni. Ni katika kiti hiki ambapo binadamu wa kwanza anaumbwa, kubashiriwa kwake kama mfalme wa ardhini, kiumbe atakayemwaga damu, atakayevunja ibada, na hata kutimuliwa kwa Ibilisi na kugubuliwa ushetani wake.

Maonyesho yanayotendeka peponi, kwa kiasi fulani, yanauvunja udhahania wa mbinguni. Katika mandhari hii, tunaona uwakilisho wa kimazingira ukiwa wa wastani; si wa duniani wala ardhini. Mandhari inayojitokeza peponi ni ile ya bustani ya Edeni. Msimulizi, katika onyesho la 'Adamu Kuwekwa Peponi', ndiye anayechukua jukumu la kutufahamisha kilichopo kwenye jukwaa. Tunaloona mbele yetu ni shamba ambalo ukubwa wake ni upeo wa macho. Shamba lenyewe limejaa vitangu vya miti iliyosongamana. Miti hii imejizalia matunda lukuki, ambayo, tunayaona yakiifanya miti kujiinamia (ubeti 131-32). Mandhari ambamo miti hiyo ya peponi imemea inafafanuliwa pia. Hisi zetu za kunusa zinachemshwa. Tunaihisi shamba, jinsi ilivyokolea manukato (ubeti 132). Mito ya asali inayotiririka pia tunaiona.

Usomaji wa kimaigizo haunuii kuyabainisha mandhari bila ya

kuyatafiti umuhimu wake. Vifaa vyote vinawasilisha ujumbe fulani ambao Abdilatif anazidi kuuendeleza kwa matukio muhimu ya maigizo. Bustani ya Edeni, kulingana na mandhari yake, ni mahala paliposhitadi nyemi. Mito ya asali, manukato bustanini, miti iliyozaa kwa kukithiri na kutojua nini njaa, ni ishara ya kutimia kwa pepo kama mahali palipomakinika. Mandhari ya pepo, vilevile, huweza ikazifafanua hali za wahusika. Adamu na Hawaa, kwa mfano, ni watu ambao wametulia katika raha hii, ingawa baadaye, maisha haya yanamtumbukia nyongo Hawaa. Mkabala na wahusika hawa ni Ibilisi, ambaye kwa kutumia hila, anafanikiwa kujipenyeza peponi. Hapa tuna mhusika mwovu katika mandhari nzuri. Mhusika huyu anaathiriana na mandhari hii, hususani ya mti, kuzusha uhasama.

Bustani, kama tulivyoiona na kufahamu uelelezo wake wa hali ya utuvu uliopo, vilevile, imetunukiwa mti. Mti huu unakuwa mwiko kwa Adamu na Hawaa, si kwa kuutumia tu, bali hata kuukaribia kimasafa. Kutotekeleza hilo kungemaanisha kuangamia kwao. Mti unabaguliwa na vyote vilivyomo peponi. Amri hii ya Mungu inatufanya tuutilie shaka mti huu na matunda yake unapotudhihirikia kwenye jukwaa. Haishangazi kuuona mti huu ukiwa uti wa mgongo wa maonyesho yote ya peponi; jambo ambalo linatufanya tuizamie mandhari hii kwa upana zaidi.

#### 3.7.2.1.2. Mandhari ya mti

Mandhari hii imepewa uzito zaidi kwenye maigizo. Mti huu ndio unaochukua sehemu kubwa ya kuhisika kwa maigizo. Kitendo cha mchezo katika maonyesho ya peponi, ama kinatekelezewa mtini, au kuhusiana nao. Mandhari hii, ikishirikiana na mbinu nyinginezo za kimaigizo, kama vile kitendo na wahusika,

inaeleweka katika misingi ya kuwa kiwakilishi cha dhana za utiifu, uhuru wa uteuzi na vilevile uovu.

Dhana ya utiifu inajitokeza kwa kuzingatia uhusiano wa Mungu na binadamu. Huu ni uhusiano usiokuwa wa kufu moja. Adamu na Hawaa wanapowekwa peponi, wanaruhusiwa wajiruzuku na chochote, isipokuwa /Matunda ya mti ule/ (ubeti 150). Mti huu anaouashiria Mungu, si mwingine ila mti huu haramu. Tayari Mungu amejitokeza kuwa na amri juu ya viumbe wake. Kwa hivyo, uhusiano utakaofana ni ule ambao utakuwa wa kihafidhina. Kuukaribia au kula matunda ya mti huu kungemaanisha badiliko la hali iliyopo. Mti huu unapodhihirika, hatuna budi kuuona kama kiwakilishi cha mkataba kati ya Mungu na binadamu. Mti ni kipimio cha uthabiti wa Adamu na Hawaa; kuwa si wakaidi katika kuzitii amri za Mungu (ubeti 149). Mandhari hii inafanikiwa katika kuipata hisia kamili ya ahadi iliyopo kati ya binadamu na muumba wake. Hawaa anapong'ang'ania kuwa mti huo una neema, tunapata msisimko fulani na kumhurumia kwa kuwa utiifu wake kwa Mungu unahatarishwa.

Kago wanayowekewa baba na mama, mwishowe inavunjika. Kuvunjika kwake ni chini ya mti, ambapo, kitendo cha kulila tunda kinatekelezwa. Hawaa, kupitia vishawishi vyake vya kike, anamlisha Adamu tunda haramu. Adamu, ambaye wakati wote anajikinga na kuidhulumu nafsi yake, anajikuta kwenye njia panda. Kwa kulila tunda, atakuwa amemuasi Mungu wake kwa kumtii mkewe. Kwa kulikataa tunda hilo, atakuwa amemkana mwanadamu mwenzake. Adamu anamfuata mkewe, na hivyo basi, kumuudhi Mungu. Utiifu unakuwa jambo la sahau.

Mbali na kuwa kiashiria cha utiifu, mti huu pia unafafanua uovu. Chini ya kivuli cha mti, kwa mfano, ndipo anapofanyiwa

sharuti Hawaa kukutana na Ibilisi. Inafaa tudadisi ni kwa nini mti ndio umechaguliwa kama mahali pa kukutana na wala si karibu na mito ya asali. Hawaa anapomchukua Adamu kwenda naye matembezini, hatima yao ni chini ya mti pia. Mandhari inasuhubiana na wahusika ili kufikia ufanisi wa kitendo cha maigizo.

<u>3.7.2.2. Mandhari ya Duniani</u>

Mandhari hii inadhihirika pindi wanaposhukishwa Adamu na Hawaa kutoka peponi. Mandhari iliyopo hairidhishi na inakatisha tamaa. Mandhari hii inasisitiza shida ambazo zinaelekea kuwakabili Adamu na Hawaa. Ustadi wa Msimulizi unatufanya sisi wasomaji tuione mandhari na kuihisi shida iliyopo hasa tunapoilinganisha na mandhari ya peponi. Msimulizi (beti 379 - 381) anatueleza;

> Adamu akitizama
> Pamoja na wetu mama
> Waona wamesimama
> Nchi isiyo mimeya.
>
> Ila kuona milima
> Mikubwa iliyo wima
> Na njia zote si njema
> Kwa mawe yalivyojaa.
>
> Kuchungua kila pembe
> Haina watu viumbe
> Ila ngamia na ng'ombe
> Na mito kupitiya.

Mandhari inayofafanuliwa inawiana na ile inayopatikana kwenye majangwa. Mahali wanapojikuta Adamu na Hawaa hapana miti. Kuna milima mikubwa na njia zilizozongwa na mawe. Kisha kuna mito na wanyama wa aina mbili tu; ngamia na ng'ombe. Mandhari hii tunaiona barabara. Ndipo Knappert (1967) akataja kuwa mandhari hii inalandana na Hijaaz au Yemen.

Kwa kadiri mandhari hii inavyolikirihi jicho la wasomaji, ndivyo wahusika Adamu na Hawaa wanavyoanza kulaumiana. Kila mmoja anamlaumu mwengine kwa kutolewa peponi. Kauli zao zimeoanishwa vizuri na mandhari iliyopo.

Kutokana na mpango wa Mungu kuwa mwanadamu ataishi duniani kama khalifa wake, hadhira inatarajia mabadiliko katika mandhari wanayoishi Adamu na Hawaa. Wahusika hawa walijitahidi kupanda miti ambayo hatima yake ikawa (ubeti 432);

Bibi Hawaa na Baba
Wakawa na kubwa shamba
Miti miraba miraba
Shambani imekuliya.

Abdilatif amefanikiwa kueleza kila aina ya mandhari ambayo wahusika wake wanajikuta. Mandhari mbalimbali zinawiana na hali za raha au shida iliyopo.

### 3.8. Kinaya Drama

Kinaya drama ni ala ya lugha ambayo inampa fursa msomaji kufahamu maana halisi iliyokusudiwa na mwandishi. Katika kinaya drama, mhusika aghalabu hutenda au husema mambo ambayo yeye mwenyewe hayafahamu uzito na athari yake kwake. Kwa upande wa hadhira, mhusika huyo huwa amefahamika kama mtu ambaye tayari ana kasoro fulani. Lile analolizungumzia mhusika huyu hatimaye huibuka kuwa jambo linalomtanza yeye mwenyewe na pengine hata kusababisha maafa fulani kwake.

Wasomaji wa tamthilia ya Oedipus Rex, kwa mfano, wanafahamu barabara kuwa yule mwuaji ambaye anatafutwa kama kisababisho cha maafa ya mji wa Theba, si mwingine ila Oedipus mwenyewe, anayekula yamini kuwa mwuaji huyo sharti aangamizwe. Oedipus, anapotoa kauli hii, anaitoa kwa dhati ya nafsi yake, bila

kufahamu kuwa yeye mwenyewe ndiye mwuaji aliyeamrisha asakwe (Carpenter 1975). Huu ni mfano wa kinaya drama ambao mwandishi Sophocles anautumia kuijulisha hadhira yake yale ambayo, hapo baadaye, ndiyo yatakayokuwa chanzo cha anguko la Oedipus.

Kisa chenyewe cha Adamu na Hawaa, kama kinavyojitokeza katika The Holy Qur'an, kinatoa msingi imara wa kinaya drama ambacho Abdilatif amekitumia kama nyenzo ya kujengea maigizo yake. Ni katika misingi hii, ambapo tunamwona Abdilatif akiifahamisha hadhira yake yale ambayo wahusika mbalimbali yangewasibu. Wahusika hao, kama ilivyo ada ya kinaya drama, hawafahamu uzito wa yale wanayotamka.

Katika utungo huu, takribani kila mhusika anaathiriwa na mbinu hii. Adamu hata kabla kuumbwa kwake, anabashiriwa kuwa angeishi duniani. Anapoumbwa na kuwekwa peponi, hadhira tayari imetayarishwa kumwona kama mpita njia tu. Peponi si mahali pake, kwani azma ya kuumbwa kwake ni /Nchini ajenge nyumba, Na mashamba kulimiya/ (ubeti 17). Vitendo mbalimbali anavyotenda na vinavyomsibu Adamu, vinamwelekeza kuiandama kudura yake ya kuishilia ardhini.

Katika faragha yake na Mungu, Ibilisi, miongoni mwa viumbe vyote vilivyoko mbinguni, ndiye anayejulishwa kuwa mmoja kati ya watumishi wa Mungu angekuwa muasi. Ibilisi, kuambiwa hivyo, haamini kuwa kiumbe duni cha Mungu kinaweza kuikana amri ya Muumba. Msimulizi (Ubeti 78) anaeleza kuwa;

> Ibilisi akakuli
> Akuasiye jalali
> Baada zako fadhili
> Laana namuombeya

Ibilisi, anapoyasema haya, ana dhati na kile anachozungumza. Fikira kuwa laana hiyo alikuwa akijiombea mwenyewe haimjii.

Lakini hadhira, tayari inajua kuwa Ibilisi ni shetani; kwani Msimulizi (ubeti 71) anadokezea kuwa;

> Kwavyo ilivyo jueni
> Ibilisi ni sheitani
> Alokuzwa na Mannani
> Alipokinyenyekeya.

Baada ya faragha hiyo tu, Ibilisi huyo huyo aliyeapiza na kulaani, ndiye anayekataa amri ya Mungu ya kumsujudia Adamu. Sababu anazozitoa ni pamoja na kuwa yeye aliumbwa kwa zana za kifahari zaidi kuliko Adamu. Huu ni ufidhuli ambao Ibilisi anamfanyia Mungu wake (beti 82-7). Mja yule ambaye alitabiriwa na Mungu kuwa angeasi haja yake anakuwa Ibilisi (ubeti 77). Lakini Ibilisi anaikubali hali yake na kuandama lile analotaka. Anaikabili kudura ya Mungu aliyopangiwa bila kurudi nyuma: tofauti na Adamu aliyerudi kuomba msamaha.

Hawaa, kama vile Ibilisi, ametumiwa na Abdilatif kuendeleza mbinu hii ya kinaya drama. Hawaa anapotokea kwenye jukwaa, tayari hadhira ina vuguvugu la ubaya fulani unaofungamana na kuutumia mti wa haramu. Amri ya Mungu kuwa Adamu na Hawaa walikuwa na uhuru wa kula chochote kilichomo peponi isipokuwa mti huo, ni onyo linalomfanya msomaji kuwa na hisia kuwa mti huo si muruwa kwa wahusika hao.

Ibilisi anakuja na habari nyingine. Anamshauri Hawaa kuwa mti huo umefanywa mwiko kwa minajili ya kumkosesha yeye na mumewe kizazi, anasa, na mambo mbalimbali ya tunu (beti 190-7). Hawaa anajitwika habari hizo na kuzishikilia kimsahafu. Anajitahidi hadi kufikia ufanisi wa lile aliloshauriwa na Ibilisi. Ni baada ya kupata tija na hatima mbaya ambapo mhusika huyu anazinduka na kufahamu kuwa Ibilisi hakumtakia heri.

# SURA YA NNE

## MBINU ZA KIMAIGIZO KATIKA 'KUTENDANA', 'MNAZI: VUTA N'KUVUTE' NA 'USINIUWE'

### 4.1. Utangulizi

Kama tulivyodokeza katika sura ya kwanza, tungo hizi zinapatikana katika diwani ya Abdilatif ya Sauti ya Dhiki (1973). Sura hii imeangalia jinsi mshairi huyu anavyozitumia mbinu za kimaigizo katika kutuhisisha tungo zake. Mbinu tulizozishughulikia ni pamoja na lugha, kaida za kijukwaa, ploti, kitendo, wahusika, mandhari na maleba. Kwa kufanya hivyo, tumeibuka na aina ya usomaji ambao umetuwezesha kuyaona maigizo yakitendeka katika jukwaa la akili zetu.

### 4.2. Lugha ya Kimaigizo katika Tungo

Lugha, mbali na kuwa nyenzo ya mawasiliano yote, imetumika pia kama mbinu inayojisimamia dede katika kutoa hisi na maana ya maigizo. Katika sehemu hii, tumeangalia sifa kuu za lugha, hususani jinsi lugha hii ilivyotumika kimaigizo, ghairi ya ilivyotumika kishairi kama tulivyobainisha katika sura ya pili.

Lugha aliyoitumia mshairi huyu ni ya kidrama. Tungo za 'Mnazi: Vuta N'kuvute' na 'Kutendana' zinatumia majibizano. Maigizo ya 'Usiniuwe', ambayo ni uzungumzi wa Mtoto pekee, pia yanaashiria kujumuika kwa wahusika wengineo wakiwemo Mama, Uhai, Haki na Mauti, ingawa hatuwaoni wahusika hawa wakitoa kauli yoyote. Vile kauli zinavyoweza kutueleza mengi kuhusu mhusika, ndivyo kimya cha wahusika hawa pia kinakuwa sehemu ya majadiliano. Wahusika hawa, mbali na kutotamka lolote, wanamweleza Mtoto hisia zao kupitia kimya. Chambilecho wahenga, kimya kingi kina mshindo.

Lugha ya maigizo haya inachukua mfumo wa nipa nikupe; kwamba

kila mhusika anatarajiwa ashiriki kikamilifu katika mazungumzo. Usuhubiano wa wahusika, kwa kuitumia lugha, ni jambo la kimsingi katika maigizo haya. Mhusika anayemsaili mwenzake, kwa mfano, anatarajia apate jawabu toka kwa mhusika mwingine. Alii anaposema /Ndugu ulo mnazini ... Utashuka au la?/, anauliza akitarajia kwamba Badi atamjibu ipasavyo. Abdilatif, anamfanya Badi atoe kauli yenye mashiko /Ndugu tini ya mnazi, nilo juu nakujibu.../. Huu ni mtindo halisi wa kidrama ambao wahusika wanafanywa wajibizane kwa kuuzingatia muktadha waliomo.

Kulingana na umuhimu wa kusisitizwa kwa utendaji katika drama, lugha ya maigizo haya, pia tunaitarajia iwape uwezo mkubwa wahusika wake kuicheza. Kauli ya Mtoto (ubeti 15) /Ngoja! Usinisongowe, niweka mama niweka.../, ni mfano mzuri wa jinsi lugha ya maigizo haya inavyoweza kumpa fursa mhusika Mama na Mtoto kuicheza. Mama, ingawa hazungumzi lolote, anatudhihirikia akiupunguza urefu wa kimasafa kati yake na Mtoto ili autimize ukatili wake. Tunamwona Mtoto akimuona mamaake akikaribia kumbana koo, na hivyo basi, kumkanya asubiri ajitetee zaidi. Hivi ndivyo lugha ya maigizo ya 'Kutendana' ilivyo. Mwanamke, akiwa ametiwa uchungu na maudhi ya Mwanamume, anapewa lugha inayotuonyesha uchungu huo. Lugha iliyotumika inadhihirisha machungu hayo yanayoelezwa kwa muhtasari na 'maelezo' kuwa Mwanamke alikuwa amebadilikwa na rangi ya uso wake, akiongea kwa ukali, huku mwili ukimcheza. 'Maelezo' haya yanatudokezea uwezo wa lugha iliyotumika katika kuwawezesha wahusika wake kuitenda, na hivyo basi, kuonekana kwa wasomaji.

Dhana ya uwezo wa kutendwa kwa lugha inatuingiza kwenye sifa nyingine muhimu ya lugha ya mshairi huyu. Sifa hiyo, ni ile ya

kutumika kwa lugha inayoonyesha picha halisi za kidrama, zinazotokana na upangwaji stadi wa lugha. Picha na hali zilizotumiwa ni zile zinazotuwezesha, kwa mfano, kuuona mnazi na mkwezi wake Badi, huku Alii akiwa chini ya mnazi huo. Vilevile, tunamwona Mtoto akiwa tumboni katika 'Usiniuwe'. Mwanamke na Mwanamume nao, katika 'Kutendana' tunawaona wakikabiliana, dirisha likiwa kifaa kinachowatenganisha.

Kutokana na uwezo wa kutendwa kwa lugha ya maigizo haya, tunaibukiwa na suala la kuzuka na kuendelezwa kwa matendo yanayotendwa na wahusika. Mwanamume anajitokeza akitaka afahamishwe iwapo 'atapewa'. Hata kwa mkopo, anadai yu radhi kukopa. Kauli hii ya mwanzo tunaiona ikiipa ploti ya maigizo ya 'Kutendana' msukumo; kimasafa na kimaudhui. Kauli hiyo inatuwezesha kujionea matukio mengine ambayo yana uhusiano wa moja kwa moja na 'kupewa' huko anakokuzungumzia Mwanamume. Unyumba uliokuwepo kati ya wahusika hawa, maudhi ya Mwanamume kwa Mwanamke, uchu uliomsakama na hatima inayompata Mwanamume, ni baadhi ya mambo tunayoyashuhudia.

Maigizo ya 'Mnazi: Vuta N'kuvute' pia yana sifa hii. Suala la kushuka au kutoshuka chini ya mnazi, mbali na kuwa kiini cha mvutano, linaipa ploti msukumo wake unaostahili kwa kuzizingatia kauli za wahusika. Kutokana na mazungumzo hayo, tunafahamikiwa na udhalimu uliokuwepo, na ambao bado unamshamiri Badi. Ni mazungumzo hayo hayo, yanayotufahamisha juu ya azma ya Alii ya kutumia mabavu baada ya ushauri wake kukataliwa na Badi. Lugha ya Abdilatif, ndiyo inayowapa wahusika hawa fursa ya kuwa watendaji wa matendo mbalimbali, na hivyo kuipa ploti ya maigizo yake umbo la kiyakinifu.

Matumizi ya lugha ya kishairi ni jambo alilolizingatia Abdilatif. Lugha hii ni ya kitaathira (Mazrui na Syambo 1992). Nafasi ya lugha hii katika maigizo haya, kama tulivyoona katika sura ya pili, ina umuhimu wa kutuhisisha na hatimaye kutuibulia maana na tajriba ya maigizo yake. Kwa kuzichota zana mbalimbali za lugha, Abdilatif, anafanikiwa kuiwezesha hadhira yake kuyahisi maigizo yakitendeka kwenye bongo zao.

## 4.3. Kaida za Kimaigizo

Tungo hizi, isipokuwa 'Mnazi: Vuta N'kuvute' zinatumia kaida mbalimbali za kijukwaa. Katika utungo huu wa 'Mnazi Vuta N'kuvute', Abdilatif anawaacha wahusika katika majadiliano yao bila ya kutumia usaidizi wa 'Maelezo' au 'Mnong'ono kwa msomaji' kama alivyofanya katika maigizo ya 'Kutendana'. Hivyo basi, tumeangalia kaida za maigizo ya 'Kutendana' na 'Usiniuwe'.

### 4.3.1. Maelezo

Kaida hii, kama neno lenyewe linavyoashiria, ni ufafanuzi unaojitokeza kila baada ya majadiliano yaliyopo kati ya Mwanamke na Mwanamume katika maigizo ya 'Kutendana'. Kaida hii haikutumika kisadfa, bali ina nafasi muhimu katika kuyahisi maigizo.

'Maelezo' si vituo vya kimsimu kwa ajili ya vituo tu. Hii ni kaida yenye uamilifu wa, miongoni mwa mengineyo, kutoa maelezo zaidi na hali za wahusika, kukipanua na kukikuza kitendo cha maigizo hadi kufikia hatima yake. Vilevile, kaida hii inatoa maelezo yanayohusiana na mandhari. Mbali na hayo, vituo hivi

vinaitafakarisha hadhira juu ya yale yaliyojiri na yatakayojiri katika maigizo haya.

Maigizo ya 'Kutendana' yanapoanza, akili zetu zinashuhudia ugomvi kati ya Mwanamke na Mwanamume. Ugomvi huu, ambao ni msingi wa kitendo cha maigizo haya, hatuufahamu usuli wake. Tunapozidi kuyatafakari majadiliano yao, ndipo tunapofahamu 'ugonjwa' aliokuja nao Mwanamume ili apewe 'tiba'. Majadiliano yao yanapoisha na kujitokeza kwa 'Maelezo', tunakihisi kitendo na wahusika wenyewe tu. Ni katika 'Maelezo' ambapo baadhi ya mambo muhimu, yanayohusiana na mgongano kati ya Mwanamke na Mwanamume, yanaibuliwa.

Kupitia 'Maelezo', tunafahamu kuwa Mwanamke alikuwa amejinyosha kitandani. Hili ni baada ya kujirembesha kwa vitu kama vile wanja na manukato. Hali inayosawiriwa na 'Maelezo' ni ya utuvu kabla ya kutokeza kwa Mwanamume. Utuvu huo unatoweka na mahala pake kuchukuliwa na kugongwa kwa dirisha. Ndipo Mwanamke, baada ya kusita, anapoamua kufungua dirisha na kuchungulia nje. Hapo ndipo anapomwona Mwanamume, na baada ya muda wanaanza malumbano yao (uk. 104-105). Maelezo haya yanakuwa sehemu muhimu ya ujengaji wa ploti. Hizi ni habari za kiufunuo zinazokuwa msingi au uandaliwaji wa vitendo vikuu katika maigizo haya.

Maelezo pia yanatueleza kwa ufasaha wakati uliopo. Ni kupitia kaida hii ambapo tunafahamu kwa tafsili ugeni wa Mwanamume katika eneo alilopo; kumbe vile /Nyezi nyingi zimesia, tangu walipokutana/. Miezi mingi hii iliyopita hatuifahamu ni mingapi. Maelezo hayakomei hapo bali yanaeleza saa ambayo kitendo hiki kinatokea; saa tano za usiku zimekwishapita (uk.

103). Bongo zetu zinaliona giza totoro lililofunga kila mahala hapo nje aliposimama Mwanamume.

'Maelezo' haya ya wakati ni chatni inayoongeza utamu wa kuhisika kwa maigizo tunayoyashuhudia. Kwanza, tunaona kwa uwazi mshangao unaompata Mwanamke. Haiyumkiniki kwa watu waliozoeana kupoteana kwa muda mrefu hivyo. Mwanamume, kwa upande wake, tunamhisi akiwa mgeni mahali ambapo tunamtarajia pawe pake. Hivyo basi, hatushangai kumwona Mwanamke akiujibu ukatili wa Mwanamume kwa kigezo cha muda aliojitenga naye. Pili, saa ambayo Mwanamume anajitokeza inatupatia picha kamili ya msisimuko anaoupata Mwanamke. Kwa hakika, kupindukia kwa masaa na giza totoro linaloandamana na masaa hayo, ni sababu tosha ya kumuogofya Mwanamke. Fauka ya hilo, hadhira haitaacha kujisaili uzito wa shida iliyomkabili Mwanamume, hata akawa anajitokeza wakati kama huu. Bila shaka tunapata hisia kwamba ndwele iliyompata Mwanamume ni ya kipekee. Malalamiko yake yanatuelea vyema katika misingi hii.

Kauli za wahusika zinapoambatanishwa na vitendo vya kimwili huyapa maigizo uhai zaidi. Mpiko wa viungo hivi viwili hujengana na kuwasilisha, kwa uwazi zaidi, fikra na hisia za wahusika. Kaida hii ya 'Maelezo' inalifikia lengo hili kwa kuwa, inajitokeza kama maelekezo ya jinsi wahusika wanavyostahili kuvitekeleza vitendo vyao. Kwa wasomaji, maelezo yanatusaidia kuviona vitendo mbalimbali vinavyoambatana na kauli za wahusika tunaowaona kwenye jukwaa la bongo zetu. Ubeti huu unatoa mfano aula;

Tangu hapo mwanamke, akisema kwa ukali
Na rangi ya uso wake, ikawa imbadili
Mwili umtetemeke, mkali ja pilipili
Kwa sababu ya mwenzake, alivyo kumfidhuli

Mwanamke angali akiviuguza vidonda vya moyo. Uovu aliotendewa hausemeki. Amevumilia ukiwa na shida zilizompata, kwa miezi sasa, bila kumwona Mwanamume. Tija yake, baada ya machungu yote, ni kashfa za uongo; Mwanamume akidai kuwa 'amegeukiwa' kwa sababu ya tamaa iliyomshika Mwanamke. Ufidhuli wa Mwanamume, na ile hakika yake kuwa Mwanamke hana namna nyingine ila kumtimizia haja yake, ni baadhi ya mambo ya kuikirihi roho. Maudhi haya ndiyo yanayompandisha mori mwanamke. Anayakumbuka, kwa uchungu, mateso aliyopata akijaribu kumuengaenga Mwanamume angalau apate kuridhiwa. Ndipo maelezo yanapojitokeza kutusawiria kwa undani zaidi vitendo vya kimwili vinavyoambatana na kauli za Mwanamke. Tunamwona Mwanamke, waziwazi, akiwa amesakamwa na hasira. Hasira hizo zinaandamana na ukali wa sauti. Masikio yetu yanafanywa yahisi makali hayo ya sauti pindi Mwanamke anapoongea. Vilevile, uso aliouvaa umesawajika, huku mwili ukimcheza kutokana na biwi la hasira lililomsakama. Fafanuzi hizi, ingawa hazielezi hisia zote za Mwanamke, zinatoa picha ya mtu mwenye hasira. Abdilatif, kupitia kaida hii, anamsahilishia msomaji wake kazi ya kujizalishia mwenyewe vitendo hivyo akilini mwake.

Kaida ya maelezo inajitokeza kama nyenzo ya kutoa maelezo ya kiufunuo yanayohusiana na wahusika. Kaida hii, kwa mfano, inaeleza kani ya Mwanamume ya kutaka kukidhiwa haja yake hata baada ya msusuiko anaopata toka kwa Mwanamke. Tunaelezwa kwa mfano, kuwa;

> Mwanamume alidhani, ni maneno ya dhihaka
> Mwanzo hakuyaamini, Bibi alikitamka
> Hakujuwa mwafulani, kwamba mambo megeuka
> 'Kiona kana zamani, 'tapata anachotaka

Kumbe kani yake ina mashiko, kwani ilikuwa ni jambo la kawaida kukidhiwa haja yake. Kawaida hii imekuwepo kwa muda hadi ikawa

kama sheria; Mwanamume aje wakati wowote na afanyiwe lolote alilotaka. Ndiyo maana;

Hakuiona sababu, ya bibiye kumyima
Itakwendaje muhibu, leo awe atagoma
Hajapata kujaribu, maisha yetu mazima
Akawaza taratibu, na kwenye moyo kusema

Maelezo, kwa ufupi, yanamulika misingi ya kani ya Mwanamume kwa kuiingia nafsi ya mhusika huyo na kutuonyesha fikra zake. Katika fikra hizo, ni imani kwamba Mwanamke anamdhihaki kwani haikuwa kawaida yake kumfanya hivyo. Tunaoupata ni mwanga wa kiufunuo unaohusiana na tatizo la mazoea yaliyokuwepo hapo awali kabla ya kugeuka kwa mambo. Hoja hii inatufanya tuuelewe zaidi uhusika wa Mwanamume, hususani ile kani yake ikiwa imetokana na mazoea hayo.

### 4.3.2. Mnong'ono kwa msomaji

Kaida hii, kama ile ya Maelezo, inajitokeza katika maigizo ya 'Kutendana'. Uzito wa kaida hii unatokana na kuuafiki umuhimu wa hadhira katika maigizo yoyote. Kaida hii inaanza na mwito wa kuivuta nadhari ya msomaji kwa kusema

Ndoo n'kunong'oneze, au tunong'onezane
Nilonayo n'kweleze, ya maana tupatane
Ndoo kwangu jijongeze, sitaki tusilikane
Jifite sijitokeze, kwamba tusionekane

Picha inayochorwa na kaida hii, ni ile inayokubaliana na kuwaona wasomaji kama washiriki kamilifu wa maigizo haya, ambao wana uwezo wa kudadisi masuala mbalimbali yanayojitokeza katika maigizo yenyewe. Msimamo unaochukuliwa na kaida hii unaelekea kuzipinga nadharia za kimapokezi zinazomwona msomaji kama ghala la kuhifadhia 'hekima' za mwandishi (Senkoro 1987).

Kaida ya 'Mnong'ono kwa msomaji' inayafunga maigizo ya

'Kutendana'. Kaida hii ni nyenzo ya kiuchanganuzi inayoichemsha hadhira kwa maswali yanayoambatana na matukio ya maigizo haya. Kupitia maswali na hoja mbalimbali zinazotolewa, hadhira inatarajiwa ichuje na itoe tathmini yake katika kubainisha makosa baina ya watenzi wawili: Mwanamke na Mwanamume. Baadhi ya maswali yanayoulizwa ni iwapo Mwanamke yuko huru na lawama zozote kwa kumdekeza Mwanamume hadi akaona ni haki kwake kutimiziwa lolote analotaka (uk. 108). Vilevile, kaida hii inasaili mantiki ya Mwanamume kuwekwa kinyumba badala ya kumweka Mwanamke. 'Mnong'ono' pia unaiajabikia hulka ya huyu bwana ya kujifanya hana namna za kuzumbua lolote, hata iwapo ni kwa kuuza kunazi (uk. 109).

Maswali haya ni ya kimjadala. Mjadala huo utafana pindi hadhira itakapokuwa imefuatilia kwa makini maigizo iliyoyashuhudia. Kwa kuitumia mbinu hii ya kuishirikisha hadhira, muhtasari wa maigizo, hasa katika kuizamia dhana ya kutendana, unatolewa. Kwa kuizingatia kaida hii inayowalenga wasomaji wenyewe, kuhisika kwa maigizo ni jambo linalotekelezwa na Abdilatif.

### 4.3.3. Uzungumzi Nafsia na Uhusika Bubu

Tumezitumia istilahi hizo mbili kuwarejelea wahusika wane wanaojitokeza katika maigizo ya 'Usiniuwe'. Tunapolisoma andiko hili la 'Usiniuwe', tunathibitikiwa na uzungumzi wa mhusika mmoja tu; mtoto ambaye yungali tumboni mwa mamake. Mtoto huyu ndiye anayewasilisha malalamiko yake kwa Mama, Uhai, Haki na Mauti. Maigizo yote yanaendelezwa na kauli za Mtoto pekee.

Kwa upande wa pili, wasomaji wanapasa wawaone Mama, Uhai,

Haki na Mauti, wakiwa wahusika wanaoshiriki kikamilifu katika maigizo haya. Ingawa hakuna hata mmoja kati yao anayetamka neno kumjibu Mtoto, mwandishi amewatumia kama njia ya kuendeleza maigizo yake. Kutozungumza kwao kunawasilisha fikra na mawazo yao, sawa na Mtoto anayejaribu kueleza yanayomsibu kwa wakati uliopo. Huu ni uhusika bubu ambao ungefaa uangaliwe kama kaida inayotumika katika maigizo haya ya 'Usiniuwe'. Dhana kuu inayojitokeza ni kwamba majadiliano ya ana kwa ana sio njia pekee ya kuyafanikisha maigizo. Kimya, kama vile kauli zinazotolewa na mhusika kwa mhusika mwingine, kina uwezo wa kuwasilisha hisia za mtu kwa kutegemea muktadha fulani. Uhusika bubu umetumika kuzidhihirisha nguvu za kimya kama njia ya mawasiliano.

## 4.4. Ploti

### <u>4.4.1. Ploti katika 'Kutendana'</u>

Maigizo haya ni kielelezo cha ploti iliyojengwa na mwandishi kwa kuzingatia kipengele cha kusababishana. Vitushi vyote vinatiririka, ingawa mwandishi ameyatonea maigizo yake mbinu rejeshi.

Ploti ya maigizo ya 'Kutendana' inaanza na kuwashuhudia wahusika Mwanamume na Mwanamke wakiwa wamezama katika lindi la majadiliano yao. Hali iliyopo si ya maelewano kwani nia na madhumuni ya wahusika hawa yanapungiana mikono. Mwanamume, kwa upande mmoja, ameshikwa na kiu ambayo mfariji wake hayuko tayari kuizima. Kutoelewana huko kunaukitia mizizi mgongano, yaani pande mbili zinazoabiri kuyatimiza malengo mawili tofauti. Mgongano huu ni nembo muhimu ya ploti ambayo inaifanya hadhira kuupata msisimko wa kihisia unaotokana na taharuki. Kwa

kuuangalia mgongano uliopo, hadhira imefanywa iivute nadhari, ili ifahamu nani kati ya wababe hawa wawili, ataibuka na ufanisi, na kwa hoja gani.

Abdilatif anautumia uchu kuwa kifaa cha kuipa msukumo ploti yake. Anamsawiri Mwanamume kama mhusika aliyesakamwa na uchu. Matumaini ya kutimiziwa takwa lake hayapo. Haelekei kamwe 'kufua dafu' lake. Zionekanazo ni juhudi za mfa maji; Mwanamume akitapia kila ambacho kingemnusuru na janga lake. Abdilatif anamdhihirisha Mwanamume akiwa amekabiliwa na hali ya uvunjifu, akibakia na /Kama utanipa.../; ikiwa ni ishara ya kushindwa.

Uchu unatumiwa kama nyenzo ya kuiendeleza hadithi na majadiliano kwa jumla. Mwanamume, pamoja na dalili anazoziona kuwa hana lake, ametia migati bado, kwani lililomsibu ni ndwele isiyoweza kuponyeka bila usaidizi wa Mwanamke. Kwa kupewa 'ndwele' isiyokuwa na kifani, inabidi Mwanamume amtafute mwenzi ambaye angempunga 'pepo' aliyemkaa kichwani. Fungamano la ndwele hii, na haja ya usaidizi toka kwa Mwanamke, linaelezwa kwa muhtasari na Mwanamume anaposema;

> Mwenziyo n'nalemewa, si dhihaka n'semayo
> Sina pa kwenda itowa, hii hamu nilonayo
> Na hata wewe wajuwa, kwamba sina badaliyo
> Ni mgonjwa nauguwa, na dawa yangu ni hiyo

Kwa ustadi, mshairi huyu anatujengea msingi wa ploti ambayo inategemea kipengele cha usababishano. Mwanamume amefanywa kuwa mhitaji. Uhitaji huu ni mithili ya moto unaomuunguza ndani kwa ndani maungoni mwake. Upande wa pili, ni Mwanamke ambaye amefanywa kuwa mmiliki wa funguo za dafina ya kuizima kiu hiyo, iwapo ataafiki analoelezwa na bwana huyu. Tunachoona ni juhudi za kimaandalizi, ambazo kwazo, mshairi huyu anaipatia ploti yake msukumo unaohitajika kuipeleka mbele; hasa kwa kuzingatia hali

iliyopo, na kutilia maanani kwamba wahusika hawa wamefanywa wawe wamewahi kuishi kinyumba. Hata hivyo, Mwanamke hashughulishwi na pepo duni anayejitokeza siku za shida tu.

Mjadala mpevu unaozuka, ingawa unaranda kwenye masuto na masimbuliano tofauti tofauti, unazingatia na kuupa mwanga mkinzano wa ama kupungwa au kutopungwa kwa pepo wa Mwanamume. Mwanamume anajiliza kuwa kaemewa huku akitoa ushahidi wa masafa aliyoyaabiri, alivyoshajiisha mvua na giza ili kuitafuta afueni kwa Mwanamke. Mwanamke anaziona rai za Mwanamume kama hadithi zisizokuwa na nafasi katika ulimwengu wake; jambo linalomzuzua Mwanamume, anayedai kuwa amegeukiwa.

Mwanamume anatoneshwa kidonda, hasa anapoitafakari hali ilivyokuwa hapo mwanzo. Anakumbuka, na vilevile, kumkumbusha Mwanamke jinsi walivyoyaponda maisha pamoja; 'akimpenda' naye 'akimpenda' bila ya kupimiana mapenzi. Kutokana na mapenzi hayo, Mwanamume anaomba warudiane tena. Huu ni umalenga wa huyu bwana ambao mwandishi amempa kulitimiza lengo lake moja alilolijia. Pwagu huyu anapatiwa pwaguzi na mwandishi - Mwanamke.

Mwanamke anaeleza upande wa pili wa 'kale' anayoisifia Mwanamume. Kale hiyo si buyu la asali kwa Mwanamke bali ni kumbukizi za makiwa na idhilali ambazo alizistahamilia kiasi kwamba zikamuotesha suguru moyoni. Kwake, hakuna tena penzi kati yake na huyu bwana anayejipambaniza na kudai kuwa walikuwa wakipendana. Mateso na shida, za miongoni mwa mengineyo, kuwa mufilisi kwa ajili ya penzi hilo la zamani, yanamfanya Mwanamke ajilaumu hasa anapofikiria jinsi alivyokuwa mtumwa wa mapenzi. Kwa sasa, bibi huyu amepata msisimko mpya unaoelezwa na kauli yake anaposema;

Mato unnifumbuwa, yawazi sasa yaona
Hali kaa ukijuwa, kwako huba sina tena
Mizizi nshaing'owa, hayawezi shikamana
Uwate kijisumbuwa, mi nawe tushatokana

Kumkumbusha siku za kisogoni kunampa fursa Mwanamke kulitoa dukuduku lake, ambalo kwa msomaji, ni jumla ya sababu ambazo zinatudokezea jinsi hali inavyozidi kuwa ngumu kwa Mwanamume. Alilokuwa akililia Mwanamume kama mapenzi kumbe lilikuwa zigo tupu la karaha na mateso kwa Mwanamke! Maoni ya kila upande hapa yanakuwa ufunuo unaomulika mitazamo yao kuhusu mgongano wao.

Mwanamume anajiona ameambuliwa na kubakia ganda tupu. Anakiri yote ya usafihi na udhalimu aliyotenda. Kwa ufupi, bwana huyu anadhihirika akiwa ametingwa na kutumbukiwa nyongo na kale aliyokuwa ameitegemea. Sababu badalia ni lazima zitafutwe angalau afaulu kumpiga milaza mfariji wake.

Maelezo juu ya masumbufu yaliyomsibu yanakuwa njia ya kuizima aibu na fedheha iliyoletwa na kukumbushwa ya zamani. Kwa kuueleza upeo wa uhitaji huo, Mwanamume anatarajia aangaliwe kwa jicho la huruma. Hoja zinakuwa kuukosa usingizi, kunyeshewa, na pia asikizwe kwani si haba umbali aliotoka kuja huku. Hizi hata hivyo, zinaonekana sababu za kijuu juu ambazo hazina mashiko kwa Mwanamke. Mwanamke amefanywa asimame dede kuukana uzandiki huu.

Maelezo, kama tulivyodokeza, ni sehemu muhimu inayoipa msukumo ploti, mbali na majukumu mengineyo ya uongozi, na hata kueleza kwa tafsili mandhari jukwaa. Kwa kuitumia kaida hii, mwandishi anatueleza mambo ambayo yametokea mwanzoni, kabla ya kukutana tena kwa wahusika hawa. Tunaelezewa matukio muhimu kabla ya kuanza kwa 'twaa' na 'twaa wewe' baina ya Mwanamke na Mwanamume. Matukio haya ni pamoja na kupumzika kwa Mwanamke ukumbini, kujirembesha kwake, kugongwa kwa dirisha lake la

chumbani hadi kwenda kulifungua na kustaajabia anayemwona gizani. Maelezo haya yanahitaji bongo chapuchapu kwa upande wa msomaji. Itambidi msomaji arejee nyuma na kuyapanga matukio haya ili aweze kuibuka na mtiririko halisi wa maigizo haya. Mpangilio huu unathibitisha maoni ya Forster (1924) kwamba kueleweka barabara kwa ploti kunahitaji kumbukumbu imara kwa upande wa msomaji. Kumbukumbu bora, bila shaka, itamfanya msomaji kuyaona maelezo ya kurasa za 103-5 yakiwa ufunuo wa maigizo haya. Msimulizi, katika kurasa hizi, anatoa maelezo yanayolengwa kuistawisha hali iliyopo kabla ya kuanza kwa maigizo yenyewe.

Tukio muhimu baada ya maelezo haya ni lile la kuelezwa kwa Mwanamume kuwa kulikuwepo na mwandani mwingine. Tukio hili lina umuhimu wa kumfanya Mwanamume kuimaizi nafasi yake kwa bibi huyu. Nafasi hiyo inafafanuliwa vyema na 'Maelezo' ambayo yanatumulikia hali aliyomo Mwanamume. Tukio hili linapewa sura ya kombora kwa jinsi bwana huyu alivyodundwa na moyo.

Baada ya donda hilo, msumari wa moto unafuata. Mwanamume anakomelewa tumbuu mbele yake. Kiploti, njia aliyoichagua Abdilatif ya kukwamishwa kwa Mwanamume inakuwa kilele cha maigizo haya. Ukweli lazima autafute na afahamu la kutenda baada ya janga hili. Mwanamume amefahamu ukweli wa mambo, sio kwa maneno ambayo wakati wote wamekuwa wakitupiana na Mwanamke, bali sasa kwa vitendo pia. Amejua kwamba nambari keshaipoteza na kamwe hahesabiwi kama mtu wa maana. Ameonyeshwa dhahiri kuwa hatakikani kwa kufungiwa dirisha machoni pake. Akasubiri pia akifikiria kuwa Mishi ataulegeza moyo. Yote ikawa ni kazi ya bure tu. Mishi keshaamua na wala si jambo la masihara. Ndipo Mwanamume anapofahamu kwamba kwake ni kule alikokuhama kabla ya

kuja kwa Mishi. Mwanamume anabaki akiijutia nafsi yake na kulia kwa jinsi ulimwengu unavyomtenda.

Katika kuuleta usawazisho baada ya Mwanamume kudhihirikiwa na ukweli wa mambo, Abdilatif anautumia 'Mnong'ono kwa msomaji'. Mnong'ono huu ni sehemu ya ploti inayojaribu kurekebisha tata zilizoibuka katika maigizo haya. Swali kuu linalozingatiwa ni, je, mfumo gani unaofaa kuzingatiwa baada ya 'kutendana' kwa wahusika hawa?

Kama tulivyoeleza, 'Mnong'ono kwa msomaji' umetumiwa kutoa tathmini ya Msimulizi juu ya mkosa na mkosewa kati ya wahusika hawa wawili. Katika kulitoa suluhisho la kuwasawazisha watendaji hawa, tunawekewa bayana udhaifu na haki inayomhimili kila mmoja baina ya Mwanamke na Mwanamume. Mnong'ono huu unamkaribisha msomaji kuajabikia ulezi aliojibandika Mwanamke, akifahamu barabara kuwa mume si wa kisheria. Mwanamume naye hakusalimishwa na msururu wa maswali yanayoinyooshea kidole hulka yake. Kaida hii inasaili iwapo lilikuwa jambo la busara, kwa Mwanamume kujiruhusu aengweengwe hadi kuwa mtundu, na kumtoroka Mwanamke pindi tu maisha yalipompa uso. Kwa kuwa huu ni msiba aliousababisha Mwanamke, Mnong'ono vilevile unasaili iwapo Mwanamke hakupitisha kiasi kutokana na kufumbuka kwake macho. Yote haya ni masuala ya kimjadala ambayo yanatarajiwa kutokeza pindi maswali yatakayotegemea uzito wa hoja hizi yatakapoulizwa.

Mrengo unaoyachukua maigizo haya, kama inavyodhihirika, hautoi kauli au tamko mahsusi katika kuutatua mgongano uliokuzwa na ploti hii. Kulingana na Mnong'ono, mgongano huu, kamwe hauwezi ukawa na suluhisho la moja kwa moja. Mtazamo unaochukua kaida hii (uk. 110) katika maisha unaelezwa na kauli kuwa;

Na ambavyo nawaona, watendaji hivi visa
Wantafautiyana, kwa kadiri ya makosa
Yuko aliyekazana, kidogo akayagusa
Wako walozidiyana, na alozidi kabisa

Kauli hii inaelekea kuliona suala zima la 'Kutendana', kama njia ya kimaisha isiyokuwa na suluhu yoyote. Kulipizana visasi ni jambo ambalo, hata iweje, litaendelea. Watu wote huwa na ari hii ya kutenda pindi wanapotendwa. Tofauti iliyopo ni ya viwango tu; kwamba kwa namna mtu anavyojiona anaweza kutenda, basi wapo ambao huweza wakauzidisha utendaji huo.

4.4.2. Ploti katika 'Mnazi: Vuta N'kuvute'

Ploti ya maigizo haya inaanza na kuimarishwa kwa hali ya mgongano kati ya ndugu wawili, Alii na Badi. Abdilatif ameuteuwa mnazi kuwa kifaa cha mgongano huo ambao kwao pande mbili hizi zitaonekana zikivutana. Wahusika hawa, kama kichwa chenyewe cha maigizo kinavyoashiria, wanavutana. Dhana hii ya mvutano inatiliwa nguvu zaidi na tofauti za kimahala; Badi akiwa juu, Alii akiwa chini ya mnazi huo unaogombaniwa.

Tukio kuu linalotumika kuipa msukumo ploti ni amri anayoitoa Alii kwa Badi; ashuke chini ili naye aukwee mnazi. Kwa mintarafu ya amri hii Badi, bila shaka, atapuuza na kujihami asitolewe tonge mdomoni. Mengi yanatokea kutokana na amri hii anayoitoa Alii. Anavyofahamu Badi ni kwamba yeye pekee ndiye mwenye haki ya kuumiliki mnazi. Ukaidi, hila na kila mbinu ya kidhalimu inatumiwa na Badi kuhakikisha kwamba mnazi umo katika mamlaka yake.

Dai la Alii linamfanya Badi aingie utetezini. Kwanza, anasingizia kuwa Alii ana kichaa na vilevile kujaribu kuukana ufungamano wa kinasaba anaopangiwa na Alii. Kuikatalia mbali

nasaba hiyo kungemwezesha kumzuia Alii kuukwea mnazi. Badi anazidisha ukaidi ili aihifadhi nafasi yake. Anamweleza Alii kuwa /... bado tavutana nawe/. Kauli hii, inaeleza umufilisi wa mawazo kwa upande wa Badi, ambaye anaukwepa ukweli wa kinasaba na badala yake kuurukia ushirika kama anavyouna yeye. B a d i anausana ushirika kujinufaisha. Kulingana na mhusika huyu, ushirika unamaanisha asiharakishwe kwani angeshuka wakati unaofaa.

Ushirika pia unatumiwa na mwandishi kufafanua masuala ya kiufunuo. Hapa tunatolewa maelezo yanayohusiana na mambo yaliyosababisha hali iliyopo. Maelezo hayo yanaturudisha siku za nyuma hadi kwa wazazi wa wahusika hawa. Kwa kuwa baba zao walikuwa ndugu, ushirika haukuwa wa mnazi kama kifaa tu, bali hata kidamu. Kwa hali na mali, Alii na Badi walihitajika kuwa washirika.

Ushirika halisi kama ulivyotendwa na wahusika hawa ulipitisha mipaka. Dhuluma ilijipenyeza huku tija ya mnazi ikielemea upande wa Badi. Badi alianza kumpunja mwenziwe kwa msingi wa umri wa baba zao, baba ya Alii akiwa mdogo. Mbali na umri, Badi alimtaka Alii aishi kwa kuitegemea kudura ya Mungu kuliko 'ulafi wake'. Hili lilimaanisha kutosheka na alichopata ingawa kichache. Alii, kwa upande wake, hakuweza kuyastahamili maonevu hayo; na hivyo basi, kuuvunja ushirika huo. Mateso na dhiki, hasa katika kuikirimu familia yake kwa chakula, mavazi na mahitaji mengineyo, yalimwandama. Tabu na dhiki hizo ndizo zilizomfanya ajitokeze kuidai haki yake.

Kwa jinsi pande mbili hizi zinavyovutana, hakuna mmoja kati ya wahusika hawa anayeafikiana na mwenziwe. Alii anakuwa wa

kwanza kuona kwamba Badi hangebanduka mnazini. Kwa kumfanya mhusika huyu kumaizi hali ilivyo, Abdilatif anaitayarisha hadhira kushuhudia kilele na, hatimaye, suluhisho la mgongano huu.

Alii anaamua kumwacha Badi hapo mnazini. Hatua ya kumkabili Badi ilikuwa ni kujuza tu kwamba mnazi si mali yake peke yake kama anavyofikiria Badi. Anachoahidi ni matumizi ya nguvu. Kauli hii anayoitoa Alii ni maoni ya maigizo haya yanayosisitiza majadiliano na maelewano ambayo yasipoleta fanaka, yanaafiki matumizi ya nguvu.

### 4.4.3. Ploti katika 'Usiniuwe'

Maigizo ya 'Usiniuwe', sawa na yale ya 'Mnazi: Vuta N'kuvute' na 'Kutendana', yanaanza na hali ya mgongano. Tofauti na maigizo ya 'Mnazi: Vuta N'kuvute' na 'Kutendana', ambayo yanadhihirisha kuwepo kwa wahusika wawili wanaoshiriki katika migongano hiyo, 'Usiniuwe' ni maigizo ambayo yanamdhihirisha mhusika mmoja. Mhusika huyu ni mtoto ambaye bado yumo tumboni mwa mamaake akiwa ni nofu la nyama. Wahusika wengine ni Mama, Uhai, Haki na Mauti. Wahusika hawa wanahisika kwenye jukwaa, ingawa hawatoi kauli zozote.

Tukio muhimu, ambalo linakuwa uzi unaoshikiliwa na ploti ya maigizo, ni uziraili anaojipa mama kwa mtoto huyu. Tukio hili linazigawanya njia za kufuatwa; Mama akielekea upande unaotofautiana na ule anaoenda Mtoto. Abdilatif amempa uhai mtoto huyu, akiwa bado yu tumboni mwa mamaake ambaye lengo lake ni kumtimua kiumbe huyo tumboni mwake. Mtoto, kwa upande wake, anaihami nafsi yake isitolewe uhai ilionao huku Mama, kwa kuihofu aibu na kuchekwa na jamii, anaiona afueni katika kumuavya mtoto

huyo.

Kupitia uzungumzi nafsia huu wa mtoto kwenye jukwaa, Abdilatif anachukua fursa ya kueleza, kwa tafsili, masuala mbalimbali ambayo kwayo kujibika kwake ndio msingi wa kupatikana kwa suluhu ya mimba haramu. Mtoto anarudi nyuma kimasafa na kueleza matukio ya kabla ya kujiri kwake. Kurudi kwake nyuma kunanuiwa kumfahamisha Mama kuwa ndiko kulikomhakikishia kuwepo kwake. Kwa ufupi, kurudi nyuma kiwakati ndio utetezi wake wa kuachwa aishi kwani, ni nyuma ambako Mama alikuwa amehiari aishi; jambo ambalo, kwa sasa, Mama halioni na mantiki.

Kwa kuyatathmini ya hapo nyuma, tunawekewa bayana ile mikutano ya faraghani aliyoihusudu Mama. Mikutano hiyo ilifuatilizwa na maneno matamu ya kimapenzi, hadi kufikia kitendo cha zinaa. Mtoto anaziona hatua zote hizi kama sahihi aliyoitia Mama, na kumhakikishia uhai wake. Kujiri kwake, anashauri, kusionekane kama suala la kimatokeo. Mama mwenyewe ndiye alihiari tangu mwanzo kuwepo kwake. Ni kutokana na kutuhumika vibaya kwa silika ya mamaake ambapo mtoto anathubutu kusema ;

> Huna haki kuniuwa, japo sijakamilika
> Huna haki kunitowa, kabla siku kufika
> Niwata nipate kuwa, mimi mwenyewe 'tatoka
> Mama wata kuniuwa, mamangu nihurumiya

Inavyodhihirika, Mama hapa anatishia kumwuuwa mtoto. Mtoto anaendelea kusihi, angalau aangaliwe kwa jicho la rehema.

Rai anazotoa zinalengwa kuitoa suluhu ya suala hili la mimba zisizotakikana. Badala ya kumpoka uhai, Mtoto anaona ni heri aachwe aishi hadi siku ya kuzaliwa kwake ambapo anahiari kutupwa njiani. Njiani anaamini atampata wa kumuauni na kumtimizia mahitaji yake ya kila siku. Akisha kua ataishi kama vile Mungu alivyomkadiria; awe mwizi au shetani, yote yatamwelea Mungu

mwenyewe.

Hata hivyo, suluhu hii inayotolewa na mtoto haiwi hatima ya maigizo. Katika maigizo haya, Mama hafanyi yale anayoyapendelea mtoto. Lengo lake bado ni lile lile la kumwuuwa mtoto huyu. Hili tunaliona waziwazi wakati mtoto anapolazimika kuomba msaada toka kwa watetezi wengineo wakiwemo Haki, Uhai na Mauti ambao anatumai watamkanya mama asimtishe na udhalimu wake.

Kinachojitokeza ni kwamba, tatizo hili la mimba haramu halina suluhisho la kiyakinifu. Ugaidi wa akina mama utaendelea kila mara hali kama hizi zitakapojiri. Kwa vyovyote vile, ploti hii inatusisitizia ukosefu wa matumaini kwa viumbe vinyonge ambavyo vitaendelea kudhalilishwa na kuangamizwa na wale wenye nguvu. Wanasiasa, kwa mfano, watazidi kuwakandamiza wafuasi wao. Badala ya kuwa tegemeo la wanaowaongoza, wanasiasa hawa watazidi kuyajali masilahi yao, bila ya kujali athari za ulafi na udhalimu wao kwa wananchi.

## 4.5. Kitendo

### 4.5.1. Kitendo katika 'Kutendana'

Kitendo katika maigizo haya kinajengwa na uhusiano wa kinyumba kati ya Mwanamke na Mwanamume. Uhusiano huu wa kinyumba, ambao umedumu kwa muda, hatimaye unayumba. Mwanamke, kutokana na visa alivyotendewa na Mwanamume, anaupiga moyo konde na kujiamulia kuwa hatatumiwa tena kama kifaa cha kuzituliza ashiki za Mwanamume huyo. Mwanamume hamaizi hatua aliyoichukua Mwanamke. Amerambishwa asali kwa muda hadi akauchonga mzinga. Kama ilivyo kawaida kwake kumwendea Mwanamke anaposhikwa na uchu, Mwanamume anarudi kutibiwa ndwele yake. Ugomvi huu wa kingono

ndio unaokuwa msingi wa maigizo haya. Mwanamume, kwa upande mmoja, analalamika apewe 'tiba' ya ugonjwa wake huku Mwanamke akiwa ameamua kuepukana naye.

Onyesho la maigizo haya linafunguliwa na kunoga kwa kitendo cha maigizo. Wahusika Mwanamke na Mwanamume, inavyoonekana katika majadiliano yao, wamekwisha tumbukia katika lindi la mzozano ambao umedumu kwa muda. Mwanamume anaanza kwa kusema;

> Kama bure utanipa, nipa sinisimbuliye
> Kama hutaki takopa, Nikulipe baadaye
> Hivi sasa cha kukupa, sina; kweli nikwambiye
> Mtu huwa hakutupa, amfaapo mwenziye

Kauli hii inatoa fununu kuwa ugomvi huu umekuwepo kabla ya kuanza rasmi kwa onyesho hili. Inavyojitokeza, Mwanamume amelalamika kwa muda, akitaka akidhiwe haja yake. Kauli hii ya kiufunguzi ni maendelezo ya rai anazotoa Mwanamume; 'apewe', ijapokuwa kwa mkopo. Kauli hii inazusha mjadala mpevu unaozusha nipa nikupe ya maneno kati ya wahusika hao. Ushirikiano, ingawa wa kihasama kati ya wahusika hao, unakuwa msingi wa kitendo cha maigizo. Mwanamke haridhi kutoa bure. Nyege ni kunyegezana na wala si maneno matupu. Kwa muda sasa, anadai, ndiye aliyekuwa akitoa bila ya kupewa chochote. Mwanamume naye anajaribu kumshawishi mwenzake akubaliane na matakwa yake.

Mwanamume anakumbwa na jukumu la kumshawishi Mwanamke. Ushawishi huo unajitokeza wakati mhusika huyu anapoeleza 'mwako' wa nafsi yake. Kati yake na maisha, ni kutimiziwa haja aliyoijia. Ndipo tunapomwona akianza kueleza usumbufu wa kunyeshewa na mvua na umbali wa kimasafa alioutembea. Kwa maoni yake, hii ni ithibati kuwa yu taabani, kwa jinsi alivyobanwa na ashiki. Haoni mwingine wa kumtibu ila huyu bibi.

Mwanamke halainishwi na papatiko la Mwanamume. Papatiko hilo

analiona kuwa ni chumbi ya vishawishi tu, ambavyo, kwake, si chochote ila hila tupu. Haoni jinsi atakavyomkidhia haja yake. Anamshauri Mwanamume arudi alikotoka: jambo linalomfanya Mwanamume atoe kauli kuwa hapendwi kwa sababu ya tamaa.

Dai kuwa tamaa ndiyo iliyomshika Mwanamke hadi akafikia uamuzi wa kumwacha Mwanamume, linamkasirisha Mwanamke. Kauli hii ndiyo inayotuingiza katika maana halisi ya kitendo cha 'Kutendana'. Mwanamke, katika majibizano yake, anatoa kauli ambazo zinauhalalisha msimamo wake wa kumtenda Mwanamume.

Mwanamke anaanza kwa kuusimulia ukarimu aliomfanyia Mwanamume. Pesa zote alizokuwa nazo wakati huo alizitumia kuyakirimu mahitaji ya huyo bwana. Bidii zake, anadai, zilimfanya Mwanamume kujibari na ukondefu na, mahali pake, kuchukuliwa na hali nzuri ya kiafya. Hayo yaliendelea hadi Mwanamume akatononoka mwili na kuwa mtanashati. Kuona hivyo, Mwanamume akaota mbawa na kumgura mwenziwe. Mwanamke akabaki hana pa kushika. Madeni yalimbana, na kwa jinsi madeni hayo yalivyomwandama, akawa hana jingine ila kuviweka rahani vitu vyake. Mwanamke anaona uchungu anapoyakumbuka yote haya.

Ni wazi kwamba, katika masutano haya, maneno pekee si kitendo kikuu kinachoashiria uchungu uliompata Mwanamke. Kaida ya Maelezo inaliziba pengo hilo kwa kutuelekeza kuona hali aliyomo Mwanamke wakati wa hekaheka hizi. Kaida hii inajaribu kutuletea, kwa ukaribu zaidi, picha ya Mwanamke ili tupate kuuhisi uchungu wake. Tunaposoma utungo huu, kaida hii inatuelekeza kumwona Mwanamke akiwa ameangaliana uso kwa uso na Mwanamume, akichezwa na mwili, huku uso wake ukiwa umesawajika kwa jinsi alivyopandwa na mori. Ukali huo unampanda zaidi

anapokumbuka mateso aliyoyapata alipokuwa akiishi na huyo bwana (uk. 96). Kila hatua katika maongezi yake ni hatua ya kuongezeka kwa ukali wake. Kitendo cha kuchezwa na mwili pamoja na kubadilika kwa rangi ya uso ni vitendo vyenye nguvu za kuashiria hasira za Mwanamke, kama vile cheche za maneno makali anayoyatoa zinavyofafanua uchungu huo. Kwa pamoja, mseto wa maneno na maungo ya Mwanamke yanatutolea picha kamili ya ghadhabu zilizomsakama. Fauka ya hayo, dhana ya kuangaliana uso kwa uso inatusisitizia kutoweka kwa uoga katika nafsi ya mhusika huyu akidiriki kumwangalia mwenziwe na kuwa tayari kumkabili kwa lolote.

Mwanamume, tunaelezwa kuwa yu kimya wakati Mwanamke anaposema kweli yake. Maelekezo haya yana lengo la kutuibulia fikra kuwa hii ni alama ya kushindwa au kuingiwa barabara na ukweli unaosemwa. Tunaelezwa kuwa Mwanamume hana la kusema isipokuwa kusakamwa na hasira tu. Kwetu sisi, hii ni kauli inayothibitisha msemo kuwa ukweli ni mchungu.

Mwanamume, tunaelezwa, anarudi matao ya chini, ikiwa ni mbinu ya kuupoza ukali wa Mwanamke. Anaanza kwa kulilaumu jicho lake ambalo, kila anapojaribu kulifumba, linakataa na kumwelekeza kwake. Usingizi pia anasema umempaa akabakia kuhesabu boriti na kugaagaa kitandani. Ndipo akaona ni bora akifuate kile alichojia ili aupoze moyo wake. Mbali na hayo, anamkumbusha Mwanamke mvua inayonyesha na kibaridi kinachoandamana na mvua hiyo. Vishawishi hivi ni miongoni mwa njama za Mwanamume kupata nafasi ya kujipenyeza nyumbani ili azidi kuendelea na vishawishi vingine. Vishawishi hivyo vinakutana na kicheko; ishara kuwa anayoyaongea Mwanamume hayampigi mshipa anayemshtakia hali yake.

Mwanamke anaelekea kuwa keshaumaizi ujanja wa Mwanamume. Anampa hongera kwa ustadi wake wa kuyapanga maneno na kumwombea fanaka mahali kwingineko. Mwanamume bado hajakata tamaa. Anaomba msamaha warudiane kama zamani, kauli inayomfanya Mwanamke kumshauri Mwanamume amuhesabu miongoni mwa wafu.

Mwanamume anabadilisha mbinu na kuanza kutoa ahadi za kufurahisha. Anaahidi kuwa fedha zote, kuanzia wakati huu, zitakuwa halali ya Mwanamke. Kwa Mwanamke, mapenzi si bidhaa ya kununuliwa kwa fedha kama anavyofikiria mwenzake. Pesa kwake ni mapenzi 'rahisi'. Bei ya mapenzi yake, kama anavyoeleza, ni ghali (uk. 102). Haoni lolote la kulipwa ambalo litafidia mateso yake. Kumtenda Mwanamume ndiyo njia pekee ya kujilipiza kutendwa alikotendwa na Mwanamume. Anatia migati na kuhakikisha kuwa anajilipa kwa kumyima bwana huyo penzi lake.

Wakati huu wote wanapoongea, Mwanamume yu nje ya nyumba akiomba afunguliwe mlango. Mvua nayo inanyesha, hivyo kumfanya Mwanamume alowe chapachapa. Hali hii tunatarajia iwe kisingizio atakachotumia Mwanamume, kuruhusiwa kuingia ndani. Hilo linajiri. Mwanamume anaomba afunguliwe mlango ajisitiri, hata ingawa amekataliwa ombi lake. Ombi hilo linakataliwa kabisa. Kukataliwa kwa rai hiyo ni jambo linaloeleweka. Pengine Mwanamume angepewa nafasi hiyo, angeendelea na porojo zake ambazo zimemchachukia Mwanamke. Uchu uliomkaba ungemfanya atumie mabavu ili aitulize hamu yake. Baada ya donda hilo, unafuata msumari wa moto. Bwana anaelezwa kuwa yupo mtu bora anayehimili penzi lake anayemsubiri.

Kwa watu waliozoeana, tamko kama hili lina uwezo wa kumfadhaisha mtu. Haiyumkiniki, ingawa inawezekana, kuwa mtu

ambaye kwa siku zote amekuwa akikufadhili kwa kila njia ghafla kuja kukugeukia na kukueleza kuwa amepata mwingine, tena bora kuliko wewe. Mwanamume anashtuka (uk. 107). Kupitia 'Maelezo', tunamwona akiweweseka na kujizuia asianguke, nusurani na kiguzo anachokiegemea. Kauli hii inakuwa usemi wa mwisho wa Mwanamke. Usemi huu unafuatwa na kufungwa kwa dirisha. Kitendo cha 'Kutendana' kinakamilika.

Mwanamume anakiona kitendo cha kufungwa kwa dirisha kuwa ni kumdhihaki. Anasimama nje, akitumai kuwa huenda Mwanamke akarudi na kumfungulia mlango. Hilo haliwi. Mwanamume, baada ya kutendwa, anajitenda mwenyewe. Anarudi alikotoka bila kuupata mradi wake. Kama vile alivyomtenda mwenzake, naye pia yamemkumba ya kutendwa. Hadhira inaachwa ikijisaili mkosa kati ya Mwanamume na Mwanamke; jambo ambalo linajadiliwa kwa kirefu na 'Mnong'ono kwa msomaji'.

4.5.2. Kitendo katika 'Mnazi: Vuta N'Kuvute'

Katika maigizo haya, tunawaona wahusika Alii na Badi wakiingia katika kinyang'anyiro cha kuumiliki mnazi. Mnazi ndio unaokuwa mhimili wa kitendo katika maigizo haya. Tunaweza tukakieleza kitendo cha maigizo haya kwa muhtasari kama 'Jitihada za wanyonge katika kupigania haki' au hata 'Vuta nikuvute kati ya wanyonge na wenye nguvu'. Kauli hizi za kijumumla zinaeleweka kwa kuiangalia nipa nikupe ya maneno kuhusiana na mnazi, baina ya Alii na Badi. Majadiliano kati ya wahusika hawa ndio msingi wa maigizo ya onyesho hili moja.

Onyesho hili linaanza na tofauti ya kimahali iliyopo; Alii akiwa chini, na Badi akiwa juu ya mnazi. Tofauti hii ya kimahali

inaonyesha kule kukosekana kwa hali ya usawa miongoni mwa wahusika katika jamii. Hali hii ya kutokuwa sawa kimahali inaonekana imekuwepo kwa muda mrefu. Wazo hili tunaweza tukaliona kupitia kwa Alii ambaye inaonekana amesihi, kwa muda sasa, apewe fursa ya kuukwea mnazi. Hali ya mgongano iliyopo inakuwa msukumo imara wa kitendo cha maigizo.

Badi, inavyodhihirika, hayuko tayari kushuka chini ya mnazi kama anavyoamuru Alii. Alii, akiwa chini ya mnazi, anaiona nafasi ya kuukwea mnazi ikiwa jambo la tunu kwani faida iliyomo haikadiriki. Badi naye, kwa upande wake, ameshafikia kilele cha fanaka na haoni cha kumteremsha mnazini. Mnazi huo, anavyodai, ni wake; na anamsingizia mwenzake kichaa. Tunahisi kuwa Badi anamghuri mwenzake kwani si jambo la kiyakinifu kwa mtu kudai kisichokuwa chake. Alii anaposhikilia apewe nafasi ya kuukwea mnazi, Badi anaomba ajulishwe sababu ya kushuka chini.

Kauli ya kutaka kujua sababu ya kushuka chini ndiyo inayotupatia nafasi kufahamu chanzo cha mgogoro uliopo kati ya wahusika hawa wawili. Mgogoro huo unaposimuliwa, unakifanya kitendo cha wakati uliopo kutegemea vitendo vilivyotokea hapo zamani. Kushuka au kubakia juu kwa Badi kunategemea yale yaliyotokea hapo zamani.

Kupangiana nasaba, na jinsi nasaba hiyo inavyoathiri masuala ya kiurithi, ndilo jambo la kwanza analolizingatia Alii. Mnazi, kulingana na Alii, ni wa shirika; ukiwa ni urithi walioachiwa na baba zao. Kwa kuwa wote ni wana halali wa baba hao, kila mtu alistahili kupata fungu sawa. Badi kusikia hivyo anagutushwa na ukweli uliosemwa. Ndipo anapojitafutia sababu za kudumu kwenye mnazi. Kwa maoni ya Badi, ukubwa wa kiumri kati ya babaake na

babaake Alii, ndicho kigezo kinachomfalia kuupimia urithi. Kwa kukumbusha kuwa babaake alikuwa mkubwa, Badi anafikiria namna ya kujinusuru ili azidi kukaa juu ya mnazi. Alii anatoa jawabu kuwa, ingawa babaake alikuwa mdogo, hiyo si sababu ya kumnyima fungu lake.

Jawabu hiyo inamfanya Badi kutafuta mbinu zaidi za kuyanusuru makazi yake. Anaitumia kauli ya ushirika kuhalalisha kukaa kwake juu. Anauliza sababu ya kuamriwa kushuka chini haraka iwezekanavyo iwapo mnazi ni wa shirika. Dai hili inapasa tulione kama njama ya kuung'ang'ania mnazi, kwani kuafikiana na ombi hilo kungemaanisha ushindi kwa Badi.

Badi anajaribu kuusawazisha na kuuhalalisha udhalimu wake. Anasingizia kuwa hali iliyomsibu Alii haitokani na kuwepo kwake juu ya mnazi, bali ni msiba aliojitakia. Anauona uhodari na weledi asiokuwa nao Alii ukiwa chanzo cha idhilali zake. Badi anaonyesha upofu wake kwa kudai kuwa ni Alii mwenyewe aliyekubali wachanganye mali zao kwa pamoja, wazo ambalo halikuchukua muda, kwani Alii 'alizua mengine'. Hivyo basi, Badi anashangaa kwa kusema;

> Ndipo kunipiga vita, nisivyojuwa mwanzowe
> Ulotafuta 'mepata, hasara ni kwako wewe
> Mpiga ngumi ukuta, huumiza mkonowe
> Wapigiyani mayowe?

Kulingana na Badi, kutengana na Alii lilikuwa jambo zuri kwani Alii, kwa mapenzi yake, alikataa kuchukua fungu lake. 'Mengine' hayo anayozungumzia Badi yanatufanya tusaili iwapo haendelezi mipango ile ile ya kutaka kubakia juu ya mnazi.

Alii anaeleza aina ya ushirika uliokuwepo kati yao, na sababu zilizomfanya asilichukue fungu lake. Anadai kuwa ni Badi, aliyeanza visa vya kumnyima fungu lake la sawa. Kwa Alii, nusu

shari ni sawa na shari kamili, kinyume na Badi ambaye anamshauri kwamba halikuwa jambo la busara kukataa kidogo alichompa. Kwa kukikataa kichache, Alii anaeleza kuwa lengo lake lilidhamiria kuondoa tashwishi yoyote kwa jamii na familia yake, kuwa alichopata hakukitumia kuitunzia familia yake. Kwa kuchelea lawama, Alii anaeleza msimamo wake wa kuhiari kutochukua kichache alichopewa.

Kwa kumsingizia ulafi mwenzake, Badi anajiweka peupe na kutambulikana kuwa anayosema Alii si ya uwongo. Badi haoni kuwa kumpunja mwenziwe ni kosa, kuliko kutoliridhia fungu dogo lisilotimia kiwango anachostahili mwenziwe. Kwa maoni yake, kukikataa kichache ndilo kosa kubwa alilotenda huku akikumbusha kuwa /Ni heri nusu shari, kuliko shari kamili/. Kwa kuwa Alii alikuwa keshakitapika alichokila, haikuwa vyema, kulingana na Badi, kuja kukiramba tena.

Rai za Alii kumtaka Badi ashuke bila nguvu zinafikia ukingoni. Ndipo Alii anapoahidi matumizi ya nguvu ili ajipatie haki yake. Kutangaziwa vita ni kitendo cha uwoga kwa Badi. Kwake, mpiganaji huwa hatangazi bali humuotea mvita wake. Alii ana msimamo tofauti. Hapendelei kunyemeleana katika vita. Onyo hili ni la kumtahadharisha Badi na siku ya vita ambavyo vitakuwa vya haki machoni mwa jamii.

### 4.5.3. Kitendo katika 'Usiniuwe'

Kitendo cha maigizo haya kinahusu rai za Mtoto, asiadhibiwe kifo kinachomkabili. Katika uzungumzi huu nafsia, Mtoto anaweka dhahiri ukatili wanaotendewa watoto wakiwa tumboni bado. Mama, Uhai, Haki na Mauti ni washiriki wa maigizo haya, ambao uzungumzi

huu nafsia unawalenga.

Watoto wanaopatikana nje ya ndoa, aghalabu, hawana hadhi katika jamii. Kwa wazazi wenyewe, watoto kama hawa ni chanzo cha kuvunjikiwa na heshima na kusababisha mfadhaiko wa nafsi. Wazazi, hususani mama ya mtoto kama huyo, huchelea kupatikana na aibu: wakiwa na lawama ya kushindwa kuzichunga hadhi zao. Uavyaji wa mimba huwa ndiyo njia pekee ya kudumisha hadhi zinapotokea mimba haramu. Mama wengi wanaojikuta wametupwa na wapenzi wao huufikia uamuzi huu wa kuziavya mimba. Hilo linapotokea maisha ya viumbe waliomo tumboni hupotea. Maisha ya watoto huwa yamo mikononi mwa mama zao.

Maigizo haya yameichukua hali hii inayomsibu mtoto akiwa bado yumo tumboni kama msingi wake. Katika tumbo la mama, tunamwona Mtoto akiutetea uhai wake usichukuliwe. Utetezi anaoutoa unasikilizwa na Mama, Uhai, Haki na Mauti, ambao wataamua, iwapo hoja wanazozisikia zitamnusuru na uamuzi wa Mama.

Katika kutoa utetezi wake, Mtoto anasihi asiuwawe kwa kuwa ni mamaake pamoja na huyo mpenzi wake waliopanga uzinifu uliomleta duniani. Yeye anadai hafahamu mahali, wala masaa ya mipango waliyoipanga hadi wakazini. Na hata walipobembelezana, Mtoto anasema hakujua maneno matamu waliyotupiana. Mbali na hilo, Mtoto anataka mamaake azilaumu hawaa zake zilizomshinda kuzuia hadi zikamfanya azini.

Mtoto anazidi kusihi apewe nafasi ya kukua ili awe kama wanadamu wengine. Anatoa muhtasari wa kukua, hadi ngazi aliyoifikia. Asili yake anaibainisha. Anataja kuwepo kwa tone la manii lililoanguka mahali pake maalum. Baadaye akawa pande la damu na kisha nofu la nyama; ngazi ya kukua ambayo ameifikia

kwa wakati huu wa maigizo. Ni nofu hili ambalo linalalamika kwa wakati huu. Anasihi aachwe hadi akamilike kiumbo.

Uhai, kulingana na Mtoto, ni halali yake. Mama akiwa mja kama yeye hana haki ya kuuchukua uhai wake. Fauka ya hayo, ni Mama huyo huyo, ambaye amemwacha tangu mwanzo hadi akawa nofu la nyama. Ndipo anapomwomba amwache hadi atakapotimia na kujitokea mwenyewe tumboni. Anashauri atupwe baada ya kuzaliwa, iwapo Mama ataiona haja ya kufanya hivyo. Njiani, anaamini atapata sitara kwa wanadamu watakaomwangalia kwa jicho la huruma. Duniani, ana imani, atatunzwa hadi afikie kiwango cha kujitunza mwenyewe kulingana na mipango ya dunia.

Mtoto, mbali na rai hizo, anastaajabu iwapo mama anahofu domo kaya la walimwengu wenzake kuhusiana na 'aibu' yake. Anaitilia shaka 'heshima' anayojaribu kuipata Mama, kwani anadhamiria kuitumia roho yake kama tambiko la kuipata heshima hiyo. Kauli hii inatuwekea wazi udhalimu wa Mama kwa kuitapia heshima kwa misingi batili. Anamtahadharisha mamaake na hatari ya kupatwa na jinamizi baada ya ukatili wake.

Mama, inavyoonekana, hapigwi na mshipa. Maombezi ya ghafla, toka kwa Mama hadi kwa Uhai, ni dhihirisho kuwa Mama yuko tayari kuichukua roho ya mtoto. Ukatili alioudhamiria Mama anautilia azma ya kuutekeleza. Kwa kupewa sifa za kibinadamu, Mtoto anausihi Uhai uingilie kati. Anauambia;

> Uhai! Nakuliliya, wewe ndiye upendwaye
> Uhai! Huna ubaya, yupi akutukiyaye?
> A! Uhai niombeya, mamaangu sema naye
> Pengine atasikiya, asiniuwe mamangu

Tunachoeleweshwa hapa ni kukata tamaa kunakomsibu mtoto. Kwa kuusihi uhai kuingilia kati, Mtoto anaamini huenda mamaake akakiacha kitendo alichokusudia.

Mbali na Uhai, kuna pia Haki na Mauti, ambao wanaitwa kuwa watetezi wa mtoto. Mahali alipo, yu taabani. Kuitwa kwa Haki, kama kiumbe atakayesema ukweli, na hatimaye nasaha kwa Mauti yasimkasirikie, ni vielelezo vya kutindikiwa na maisha anakokukabili Mtoto. Usaidizi anaoutarajia, kwa namna iwavyo, hautafanikiwa kwani Mama ndiye mwenye kauli ya mwisho ya kuusalimisha au kuukatisha uhai wa mtoto.

## 4.6. Wahusika

Kama tulivyodokeza katika sura ya tatu, wahusika katika maigizo huwa ni watendaji au watekelezaji wa mambo fulani. Daima dawamu, wahusika hawa hutaka kulitekeleza lengo ambalo liko nje ya himaya za nafsi zao. Hivyo basi, wahusika huingia mbioni wakazielekeza jitihada zao katika kuyatimiza malengo haya. Ni katika kuizingatia misingi hii, ambapo tunawazamia viumbe hawa wa kubuni katika maigizo haya. Tumejaribu kuchanganua mambo ambayo yanakuwa changamoto ya utendaji wao.

### 4.6.1. Wahusika katika 'Kutendana'

Maigizo haya yanatendwa na wahusika wawili wakuu, Mwanamke na Mwanamume. Uhusika wa wahusika hawa unajengwa kutokana na yale yaliyowahi kutokea baina yao. Mwanamume aliwahi kutenda zamu sasa ikiwa ni ya Mwanamke kutenda katika duru ya pili ya kukutana kwao.

#### 4.6.1.1. Mwanamke

Katika uumbaji wa wahusika wa kidrama, mhusika huyu ni

kielelezo cha ustadi wa Abdilatif katika kumdhihirishia msomaji au hadhira yake mhusika mwenye ushikamano. Umbo, lugha, mandhari na hata maleba ni sehemu ya mali ghafi ambayo mwandishi anaitumia kutudokezea mhusika huyu. Mwanamke ni mhusika halisi wa kidrama ambaye si vigumu kwa hadhira kumwona akiwa mtendaji wa maigizo haya ya 'Kutendana'. Uhusika wake ni tufe katika tufe la maana ya maigizo haya. Kila sifa inayomfafanua ni hatua ya kuielewa dhana ya 'Kutendana'. Vitendo, kauli na hata umbo la mhusika huyu ni nyenzo za kutugubulia maana ya maigizo haya.

Abdilatif analichukua jukumu la kutuwekea machoni mwetu mhusika huyu. Tunachoona ni dhana ya uzuri kwa mshairi huyu wa kijukwaa. Beti saba za 'maelezo' (uk. 103) zinatueleza uteuzi wa maleba ambayo yananuiwa kumpa uzuri wa kiupeo. Uzuri huo unaifanya kaida hii ieleze kuwa Mwanamke huyu /...Umwonapo utadhani, si mja ni malaika/. Tunauhisi uzuri wa mhusika huyu kutokana na vipochopocho anavyotumia kujirembeshea.

Tunatajiwa jumla ya manukato yakiwemo nyudi za Arabuni, piya alizoweka chetezoni, na asumini. Pia kuna vito vya thamani alivyojinakshia vikiwemo kidani alichofunga shingoni, kipini puani, vipuli, pete na bangili za dhahabu. Mbali na hayo, bibi huyu amejivalia leso mbili. Utanashati huu si wa vyombo pekee bali hata yeye mwenyewe amejinadhifisha kwa kujipaka liwa, kuzikata vyema nyushi na kuitengeza sikini.

'Maelezo' haya, yakiwa juhudi za kiuzingativu juu ya suala la maleba kwa wahusika, zinatusaidia kuikweleza dhana ya maigizo ya Abdilatif. Ufafanuzi huu unatuwekea machoni mwetu Mwanamke aliyekamilika. Kuonekana kwake ni tukio halisi la kidrama. Sifa mbalimbali alizolimbikiwa mhusika, si mapambo kwa ajili ya

kuitamanisha hadhira tu, bali lengo lake kuu litajitokeza kwa kuizingatia athari inayonuiwa na taaluma hii ya maleba kwa maigizo yenyewe. Uteuzi huu wa kimaleba unanuiwa kumtamanisha na kumpa kiwewe Mwanamume ambaye, kwa sasa, amebanwa na uchu. Mbali na kumtamanisha, maleba yaliyotumika yanamsimanga Mwanamume; kuwa si mlezi, kama wanaume wanavyohitajika kuwa. Uzuri huu unalengwa kumtia mtegoni. Haya yanadokezwa na 'Maelezo' kwamba si Mwanamume pekee ambaye angeathirika bali pia

...Mpita hiyo twariki, angataka kujipinda
Moyo utataharaki, uwe ni mbiyo kumwenda
Na bila shaka ashiki, zitazidi kumpanda

Kwa wale wanaofahamu na kuibukiwa na picha halisi ya mapambo haya yaliyokuwa sehemu ya Mwanamke, uzuri wake bila shaka utakuwa ule uliokithiri. Hadhira, kwa kutajiwa mapambo hayo tu, inathibitikiwa na uzuri unaovutia ambao kaida ya 'maelezo' imejaribu kuutolea uchanganuzi.

Kutokana na mapambo hayo, mbabaiko unaompata Mwanamume unaweza ukatabirika. Mwanamke anakuwa mtego madhubuti kwa jinsi anavyoivuta na kuuathiri moyo wa madhulumu wake. Mwanamke, kwa kuzingatia tu urembo wake, ni kauli thabiti katika dira nzima ya suala la 'Kutendana'. Tayari Mwanamume anatendwa na umbo la Mwanamke huku kauli zake na vitendo vikiwa na yake ya kutuelezea.

Wahusika wa kidrama huwa ni watendaji wa sehemu zao ambazo waumbaji wao huwapa. Mwanamke, mbali na kuwa mtendaji anajifahamu kwamba yeye ni mchezaji wa nafasi aliyopewa. Mwanamke anatudokezea nafasi yake kwenye maigizo haya anapouliza;

Wajuwa yake maani, ya la wema kutendana ?
Naapa n'na yakini, huyajuwi; hungenena
Lau ungeyabaini, vilivyo haya maana
Wallahi hungetamani, uso wako kwonekana

Usemi huu unafuatiliziwa na ushuhuda wa mema mbalimbali

aliyomfanyia Mwanamume hapo awali kabla ya bwana huyo kumuasi. Kwa sasa, penzi hilo, mahali pake pamechukuliwa na chuki na uhasama kati yao. Mwanamke, kwa kulipwa mabaya badala ya wema wake, hivi sasa naye ananuia kujilipizia kisasi. Utendaji wake hivi sasa si wa wema tena.

Chuki na mori alionao unatuelekeza kumwona mhusika huyu akitenda, si kwa maneno tu bali hata kwa vitendo. Kila analofanya linatumulikia ari yake ya kutenda kama alivyotendwa. Tayari mapambo yake tumeyaona yakimwadhibu Mwanamume. Ari hii ya 'kumtenda' mwenziwe inaashiria na vilevile kuwa nyongeza ya kumuambua Mwanamume kiasi cha kumbakisha ganda tupu. Katika kiwango cha chini zaidi, tunaiona lugha ya Mwanamume ikibiruliwa na kuwa kitanzi cha kujinyongea mwenyewe. Mchezo wao wa maneno unatoa mfano mwafaka wa jinsi Mwanamume anavyobainishwa kama malenga guni wa maneno yake mwenyewe. 'Sina', 'pepo', 'dawa' na 'n'natoka nitokako' za Mwanamume zinabiruliwa na kumchachukia zinapotiwa kinywani na huyu bibi. 'Sina' yake anapigiwa kijembe nayo kwa kutahadharishwa kuwa 'nyege ni kunyegezana'; kuwa 'sina' yake haifai kitu kwani muda wote ni yeye tu aliyefaidi bila ya kuonyesha kuwajibika kwake. Kadhalika ni masuala ya 'dawa' na 'pepo' ambayo kwayo anaelezwa kinaganaga kuwa hangepewa 'dawa', aula afe kwa maradhi. Vilevile, Mwanamke anamshauri Mwanamume ampeleke 'pepo' wake kilingeni kwani hayuko tayari kumpunga 'pepo' duni. Aidha upo msisitizo wa /Rudi kuko utokako.../ kama jawabu ya Mwanamke kwa Mwanamume anapoeleza /Nnatoka nitokako.../. Jawabu hizi zinaeleza ugumu wa Mwanamke katika kuilegeza azma na lengo lake la kumtenda Mwanamume.

Ufanisi wa Mwanamke, kama mtendaji wa 'Kutendana',

unatokana pia na weledi na uzito wa kumbukumbu dhidi ya Mwanamume. Kutokana na kumbukumbu yake pevu, Mwanamke anajitokeza kama pwaguzi: mkabala na Mwanamume ambaye haelekei kufahamu barabara yaliyotokea hapo awali. La kustaajabisha ni vile Mwanamume anavyokuwa na yakini na kuiimba kale kama jambo tunu kwake akidai kwamba mapenzi yake yalikuwa yamenoga. Bila ya kusita, Mwanamke anaiweka bayana hali iliyokuwepo ya idhilali na mateso aliyopatishwa. Hatima ya ushuhuda wa tajriba ya penzi hilo inamwacha Mwanamume kukiri yote aliyotenda. Anasema (uk. 97),

Vyema n'nayasikia, yote uliyoyanena
Orodha 'menipangiya, ya mambo kila namna
Yote 'menihisabiya, ulobakisha hakuna
Ni kweli 'menifanyiya, moja siwezi likana

Kukubali huku kunamfanya Mwanamume aonekane mtu dhalimu na katili anayestahili kutendwa. Mbali na kuwa ushuhuda wa mateso na mikasa iliyomsibu huyu bibi, Mwanamke pia anakuwa kioo cha kuionea silika ya Mwanamume.

Tajriba ya kuishi na Mwanamume imemwelewesha Mwanamke hila za huyu bwana. Ufahamu na umalenga wa Mwanamume katika kuhadaa unabainiwa kirahisi na Mwanamke. Msamaha bandia anaoumba na visababu vya uwongo unatambuliwa, na hivyo basi, kumkatisha tamaa Mwanamume. Visingizio vya kuukosa usingizi, hadi akafikia kuzihesabu boriti, kuja kwake na hata kuisingizia mvua kama sababu kamili ya kuachwa aingie ndani, yanatiliwa pamba masikioni. Bibi (uk. 100) ametia migati na kujibu kwa imara;

Licha maneno matamu, ambayo waniambiya
Hata matozi ya damu, lau hayo utaliya
Hayawezi n'lazimu, wewe kukuhurumiya
Uombe wako ugumu upate kukusaidiya

Penzi kwa Mwanamke limeisha. Radhi anayoomba Mwanamume inapuuzwa

unatokana pia na weledi na uzito wa kumbukumbu dhidi ya Mwanamume. Kutokana na kumbukumbu yake pevu, Mwanamke anajitokeza kama pwaguzi: mkabala na Mwanamume ambaye haelekei kufahamu barabara yaliyotokea hapo awali. La kustaajabisha ni vile Mwanamume anavyokuwa na yakini na kuiimba kale kama jambo tunu kwake akidai kwamba mapenzi yake yalikuwa yamenoga. Bila ya kusita, Mwanamke anaiweka bayana hali iliyokuwepo ya idhilali na mateso aliyopatishwa. Hatima ya ushuhuda wa tajriba ya penzi hilo inamwacha Mwanamume kukiri yote aliyotenda. Anasema (uk. 97),

> Vyema n'nayasikia, yote uliyoyanena
> Orodha 'menipangiya, ya mambo kila namna
> Yote 'menihisabiya, ulobakisha hakuna
> Ni kweli 'menifanyiya, moja siwezi likana

Kukubali huku kunamfanya Mwanamume aonekane mtu dhalimu na katili anayestahili kutendwa. Mbali na kuwa ushuhuda wa mateso na mikasa iliyomsibu huyu bibi, Mwanamke pia anakuwa kioo cha kuionea silika ya Mwanamume.

Tajriba ya kuishi na Mwanamume imemwelewesha Mwanamke hila za huyu bwana. Ufahamu na umalenga wa Mwanamume katika kuhadaa unabainiwa kirahisi na Mwanamke. Msamaha bandia anaoumba na visababu vya uwongo unatambuliwa, na hivyo basi, kumkatisha tamaa Mwanamume. Visingizio vya kuukosa usingizi, hadi akafikia kuzihesabu boriti, kuja kwake na hata kuisingizia mvua kama sababu kamili ya kuachwa aingie ndani, yanatiliwa pamba masikioni. Bibi (uk. 100) ametia migati na kujibu kwa imara;

> Licha maneno matamu, ambayo waniambiya
> Hata matozi ya damu, lau hayo utaliya
> Hayawezi n'lazimu, wewe kukuhurumiya
> Uombe wako ugumu upate kukusaidiya

Penzi kwa Mwanamke limeisha. Radhi anayoomba Mwanamume inapuuzwa

na badala yake kuaswa;

Sasa nihisabu kwamba, n'shakufa kwako wewe
Na kaburi ukatimba, nimo ndani nifukiwe
Siwe na haja kuomba, kurudiyana mi nawe
Kama waweza kuumba, umba mimi mwingine

Rai hii kuwa Mwanamume aumbe Mwanamke mwingine ni kizingiti thabiti anachowekewa kama njia ya kuukatisha uhusiano wowote anaoufikiria bongoni mwake.

Msimamo huu hauna masihara. Kuepukana na huyu bwana ndilo lengo kuu lililomkaba kooni. Kwa kuumaizi ukaidi wa Mwanamume, bibi huyu anamjulisha kuwepo kwa mume mwingine anayestahili penzi lake. Kauli hii, hata ikiwa ni ya kujibandika, inatosheleza kuufanikisha uchawi wake. Isitoshe, urembo wa Mwanamke ni ushuhuda tosha kwamba amempata wa kumtunza. Nafasi aliyowahi kupewa Mwanamume ilimshinda, hadi alipotokeza mwenzake aliyeweza kumtunza mke. 'Maelezo' (uk. 107) yanatueleza kushtuka kwa huyu bwana akiwa amefahamishwa jinsi wakati unavyoweza kuzaa yasiyotarajiwa. Nafasi aliyoichezea ilikuwa imemdondoka mikononi mwake. Licha ya hilo, yanatokea yale ya kufungiwa dirisha, na hatimaye kukomelewa kwa tumbuu machoni mwake. Kwa kufanya hivyo, Mwanamke anaikamilisha nafasi yake ya kuwa nguli wa kutenda katika maigizo haya ya 'Kutendana'.

4.6.1.2. Mwanamume

Mhusika huyu anaicheza nafasi ya mhusika hasidi. Sifa kuu inayomwezesha kuicheza sehemu hiyo ni uchu uliokithiri ambao mtunzi amempachika. Kwa kumpa sifa hii, Abdilatif anamfanya mhusika huyu awe mfungwa wa uchu wake. Mkabala wa uchu huu ni Mwanamke ambaye amewahi kuishi naye, akimtimizia kila alilolitaka hapo awali. Anapojitokeza nje ya dirisha la Mwanamke, mhusika

huyu ana yakini kwamba uchu wake utajibari naye kwani mengi wameshafanya bila pingamizi. Hoja zake hizi zinamfanya ajitokeze baada ya siku nyingi kupita; isitoshe, tena usiku. Msingi wa kutendwa kwake unajengwa kutokana na mambo hayo.

Uhitaji wa Mwanamume, kinyume na matarajio yake, unamgeuza kuwa 'ombaomba'. Cheche za masimbulio, masuto na kebehi hazina uzito wowote kwake isipokuwa lile alilolijia. Uchu wake tunauona ukishinda matumizi ya ubongo wake na hivyo basi, kumfanya kerekecha asiyekuwa na hoja thabiti za kukidhiwa haja yake. Hali hii ya Mwanamume na nafasi yake katika maigizo inaelezwa vizuri, na 'Maelezo' yanayotudokolea kuwa;

> Una mambo ukosefu, ukitokusubiriwa
> Hupa mtu kuwa pofu, kadhalika zuzu kuwa
> Akajiona yu dufu, hafai kuthaminiwa
> Akawa mtu dhaifu, hajiwezi 'ngaonewa

Ukosefu unaotajwa si mwingine isipokuwa uchu wake. Uchu huu unamfanya achanganyikiwe kiasi cha kutotafakari yale anayoyasema.

Tunayemwona ni mhusika aliyedumaa kutokana na kutomaizi kuwa nyakati huenda na kubadilika. Bila ya kutafakari, tunamwona Mwanamume akiabiri kwenda kwa Mwanamke, kwa kuyategemea mazoea. Mazoea hayo, kila alipoyafikiri, anajiona akinyimwa haki yake ya kupenda. Wazo kwamba aliwahi kuishi kinyumba na Mwanamke analiona kama sababu tosha ya kumwendea ili kuzitoa ashiki zake. Isitoshe, huu ni muda ambao /...Nyezi nyingi zimesiya, tangu walipokutana/ (uk. 104). Muda huu haoni ukiwa na nafasi yoyote katika 'penzi lake' kama anavyodokeza;

> Amma um'badilika, hu tena kama zamani
> Waniona nadhikika, hutaki kuniauni
> Mwenziyo nataabika, hunionei imani ?
> Hafanyi hafarijika, hatowa pepo kitwani ?

Kwa mtu mwenye akili timilivu, tafakuri ya yale ambayo yangemsibu

ingemzuia kwenda huko hasa baada ya kujipoteza kwa miezi mingi. Mwanamume, hata hivyo, haoni kwamba kujipoteza kwake ni hatia tosha ya kunyimwa mradi wake.

Kutoikubali na kujikakamua kuishi leo yake ni jambo gumu kwa mhusika huyu. Bado tunamwona Mwanamume akiishi jana yake. Haishangazi kumwona akikumbusha ya zamani anaposema;

Nyuma ungeangaliya, toka twalipoanza
'Ngekumbuka mazoweya, na wema tulotendana
Ungejuwa ni vibaya, kunifanyiya khiyana
Mwenzako nihurumiya, si vizuri kutesana

Mawazo haya anayaeleza akisahau kwamba nyakati hizo zilikuwa za kijahili. Inabidi akumbushwe kwamba 'penzi' analozungumzia lilikuwa likimfaidi yeye tu na wala si la kuegesheana mapenzi kama anavyodai.

Badala ya kulitatua suala la kujileta huku, sababu guni ndizo zinazotolewa na Mwanamume. Kuukosa usingizi hadi kufikia kuhesabu boriti, kujileta kwake muda uliopita saa tano na mvua inayomyeshea anaziona sababu zenye uzito zinazoweza kuyafuta madhambi yake. Sababu hizi, kama inavyoonekana, hazimfaidi lolote bali zinazidi kumdidimiza na kumtamausha na ombi lake. Kwa upuuzi huu, Mwanamke anazidi kupata fursa ya kumtenda.

### 4.6.2. Wahusika katika 'Mnazi Vuta N'kuvute'

Maigizo haya yanamilikiwa na ndugu wawili, Alii na Badi. Uhusika wao unachukua umbo lake kutokana na vuta nikuvute iliyopo kati yao. Vuta nikuvute hiyo ni zao la urithi wa mnazi, mmea ambao wahusika hawa waliachiwa na baba zao, baada ya wazazi hao kufa. Masuala ya urithi yanazua nuksani kutokana na kufa kwa wazee hao. Alii ghafla anajikuta ametolewa shirikani na ndugu yake. Badi naye, kwa makusudi au kwa kutofahamu kilio cha Alii,

anang'ang'ania kuumiliki mnazi pekee. Maono tofauti na yanayokinzana kati ya ndugu hawa ni mikabala miwili tofauti ambayo kila mmoja kati yayo inajiona katika haki.

Utendaji wa wahusika hawa, vilevile, unaathiriwa na mitazamo yao kuhusiana na urithi wa mnazi. Alii na Badi, wakiwa watendaji wa sehemu zao, wanazama katika lindi la kuikimu mitazamo hiyo ambayo iko nje ya nafsi zao. Kulingana na Alii, lengo kubwa ni kulipata fungu lake la sawa. Badi naye, kwa upande wake, anapigania kukinusuru kitumbua chake ambacho, kwa sasa, kinaelekea kutiwa mchanga. Kila mmoja anaazimia kulifikia lengo lake.

<u>4.6.2.1. Alii</u>

Alii, kama tulivyotaja, anaazimia kulipata fungu lake la mnazi analostahili. Nafsi yake inakereka na upungufu huu ambao unamfanya ajitokeze ili alizibe pengo hilo. Katika maigizo haya, uhusika wa Alii unasheheni kauli ambazo zinalengwa katika kulifikia lengo hili.

Maigizo haya yanapoanza, tayari tunaziona purukushani za mhusika huyu kulifikia lengo lake. Stahamala zimejibari naye na anamsaili Badi iwapo angeshuka chini ya mnazi au la. Yeye, kama vile Badi, anaona ana haki ya kuzitunda nazi. Hili linamfanya Badi amsingizie Alii kichaa.

Kisingizio cha kichaa hakimzuii Alii kuendelea kudai kilicho chake. Katika kudhihirisha kuwa yu timamu, Alii anatoa jawabu ambayo ni msingi wa dai lake la kuukwea mnazi: uhusiano wa kinasaba. Uhusiano huo unawajumuisha baba yake na yule wa Badi. Kutokana na kupangwa kwa nasaba hiyo unganishi, Alii hapa

anajaribu kuonyesha kuwa yeye pia ana haki kamilifu ya kuukwea mnazi, aaangue nazi anazozipenda.

Nasaba hiyo inamtua Badi vyema kichwani. Hata hivyo, Badi anakuwa mwepesi wa kuvumbua hila nyingine ya kutaka kufahamu nani kati ya baba zao ambaye alikuwa mkubwa. Hili anauliza akifahamu fika kuwa babaake ni mkubwa. Badi analitumia swali hili kama fimbo, akitarajia kwamba ukubwa wa babaake utamfunga kauli Alii ya kumhimiza kushuka chini ya mnazi. Hilo haliwi. Badala yake, Alii anaendeleza mapambano na kudhihirisha ukomavu wa bongo lake katika kuilumbia haki yake.

Alii amesakamwa na shida. Shida hizo zinamfanya kuwa mhitaji. Jambo hilo halifichi kwa Badi na anamhimiza afanye hima kushuka mnazini angalau naye aangue nazi. Kwa kuziangua nazi, Alii anaeleza kuwa angeziuza nazi hizo ili zimwezeshe kuinunulia familia yake chakula na mavazi. Kauli hizi hazielekezewi Badi pekee. Hadhira pia inaelewеshwa kwa namna fulani jinsi Alii alivyobanwa na uhitaji. Picha hiyo tunayozalishiwa ina lengo la kutufanya tuutafakari kwa undani uhitaji huo.

Ushirika katika kuumiliki mnazi ni jambo la sahau kwa Alii. Badi anaona kuwa Alii ni wa kulaumika kwa kuukataa ushirika uliokuwepo baina yao. Badi analaumu kuwa ni Alii ambaye waliafikiana kuchanganya urithi wao na kugawana kipato hadi mwenziwe alipomuasi. Hata hivyo, Alii ana maoni tofauti yanayoeleza uasi wake wa ushirika huo. Ni ushirika huo ambao ulikuwa kitanzi, Badi alichompa amnyongee. Alii anadai alijikuta akipokea fungu dogo. Kupunjwa huku kwa kilicho chake kulimghasi moyo kwa jinsi shida zilivyomuandama. Baada ya maafa sufufu, Alii aliona heri ajitenge.

Kwa namna iwavyo, Alii anajitokeza kama mhusika anayeelewa vituko vya Badi. Sababu anazotoa kuhusiana na kujitoa kwake shirikani ni za kuridhisha. Alii aliifikiria familia yake, na domo kaya ambalo lingemsibu, kwa kudhaniwa visivyo. Anahofu, miongoni mwa mengineyo, lakabu ya ubahili asiokuwa nao. Uthabiti wa hatua yake ya kujitenga bado anaushikilia tu na kuamini kuwa ilikuwa hatua mwafaka. Alihiari kuonekana mtu dhaifu na anayedhulumiwa isipokuwa kwa wakati huu ambapo amejitokeza bila hofu.

Kwa wakati huu, Alii anasimama imara kuidai haki yake. Majadiliano yanayonuiwa kuleta uelewano kati yake na Badi yanafikia ukingoni. Njia nyingine ni lazima itumike. Alii anaiona imani ikipatikana kwa ncha ya upanga. Alii anasema;

> Kwa kuwa ni haki yangu, sitahayari kudai
> 'Tatumiya nguvu zangu, madhali ningali hai
> Nilipate fungu langu, japo kwa ya ghali bei
> Nawe hapo uwe hoi

Matumizi ya nguvu, anayaona yakiwa jawabu pekee ya kukabiliana na kani ya Badi. Kauli hii ya Alii inatuonyesha jinsi mhusika huyu alivyofumwa na ari ya kuipata haki yake. Kiwango alichofikia si cha masihara tena. Kwamba wanawe tayari walikuwa wameshazichukua fimbo zao kumkabili Badi ni ishara kwamba hakustahili kuonekana kama 'mbobokwaji' kama anavyodai Badi.

Mhusika huyu anajitokeza kama mtu mwenye busara na aliyepevuka kifikra kwa kuichukua hatua ya kumuonya Badi na hatima mbaya ambayo ingemsibu. Kuueleza undani wake, anaona kama wajibu wake, ili kuepukana na 'kuoteana ja kifaranga na mwewe'. Anaahidi kuvumilia udhalimu wa Badi lakini anatahadharisha kuwa ipo siku ambayo hatua atakayoichukua itaonekana si ya kimaonevu.

4.6.2.2. Badi

Mhusika huyu, kama tulivyotaja hapo juu, ni mtetezi wa hali ya uonevu iliyopo. Nafasi yake katika maigizo haya ni kuumiliki urithi wa mnazi kwa hila. Ung'ang'aniaji huo unatuthibitikia, hasa kwa kuzingatia uhusika wake mkabala na ule wa Alii. Matumizi ya hila mbalimbali kwa minajili ya kujihifadhia mnazi ni suala kuu linalomfafanua Badi.

Ufunuo wa uhusika wa Badi unatolewa na mahali alipo mhusika huyu. Kama anavyofahamisha Alii /Ndugu ulo mnazini.../, na kujibiwa /Ndugu tini ya mnazi.../, tunafahamu kuwa Badi ametamakani juu ya mnazi. Tofauti hii ya kimahala, na faida yake, ndiyo inayomfanya Badi kukatalia mbali kushukishwa mnazini. Amri hii kwake ni tishio la maslahi yake ambayo yamo hatarini. Kushukishwa mnazini kungemaanisha kukatizwa kwa kipato chake.

Mnazi, ilivyodhihirika, si mali ya Badi pekee. Pamoja na Alii, mnazi huu waliachiwa na baba zao. Kutokana na kutoelewana kwao na Alii, Badi ikawa anaumiliki na kuufaidi mnazi pekee. Tamu hii imemlewesha. Hivyo basi, haishangazi kumwona Badi akimdaia Alii kichaa.

Utetezi wa Badi unaashiria jinsi wenye navyo huwadhulumu wanyonge. Kichaa anachobandikwa Alii ni miongoni mwa hila za kina Badi za kutaka kujinyakulia hata vile wasivyokuwa na haki ya kuvimiliki. Hutokea pia cheche za matusi makali yakatumiwa ili akina Alii wafyate ndimi zao wanapozidai haki zao. Badi anapoulizwa tangu lini mnazi ukawa wake anajibu;

Wabobojekwa maneno, yasokuwa na maana
Ni ya kipumbavu mno, hayo uliyoyanena
Iwapo mnazi huno, si wangu; mbwa nani bwana
Sema nijuwe bayana

Matusi haya anayatamka Badi akiwa na imani kwamba yangemshitua

Alii na kumfanya ajiondokee. Vitisho hivyo havimyumbishi Alii ambaye anaeleza kwa tafsili jinsi mnazi huo unavyomshirikisha hata yeye. Badi anapangiwa nasaba na jinsi nasaba hiyo inavyomhusisha na urithi huo wa mnazi. Maelezo hayo yanamfanya Badi kuzitafuta mbinu nyinginezo za kilaghai.

Badi anaibuka na suala la umri wa wazazi wao kama kigezo muhimu kinachompa haki zaidi ya kuurithi mnazi. Kwa kuwa babaake yeye Badi alikuwa mkubwa, Alii alistahili kuambulia patupu. Kauli hizi zinapingana na maelezo yake ya hapo awali; zikionyesha kwamba mhusika huyu, kwa makusudi au kwa kutofahamu, ana lengo la kumdhulumu Alii. Maswali ya Alii yanamwingiza mtegoni kwani ni 'mbobojekwaji' huyo huyo ambaye anaafikiana naye kwamba urithi wa mnazi uliachwa na baba zao.

Ujahili na udhalimu umeganda kwenye nafsi ya Badi. Ari ya kudhulumu inamchemka na anamtangazia Alii waziwazi, kwamba /...bado tavutana nawe/ ingawa urithi huo waliachiwa na wazazi wao. Ukweli umemthibitikia Badi ambaye amefilisika kimawazo. Umufilisi huu wa mawazo ni sababu tosha ya kumfanya akubali kushuka mnazini. Hilo haliwi. Dhana ya ushirika anaiona ikimpa nafasi ya kudumu mnazini. Anasaili;

Nataka kukuuliza, suala nyingine kaka
Hivi punde 'men'eleza, mnazi ni wa shirika
Kwa nini kunihimiza, upesi nipate shuka
Na hali ni wa shirika?

Badi anauona ushirika katika misingi ya kumnufaisha yeye mwenyewe tu. Haoni kwamba mwenzake, ambaye muda wote amekuwa chini ya mnazi, ndiye anayestahili zaidi kupewa fursa ya kujiruzuku na nazi.

Badi, ambaye wakati wote alikuwa hajafahamu sababu ya kushukishwa chini, ndiye anayetufahamisha kuwa yeye pamoja na

Alii waliwahi kushirikiana hadi Alii 'alipoyazua mengine'. Kukubali huku kunatufanya tumtilie shaka zaidi Badi ambaye muda mchache uliopita amekuwa akielekea kuukana ushirika wa aina yoyote kati yake na ndugu yake. 'Mengine' hayo anayoyazungumzia Badi hayatolewi maelezo yoyote. Ni Alii anayeyamulika 'mengine' hayo ambayo kumbe ni ya unyonyaji aliyotaka kuyaendeleza Badi. Ushirika huo ulikuwepo hadi Badi alipousumu. Badi anashtumiwa kwa kosa la kumpunja mwenziwe kama chanzo cha kuvunjika kwa ushirika wao. Shutuma hii inaaminika kwani Badi ametumia kigezo cha ukubwa wa babaake kuhalalishia unyakuzi wake.

Badi bado ana yale yale ya kuvutana. Kumpunja Alii kwake si kosa kubwa na badala yake anataka Alii ajilaumu kwa kutotosheka na kichache alichokuwa akimpa. Kwa kuwa Alii alikuwa ameamua kujitoa shirikani, kurudi kwake ni jambo la kijinga kwa Badi. Yeye haoni jinsi atakavyomruhusu tena Alii kuambulia chochote kwani yeye keshashika na aliyeshika ndiye mwenyewe. Haya ni mawazo ya watu wengi wenye nafasi katika jamii ambao hujishughulisha na kujilimbikizia mali na kuwapoka haki zao wanyonge. Tumeona, kwa mfano, jinsi baadhi ya wapiganiaji uhuru walivyotengwa na kusahaulika kabisa. Mashujaa hao ambao aghalabu hawakupata nafasi za uongozi katika serikali walisahaulika kwa kuwa walioshika hatamu za uongozi walikuwa wenyewe zaidi na wengine waliokuwa maamuma wakabakia 'mazuzu'.

Mnazini ni pahala pa cheo na shibe kwa walio juu. Hawa ni pamoja na kina Badi ambao, kutokana na shibe hiyo, huwa hawajali sana yale yanayosemwa na walio chini. Hii ndiyo hali inayosawiriwa na mhusika huyu katika majibizano yake na Alii. Alii amenuna kutokana na kunyanyaswa kwa muda mrefu. Ghamidha

na kariha yake imemleta kuja kuitoa shauku yake, hasa lile dai la kugawiwa haki yake. Badi anaupuuza uhitaji wa Alii na kumtukana na kilicho chake. Hili linamkasirisha Alii ambaye anaazimia na kuahidi matumizi ya nguvu kujipatia haki yake. Kulingana Badi, hivi ni vitisho vya mbobokwaji huyu. Isitoshe, Badi haoni kuwa mtendaji hutangaza mipango yake kwa adui yake. Maoni haya yanaeleza fikra za watu wengi waovu kama Badi ambao huuwa na kuwatesa wapinzani wao kwa siri. Ndio maana labda akamwona Alii kama muotaji kwani si kawaida ya wahalifu kama yeye kutangaza vitendo vyao.

Badi, bila shaka, ameusikia ujumbe wa Alii. Kutokana na tathmini ya uhusika wake, mhusika huyu atatumia lolote kuhakikisha kwamba mnazi haumdondoki mikononi mwake. Udhalimu huwaganda hadi pale wanapopatwa na hatima mbaya.

#### 4.6.3. Wahusika katika 'Usiniuwe'

Maigizo haya yana wahusika watano. Hawa ni pamoja na nofu la nyama likiwa ni mtoto ambaye hajakomaa, Mama, Uhai, Haki na Mauti. Wahusika wanne wa mwisho wanatudhihirikia kupitia kwa mhusika Mtoto. Ni mhusika huyu anayeyaendeleza maigizo haya. Uhusika wa wahusika wengineo unatudhihirikia kwa kuzingatia kauli za mtoto huyu.

##### 4.6.3.1. Mtoto

Mtoto katika maigizo haya anawakilisha hali ya kuukosa usaidizi na kukatika kwa tamaa ya kuishi kutokana na tishio lililomsibu la kupokwa uhai. Mandhari aliyomo mtoto inatuelekeza katika kuutafakari utupu wa maisha yake. Tumboni alimo tamakani

mtoto huyu ni mahali ambamo mnampatia mama uwezo wa kumuavya mtoto huyu iwapo angependelea hilo. Na kwa hakika hilo ndilo mama wa maigizo haya alilodhamiria kulitenda.

Mtoto kwa upande wake amepewa ufahamu wa kujua kile mamaake anachonuia kukitenda. Uzuri wa maigizo haya unatokana na kuhuishwa kwa nofu hili la nyama ambalo linaongea kwa kauli zenye uzito zaidi - zikiwa zinatoka kinywani mwa mhiniwa mwenyewe. Janga linalomkodolea macho mtoto huyu linamfanya aingie mbioni kuutetea uhai wake. Lengo kuu katika kilio chake ni kupewa fursa ya kuishi kama binadamu wengineo. Mtoto anasihi asiuwawe; chambilecho maigizo yenyewe 'Usiniuwe'. Kilio hiki kinaelekezewa Mama, Uhai, Haki na Mauti. Wahusika hawa wanaolililiwa, ama ni watetezi, au wenye uwezo wa kuzuia tokeo baya linalomkabili.

Kwa ukakamavu, mtoto anatoa masuto kwa mamake. Ukakamavu huo unamfanya asaili mkosa kati yake na mamaake. Kani ya mamaake ya kutaka kumuuwa anaitilia mushkili kwani kujiri kwake si kwa kupenda kwake. Anarejelea mizizi ya kosa lenyewe, likiwa lina mamaake mwenyewe. Katika kuuweka wazi ukweli wa mambo, mtoto anatumainia kwamba 'lazima ya kumuuwa aliyoishikilia' mamaake huenda ikaachiliwa mbali. Kwa kuachiliwa mbali lazima hiyo, tumaini la kuishi huenda likapatikana.

Kwa kupewa uwezo wa kuwasiliana na mamaake akiwa tumboni, Mtoto anaeleza kwa ufasaha vitendo vilivyotokea hadi vikasababisha kupatikana kwake. Yeye si mkosa asilani. Mamaake ndiye wa kulaumika kwa kujiruhusu aongozwe na hawaa zilizomfanya ajipeleke mweyewe kwa huyo 'mwandani' wake. Anasimulia kuingia kwao mbioni - tangu kuanzana hadi kumalizana kwao katika kufanya mapenzi. Mtoto anamkumbusha mama jinsi macho yake na ya mwendani

wake yalivyokutana, kupeana burudani ya maneno tamu, na kutekeleza kitendo chenyewe cha kuzini. Anamsuta mamaake iwapo alilazimishwa na kutoitafakari hatima ya kuzini huko. Na iwapo alifanya yote hayo kwa hiyari, na kwa furaha, basi yeye haoni kwa nini awe kafara la kosa lake mwenyewe.

Tumboni, makazi ambayo kila mwanadamu hunawiria kabla kuingia duniani, ni mahali ambapo si rahisi kwa wanadamu kupatafakari. Tajriba zetu zinatufanya tuuone uanadamu katika misingi ya umbo la kawaida. Chanzo na ukuaji wa watoto kwenye matumbo ya mama zao huwa ni suala tusiloliwaza kamwe. Mama, akiwa anaihofu lawama, anaelekea kughasiwa na kiumbe kilicho ndani ya tumbo. Kiumbe hicho, kwa sasa, anakihisi tu na hakithamini kwani hakioni katika ukamilifu wake. Anakiona kama kitu kilichomzukia ghafla bila kukitarajia. Hilo linamshangaza mtoto hasa anapojua kwa yakini kwamba ni mamaake mwenyewe aliyejitakia kuwepo kwake tumboni. Mtoto anaeleza kuwa yeye si kizuka bali ni kiumbe wa kawaida kama viumbe wengine ambao kwa kawaida huwa;

Ni manii tone moja, la maji madhalilifu
Tone lililojituja, kutoka maji machafu
Ndicho chanzo changu kuja, na bado ndiya ni ndefu
S'anze sasa kunifuja, mamangu nihurumiya

Kwa kina mama wengi, akiwamo mhusika Mama wa maigizo haya, kuanza kwa hofu zao na kutuhumu kuwa ni waja wazito, ni suala la kiwakati. Ni baada ya muda, pengine kwa kuzikosa hedhi zao, ambapo wanakuwa na yakini kwamba ni waja wazito. Purukushani za kuziavya mimba huanza.

Juhudi za mama za kutaka kumuavya Mtoto ni kitendo cha unyama. Mtoto anaona kuwa ni mama mwenyewe ambaye alitaka aje ulimwenguni kabla ya kuubadilisha msimamo wake. Kwa kukubali

kwenda kwenye faragha na mwendani wake, Mama alikuwa amekubali kumpa uhai ambao kwa sasa anauhatarisha (ubeti 13). Kwa Mtoto, uhai huo angeuchukua kwa kukataa kushiriki zinaa - jambo ambalo lingeukatisha uhai wake kwa kutopewa fursa ya kutamakani tumboni alipo.

Yaliyomwagika hayazoleki. Hilo tu ndilo mtoto analoweza akasema. Kwa kuwa mamaake alikubali kumweka tumboni, anasihi aachwe hadi akomae. Njiani atakapoachwa ana matumaini kuwa walimwengu huenda wakamnusuru na kuishi kwa kuitegemea kudura ya Mungu duniani. Maisha kwake ni suala la kimajaaliwa. Duniani, ataishi 'awe shetani au mtawa' kwake yote ni sawa (ubeti 23).

Mama haelekei kushawishika na hoja za mtoto. Uhai wa mtoto umo hatarini. Usaidizi ni lazima upatikane. Ndipo Uhai, Haki na Mauti wanapoitwa kuwa waamuzi kati yake na mamaake.

## 4.7. Mandhari

### 4.7.1. Mandhari katika 'Kutendana'

Maelezo katika maigizo haya ndiyo yanayoshughulikia suala la mandhari kwa undani. Maelezo haya ni juhudi za mwandishi za kutaka kutoa sura kamili ya mahali wanamoishi wahusika wake. Ingawa maelezo haya yanajitokeza katika sehemu za katikati mwa maigizo, usomaji wetu unatakikana uturudishe nyuma kimpangilio kabla ya kuanza kwa maigizo yenyewe. Hili linaashiriwa na maelezo (uk. 105) yenyewe ambayo baada ya kueleza mambo mbalimbali, yanagusia mandhari yanayosema;

> Ndipo hapo mvutano, ulipoanza mwanzowe
> Utadhani mashindano, ya malenga mfanowe
> Kila atowaye neno, 'kijibiwa na mwenziwe
> Ukawa ule mfano, wa 'twaa' na 'twaa wewe'

Mvutano unaozungumziwa na maelezo haya si mwingine ila ule wa

Mwanamke na Mwanamume. Kimpangilio maelezo haya yanastahili kujitokeza mwanzo ili tajriba kamili ya maigizo yenyewe ipate kukamilika. Pengine ndiyo sababu tukayaona maelezo haya yakijaribu kututayarishia mandhari ya jukwaa letu.

Tunaelezwa kwamba muda uliopo kabla ya kuanza kwa mvutano huu ni zaidi ya saa tano za usiku. Muda huu unaashiria kuwa giza totoro lilikuwa tayari limechukua mahala pa mwanga wa jua. Maelezo haya hayasiti kuieleza saa na giza hilo kwa mshangao. Yanasema;

Pili twangaliye saa, yalipotukiya hayo
Giza lali mesambaa, kwa mvuwa kuu inyayo
Hata zile nyingi taa, mbingu zing'arishayo
Hata mojapo angaa, haikujitokezayo

Mbali na giza ambalo linaelelezwa na saa, kuna pia mvua inayonyesha ambayo tunatarajiwa tuione kama wasomaji.

Jukwaa linazidi kupewa mapambo yake yanayostahili kwa kuonyeshwa mahali walipo wahusika hawa. Mwanamke tunaelezwa;

Bibi ali mejinyosha, kitanda cha ukumbini
Taa aliirudisha, utambi ukawa tini
Kusudi kuliepusha, joto lisizidi ndani
Na piya halikutosha, kipepeo mkononi

Maelezo haya yanatuzalishia picha ya pale alipo Mwanamke. Jukwaa linapofunuliwa tunatarajiwa tumwone mhusika huyu akiwa amejinyosha kitandani. Kitanda hicho tunatajiwa pale kilipo, ukumbini. Hata hivyo, mwandishi haonekani kama ameyazingatia vilivyo mapambo yake ya kijukwaa kutokana na maelezo yanayohitilafiana. Haiyumkiniki kunyeshe na kuwe na baridi huko nje pasina hali hiyo kumfikia Mwanamke. Badala yake, Abdilatif anajaribu kutuelezea ya joto na vipepeo katika nyumba.

Nje ya dirisha la chumbani mwa Mwanamke ndipo tunapomwona Mwanamume. Mhusika huyu yuko katika hali mbalimbali ambazo

tunaweza tukaziangalia katika muktadha wa kimandhari. Tunamwona akiwa amelowa kutokana na mvua, ikimaanisha umajiumaji kwenye jukwaa. Jambo hili linahakikishwa na malalamiko ya Mwanamume mwenyewe anaposema;

> Nateseka kwa mvuwa, ni chapachapa mwilini
> Au hivi ni muruwa, kusema kwa dirishani
> Mlango hebu funguwa, uwate ningiye ndani...

Mwanamume huyo amesimama penye dirisha akilalama afunguliwe mlango. Bongo zetu zinauona ukuta wa nyumba wenye dirisha, ukiwatenganisha Mwanamke na Mwanamume.

Kwa muhtasari haya ni mapambo ya kimandhari ambayo mshairi wetu wa kimaigizo anajaribu kutuandalia kabla ya kuanza kwa malumbano ya wahusika hawa wawili. Maelezo haya yanayohusiana na mandhari yanatutayarisha kuona vitushi mbalimbali vya maigizo haya.

<u>4.7.2. Mandhari katika 'Mnazi Vuta N'kuvute'</u>

Onyesho moja la maigizo haya linatumia mandhari moja ambayo inafafanuliwa na wahusika wenyewe. Kwa upande mmoja yupo Alii, ambaye, anapotokeza jukwaani anaeleza;

> Ndugu ulo mnazini, wanitafuta balaa
> Nakwambia shuka tini, katakata wakataa
> Wafanya ni masikani, mustarehe 'mekaa
> Utashuka au la?

Kauli hii ya Alii pekee inatosha kutufahamisha mkabala wa kimahali kati yake na Badi. Badi yupo juu ya mnazi, ikimaanisha kwamba Alii yu chini.

Hata hivyo, Abdilatif anajizatiti kutuondolea makisio ya kimahala. Anajaribu kutuelezea kwa usahili mahali alipo Alii. Wakati huu, ni Badi ambaye anatumiwa kueleza mahali alipo Alii. Jawabu yake inasema;

Ndugu tini ya mnazi, nilo juu nakujibu
Haya ni ya upuuzi, unambiyayo swahibu
Kushuka tini siwezi, pasi kujuwa sababu
Hiyo ni yangu jawabu

Maneno wanayotumia Alii na Badi ndiyo yanayotuelekeza kufahamu wahusika hawa walipo. Picha inayotujia katika bongo zetu ni kuwepo kwa mnazi kwenye jukwaa. Kwenye mnazi huu ndipo tunapowaona wahusika hawa wawili; Badi akiwa juu, Alii akiwa yu chini.

Mnazi unatufanya tusaili umuhimu wa kuteuliwa kwake kama kifaa cha kimandhari ambacho kitendo kizima cha mchezo kinautegemea. Umuhimu huo unatufungukia hasa kwa kufanywa urithi kwa ndugu hawa. 'Vuta N'kuvute' iliyopo inatokana na mnazi - ikiashiria kuwa mandhari iliyoteuliwa ni mwafaka.

Kuonyeshwa kwa mahali mahsusi walipo wahusika Alii na Badi ni kipengele kimojawapo cha mandhari. Wahusika hawa wanakuwa sehemu ya mandhari pia kwa kuzingatia picha inayotudhihirishia bongoni mwetu. Picha ya mnazi inakamilishwa na kuwaona Alii akiwa chini na Badi akiwa juu ya mnazi huo. Mandhari hiyo inayojumuisha mnazi, Alii na Badi ni kifaa kinachoashiria kwa nguvu zaidi. Mnazi wenyewe, ukiwa mmea wenye faida, unaonekana na thamani zaidi kwa kupiganiwa na ndugu wawili hawa. Kuwa mmoja yuko juu na mwingine chini, wote wakipigania kuukwea mnazi, ni ushuhuda tosha kuwa mnazi ni mmea unaostahili kupiganiwa.

Ushahidi wa kimaelezo pia unaashiria kuwa mnazi ni mmea wa faida. Badi ambaye yuko juu ananyookewa na maisha. Familia yake inatononoka kwa vyakula vinono, mavazi bora na kwa jumla kuishi bila taabu. Yote haya ni kwa kuwa juu ya mnazi ndiko kwenye nazi, na hivyo basi, kiini cha uhai. Badi keshaukwea mnazi na ndiye mwenyewe kwa kuwa ameushika.

Kwa Alii, maisha ni mizonge mitupu. Yeye yuko chini bado. Ili kuzifikia nazi, ni sharti aukwee mnazi hadi afikie mahali alipo Badi. Na hata kama angefaulu kuukwea mnazi, basi nazi zote zilizokomaa zitakuwa zimeliwa na Badi. Suluhisho ni kushuka kwa Badi - jambo ambalo Badi analikatalia.

Kwamba Alii yupo chini ya mnazi ni ishara ya kuyakosa matunda ya mti huo. Wazo hili ni kinyume na kuwekwa kwa Badi juu. Kwa upande mmoja tuna wenye uwezo, walio juu, yaani akina Badi ambao wamebobea katika ufanisi. Ufanisi huo, kwa bahati mbaya, umewasakarisha. Kuwa au kutokuwa nacho ni tokeo la msemo wa kale unaosema /Alobwiya ndiye mwenyewe, alowata uzuzuwe/. Kwa upande mwingine wapo kina Alii ambao mahala walipo panawafanya wabaki wakiwayawaya, wakikosa pa kujiegemeza.

Mandhari hii ya mnazi na wakweaji wake ni mbinu mwafaka inayotumiwa na Abdilatif kuileta kwa uwazi picha ya vuta nikuvute ya maigizo haya.

4.7.3. Mandhari katika 'Usiniuwe'

Kama vile katika 'Mnazi: Vuta N'kuvute', maigizo haya ya 'Usiniuwe' yanategemea mhusika Mtoto kutupatia fununu ya mandhari iliyotumika. Mtoto huyu amepewa uhai unaomwezesha kuzungumza kama mwanadamu aliyekamilika. Anavyojieleza, yeye bado ni nofu la nyama ambalo halijakamilika kiumbo (beti 10-11).

Maelezo yanayotumiwa na mtoto kulieleza umbo lake ni changomoto ya wasomaji kufahamu mahali alipo mtoto au nofu hili la nyama. Ingawa hatuelezwi kwa uwazi mandhari ya maigizo haya, maelezo haya bila shaka yanaashiria mandhari ya tumboni mwa mama ambaye kwa wakati huu ni mja mzito. Mtoto huyu anayeongea

anatufanya tufikirie nofu hilo na umajimaji uliomo ndani ya tumbo la mama huyu.

Tumboni ni mahali salama pa mtoto anapotamakani na kukulia baada yo tone 'la maji madhalilifu' kuanguka 'mahalipe maalum'. Mtoto humtegemea mamaake, anayembeba tumboni, kwa uhai wake. Chakula na pumzi za mama ndio msingi wa maisha wa mtoto huyo. Kwa watoto wasiobahatika, akiwemo huyu wa 'Usiniuwe', mama zao, kwa sababu wanazozifahamu wenyewe, huona vyema kuwaavya. Mama hawa, kama wale wanaozitunza mimba zao, wana uwezo pia wa kuziharibu mimba hizo wanapotaka. Hivyo basi, uhai wa watoto ni suala lililomo mikononi mwa akina mama. Ndani ya tumbo ni salama, na vilevile, bahari ya misukosuko.

Hivyo ndivyo anavyojikuta mtoto. Tumboni alimo si salama. Uhai wake umo mikononi mwa mamaake ambaye kwa sasa anauhatarisha. Kwa kulipatia uhai nofu la nyama, Abdilatif anaitoa picha ya jinsi mandhari ya tumboni inavyoweza kuwa bahari tesi na kuzidi dhuluma. Kama vile anavyombeba tumboni kwa hiyari, mama pia anaweza akamtimua mtoto tumboni humo kufumba na kufumbua.

Mandhari na mahali alipo mtoto inatusaidia kuufahamu vizuri ukosefu wa matumaini ya mtoto katika maisha. Hali hiyo inaoanishwa na kauli za kimaombezi za mtoto ambazo zinaradidiwa na kipande cha mwisho cha kila kibwagizo. Mtoto amekuwa mithili ya ombaomba, akisihi ahurumiwe. Kwa undani tunaona jinsi viumbe dhaifu wasioweza kujitetea wanavyotiwa hekahekani na wenye nguvu. Tofauti na Alii ambaye anao uwezo wa kujitetea, hapa tuna kiumbe ambacho hakina uwezo huo. Unyanyasaji huu umekiuka mipaka kwani hapa tunao viumbe wasiokuwa na uwezo wowote wa kujihami. Uhai, ambao ni haki kwa kila kiumbe, umekuwa amali ya mama na wala si

ya mtoto tena.

Mandhari, kama vile wahusika, kitendo na mbinu nyinginezo ni mifumo ishara ambayo inaashiria na kutupatia tajriba ya maigizo haya.

**4.8. Maleba**

Maigizo ya 'Kutendana' yanadhihirisha umuhimu wa maleba kama nyenzo thabiti ya kuhisika kwa maigizo yoyote. Abdilatif, amelichukua jukumu la kumpamba mhusika Mwanamke kwa lengo la kuiathiri hadhira yake. Beti nane zimetumiwa kumfafanua Mwanamke, lengo likiwa ni kuuleta karibu zaidi uzuri wake kwenye fikra zetu.

Bibi huyu anapendeza kutokana na kuzingatiwa kwa maleba na mwandishi. Maleba haya, kwa jinsi yanavyotamanisha, yanatuvuta karibu katika kuuelewa mfadhaiko unaompata Mwanamume anapomwona. Ukamilifu wa uzuri wake umetokana na uteuzi wa vifaa vya kurembesha vilivyoteuliwa kwa ustadi. Maelezo yanatueleza kwa urefu kuwa;

Manukato muwilini, vyema yalifukiza
Ni nyudi za Arabuni, ambari na kadhalika
Ambao wavibaini, wajuwa vinavyonuka
Msojuwa ulizani, kwa ambao vyatumika

Isitoshe muwilini, vyema yalifukizika
Mpya ambazo dukani, leo leo zintoka
Nazo piya chetezoni, alikuwa 'meziweka
Zafurahisha puani, harufu njema zanuka

'Kimtizama kitwani, nyele zilivyotanika
Uzitizame na pini, jinsi alivyotomeka
Na shada la asumini, alivyo kulipatika
Lazima utatamani, ngaa upate zishika

Basi uje shingoni, shingo mfano wa ninga
Ni mjuzi wa kwa yakini, huyo aliyeitonga
Ukitizame kidani, shingoni alojifunga
Sijuwi ni fundi gani, ambaye alikitunga

Liwa jembamba usoni, alikuwa ampaka
Akatinda na sikini, vizuri ikatindika
Nacho kijembe nyushini, hakikusahaulika
Umwonapo utadhani, si mja ni malaika

Na humo mwake matoni, ni wanda ameupaka
Ule wanda wa Mangani, mno unaosifika
Namo mwake midomoni, wekundu unzunguka
Si wa rangi Ulayani, ni mdaa kutumika

Vya dhahabu viungoni, vyombo amvipambaniza
Kipini kimo puwani, kilipo kimpendeza
Vipuli masikiyoni, vyandani pete ongeza
Na bangili mikononi, kiyasi hakuzijaza

Tumenukuu sehemu hii ya maigizo yetu kwa urefu kwani ndiyo inayotoa kwa muhtasari ufundi wa maleba alioutumia mwandishi.

Mapambo haya hayakutumika kwa ajili ya kutumika kwa mapambo tu. Kila pambo limetumika kunakshia sehemu ya mwili inayohusika. Wakati ambapo nyudi na ambari zinatumiwa kuikoleza hewa kwa harufu inayovutia, wanda, mkufu na pete zinanakshi viungo husika kuleta dhana ya uzuri uliokamilika wa Mwanamke. Kila pambo lina uamilifu wake ambao unalengwa kumvuta Mwanamume na hadhira pia katika kuuhisi uzuri wa Mwanamke.

Mbali na maleba kuwa chombo cha kuueleza uzuri wa Mwanamke kiupeo, tunawajibika pia kuyatazama kama chambo cha kumtia Mwanamume mtegoni. Mwanamume 'anatendwa' kama vile alivyomtenda Mwanamke. Uchu, na ari ya kutaka kuumaliza uchu huo kwa Mwanamke, ndiyo dhamira na lengo lililomleta Mwanamume huku. Uchu pekee ni sababu tosha ya kusababisha fedheha. Mapambo ya Mwanamke, kwa jinsi yalivyosimuliwa, yanatuacha tufikiri kizunguzungu kitakachompata huyu bwana. Si ajabu kuyaona maelezo yakimtanabahisha msomaji, kumstaajabikia Mwanamume, kwa kumwambia;

Nne tizama mapambo, bibi alojipambiya
Fikiri vipi mrembo, ambavyo alitokeya
Lau angekuwa chombo, samaki angeshikiya

Yaswawiri haya mambo, n'nayokudondoleya

Mapambo tunayoelezewa yanamulikwa uamilifu wake; kuwa ni nyenzo ya kuuhamasisha uchu wa Mwanamume.

Maleba, kama vile wahusika, mandhari, na hata ploti, ni kipengele ambacho kina nafasi muhimu kama mfumo ashiriaji katika maigizo haya ya 'Kutendana'.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO

## 5.1 Utangulizi

Baada ya kuisarifu na kuimulika mada ya tasnifu hii, azma kuu sasa ni kuyashadidia masuala kiungo yaliyodhihirika. Mkazo huo utajengwa kutokana na kuzingatiwa kwa suala la mawasiliano, hususani, katika tungo zilizoshughulikiwa. Tumeonyesha ustadi wa Abdilatif katika kuzitumikisha mali ghafi mbalimbali za kimaigizo, ikiwemo lugha kama nyenzo kinara katika uwanja wa mawasiliano. Hapa tunaazimia kuonyesha uhusiano wa mbinu hizo kama nyenzo na msingi wa kuhisi, ili kuibuka na tajriba na maana ya maigizo yetu. Dhana hizi tatu tumekuwa tukizirashiarashia tu kila tulipokuwa tukiijadili nafasi ya hadhira.

Kauli shakiki na maoni yetu kuhusiana na tungo hizi kama kazi za kisanaa zinazostahili kuigwa, kwa jinsi zinavyozingatia masuala ya kisemiotiki, zimetolewa. Hatimaye, tumetoa maagizo na mapendekezo yanayolenga maeneo mbalimbali, likiwemo lile la watafiti wengineo.

## 5.2. Masuala ya Kuhisi, Tajriba na Maana katika Maigizo

Maigizo, kama tulivyodokeza hapo awali, ni amali ya mzunguko wa utatu unaojumuisha mtendaji, jukwaa na hadhira. Tumekuwa tukizichanganua matini za Abdilatif. Tumezisoma matini hizo kimaigizo ili kuibuka na maigizo ambayo tajriba yake ingepatikana kwenye jukwaa halisi la kuigizia. Jukwaa letu limekuwa bongo zetu, tukiyashuhudia maigizo humo.

Kushuhudia kwetu kwa maigizo hayo hayakuwa matokeo ya kisadfa. Abdilatif amelichukua jukumu lililotokana na kufahamu kwamba ipo haja kubwa ya kuzingatia kuwepo kwa wahusika, hadhira

na jukwaa lenyewe ambapo shughuli za nipa nikupe zitatekelezewa, hata kwa yule msomaji aliyejikalia faraghani na kuzisoma tungo zake.

Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa, kwa mfano, umetajwa kama utungo wenye sifa ya kuipoza kiu ya yule aliyekosa fursa ya kujionea michezo ikiigizwa kwenye jukwaa halisi. Hili pia tunaweza tukalidaia tungo zake nyinginezo za 'Kutendana', 'Mnazi: Vuta N'kuvute' na 'Usiniuwe'. Ni matilaba yetu kuangalia jinsi Abdilatif alivyoweza kuzitumikisha mbinu za kimaigizo na kuipoza kiu yetu ya kuyaona maigizo halisi. Madhumuni yetu, ya jinsi dhana ya maigizo katika tungo za mshairi huyu ilivyojitokeza na vilevile usomaji maalum wa kisemiotiki unaotufanya tuzihisi tungo hizi licha ya kuwa ni ushairi wa kijadi, yalitekelezwa.

Mjadala huu unaturudisha kwa Topan (1971) na maoni yake kuhusu utenzi tulioutaja hapo juu kuwa, ni andiko linalomwezesha msomaji kuiona drama ikitendeka, pindi msomaji huyo anapotafakari kwa undani yale anayoyasoma. Tunakubaliana na mawazo ya Topan. Hata hivyo, ingefaa tuongezee kwamba utungo huu na maigizo mengineyo tuliyoyashughulikia hayahusishi 'kuona' tu bali mwanda mzima wa hisi za msomaji. Mbali na kuona, msomaji anachemshwa milango mingine ya fahamu ya kuonja, kugusa, kusikia, kunusa na pia kufikiria. Abdilatif amefanikiwa kuifikia milango hiyo ya fahamu, kwa jinsi alivyoisheheni lugha yake, kwa taswira mbalimbali. Lugha ya mshairi huyu inalengwa kuziathiri hisi tulizozitaja, hivyo basi, kumpa msomaji ule uwezo wa kuwa mshuhudiaji wa maigizo yake akiwa faraghani.

Hisi za kibinadamu, kwa kiwango kikubwa, ndizo zinazotufanya

tuibuke na tajriba ya maigizo haya. Tunaweza tukaieleza tajriba kama uzoefu wa kitu, au jambo, unaotokana na kujiradidi kwake katika dira ya hisi (Perrine 1988). Katika maigizo haya, tajriba inayomuibukia msomaji ni zao la kutumikishwa kwa hisi zake. Lugha ya kishairi, kama ilivyodhihirika katika sura ya pili, imelifanikisha suala la mguso wa hisi za hadhira. Tumeziona taswira sufufu alizozitumia mshairi huyu kama ushuhuda wa uzito wa hoja hii. Tumeona, kwa mfano, kwamba kwa kuzingatia tajriba inayoambatana na hisi za kuonja na kugusa, tunda la mti wa haramu limeweza kuwa njia ya kuelewa masuala mbalimbali yanayoambatana na maigizo ya utenzi wake. Tunda, mbali na kuwa tunda la kawaida, lina uwezo wa kusimamia dhana za uhuru wa kiuteuzi na, vilevile, pambano la kiuana. Kwa kuzitumia hisi zetu za kuonja na kufikiria, Abdilatif amezifanya hisi hizo ziutumie uzoefu wake katika kuleta taathira inayoambatana na maana hizo.

Aidha, tumeona jinsi lugha ya maigizo haya ilivyojaribu kutuchorea picha zinazoonekana waziwazi. Abdilatif anaibuka kuwa mshairi wa kijukwaa ambaye anaifanya lugha iwe tendaji kwa jinsi inavyoweka machoni mwetu hali halisi za kidrama. Hapa tunatilia maanani vitushi mbalimbali ambavyo baadhi yavyo tumeviona vikiwatanza hata wahusika wenyewe kiasi cha kukosa maelezo ya kuzifafanua hali wanazozishuhudia. Adamu, katika <u>Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa</u>, kwa mfano, anashangaa kumwona Hawaa anapotokea kwa mara ya kwanza. Mbinu hii pia inajitokeza katika tungo zilizomo katika <u>Sauti ya Dhiki</u>. Tunaweza tukayataja masaibu ya Mwanamke katika 'Kutendana' anapojiwa na Mwanamume dirishani. 'Mnazi: Vuta N'kuvute' ni utungo ambao unatuwasilishia picha ya wakinzani wawili, Alii na Badi: mmoja

akiwa juu na mwingine akiwa chini ya mnazi. Vilevile, tunapatwa na msisimko fulani kutokana na picha ya kitoto kilichomo tumboni mwa mamaake katika 'Usiniuwe'. Hali hizi zinajengwa kwa ustadi, zikionekana barabara machoni mwetu. Kutumikishwa kwa hisi zetu za kuona na lugha hii ya kipicha ambayo inatufanya tujumuike katika kuziajabikia hali hizi za kidrama, ni miongoni mwa juhudi za mwandishi za kutuwezesha kuipata hisi ya maigizo yake.

Tumeona katika tasnifu yetu jinsi lugha, wahusika, ploti, kitendo, kaida, mandhari na mbinu nyinginezo kama vile maleba zinavyoweza kutumika kama mifumo ya uashiriaji. Maudhui mbalimbali yamejadiliwa na Abdilatif kutokana na kutumikishwa kwa mbinu hizo. Maudhui hayo, tunaweza tukasema, ni maana mbalimbali ambazo mshairi huyu ananuia kuziwasilishia hadhira yake. Mshairi wetu wa kimaigizo amefaulu kutuwasilishia maana kemkemu kwa kututeulia ishara zenye nguvu za kuashiria. Mbinu za kimaigizo alizozitumia Abdilatif ni mifumo ya mawasiliano ambayo kwayo hadhira inathibitikiwa na maana ya maigizo husika.

Mafanikio ya mbinu hizo, kama mifumo ya mawasiliano, yametokana na kushikamanishwa kwa kila mbinu na nyenziye hadi zikawa zinatoa maana inayojengana. <u>Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa</u> ni maigizo yanayozungumzia swala la kuumbwa kwa mwanadamu wa kwanza huko mbinguni, hadi kufikia hatima yake ulimwenguni. Kupitia mbinu mbalimbali za kimaigizo alizozitumia Abdilatif, maigizo haya yanakuwa ya kufana. Kila mbinu iliyotumiwa inajaribu kueleza mapito hayo ya mbinguni hadi ardhini. Kisa chenyewe, kama kinavyoelezwa katika misahafu, ni cha kitanzia. Kwa kulizingatia hilo, Abdilatif anaitumia mbinu ya kitanzia inayomfanya Adamu, mhusika anayejikuta katikati ya raha huko

mbinguni, kuishilia duniani, mahali palipojaa uhasama na chuki. Usukaji wa kisa hiki umeyafanya maigizo haya kuwa na mtiririko ambao ni tofauti na vile kisa hiki kilivyowasilishwa katika misahafu. Maigizo haya yamewekwa katika ploti inayomwezesha msomaji kuipata maana kwa njia ya urahisi na ya kuvutia kuliko kukisoma kisa hicho nusunusu katika misafu. Usuhubiano tuliouona kati ya wahusika ni tamko kuhusu jambo hilo. Mungu, Adamu, Hawaa, Ibilisi, Habili na Kabili ni wahusika ambao kila mmoja tumemwona akichangia hatima hiyo ya mwanadamu. Kitendo cha maigizo haya, kama tulivyodhihirishiwa na vitendo halisi vya kimwili na kikauli, nacho pia kimekuwa na nafasi ya kutumulikia anguko hilo. Hatuwezi tukasahau na mandhari, hususani ile ya peponi, ambayo ndani yake mna mti unaokuwa kisababisho cha anguko la Adamu na Hawaa.

Mbinu mbalimbali katika 'Kutendana', ni mfano wa jinsi Abdilatif alivyofanikiwa kuzioanisha mbinu hizo na kueleza maana ya kutendana. Kila mbinu inadokeza kivyake maana ya kutendana. Tukichukua maleba yaliyotumiwa na mshairi huyu, tunaona ustadi wake wa kumchagulia mhusika wake kile ambacho angekitumia kujirembeshea. Mbali na kumbabaisha Mwanamume ili apate 'kutendwa' au kulipizwa kisasi, maleba pia yanamsimanga kama mwanamume asiyejua kumtunza mwanamke. Wazo hili la kutendwa linatiliwa mkazo kivingine na mandhari. Mwanamume, mhusika hasidi, anawekwa mahali pasipokuwa salama, pa mvua na giza totoro. Mkabala na mandhari hii ni kuwekwa kwa Mwanamke ndani ya nyumba ambamo ni salama kutokana na giza, baridi iliyokithiri na hata mvua. Ipo lugha nayo, ambayo mbali na kuwa mfumo kinara wa mawasiliano yote, inaelekea kumpa ushindi wa 'kutenda'

Mwanamke. Mfano wa kutajika hapa ni kutongolewa kwa maneno anayoyatumia Mwanamume na kumchachia yeye mwenyewe. Sambamba na kauli hizo ni vitendo ambavyo vinamshauri Mwanamume ajitafutie mwingine. Kaida zilizotumika, vilevile, zinajaribu kutuelekeza kumwona Mwanamke kama nguli anayeshinda katika masimbuliano haya. 'Maelezo' aghalabu yanajitokeza na upendeleo - yakimsifu Mwanamke huku yakimuumbua Mwanamume.

Aidha, maigizo ya 'Mnazi: Vuta N'kuvute' nayo yanatumia mbinu mchangamano za kimaigizo kuyafanikisha. Maana ya kuvutana inaelezwa na, miongoni mwa mengineyo, watendaji wakuu Alii na Badi, ambao kauli zao zinatudhihirishia mvutano unaoishilia na vitisho vya umwagikaji damu. Tofauti zao za kimandhari nazo ni kauli thabiti za kuvutana kwao; Alii akiwa hana uwezo wa kujikirimu kwa kutokuwa juu ya mnazi alikotamakani Badi.

'Usiniuwe' kadhalika ni maigizo yaliyosukwa kwa mbinu mbalimbali za kimaigizo zinazomulika maana hiyo ya 'usiniuwe'. Kinachozivuta nadhari zetu zaidi ni ule uwezo wa mhusika Mtoto kuwasiliana na mamaake juu ya uhai wake. Kauli zake, zilizojaa maombezi, masuto na masimango, zinajaribu kumkanya mamaake anayenuia kumpoka uhai. Mtoto huyu anaisukuma kesi yake mbele kwa wahusika Uhai, Mauti na Haki, angalau asiuwawe. Uhai wake umo mikononi mwa mtu asiyeweza kuzuiwa. Hivyo ndivyo mandhari aliyomo inavyojaribu kueleza. Tumboni mwa mama ni mahali rahisi kwa mamaake kumtimua anapoamua hivyo. Ploti nayo, ambayo imeuteua mgongano wa kutaka kuishi kwa Mtoto dhidi ya tamani za Mama za kutaka kumuavya, inatudokolea haja ya mtoto ya kuomba asiuwawe.

Maigizo tuliyoyashughulikia yametumia mbinu za kimaigizo,

ambazo kila mojawapo inajaribu kutoa kauli juu ya swala kuu la maigizo husika. Tajriba ya maigizo, kuhisika kwake, na suala la maana, ni mambo yanayotegemea kushikamanishwa kwa mbinu hizi za kimaigizo.

## 5.3. Mapendekezo na Maagizo

Semiotiki, ikiwa nadharia inayotamba kwenye mifumo yoyote ya kimawasiliano, si amali ya kushughulikia taaluma ya ushairi-jadi pekee. Azma yetu kuu ilikuwa ni kuutazama ushairi wa Abdilatif kama mfumo wa mawasiliano uliotomelewa ishara mahsusi za kimaigizo. Kwa kuzizingatia mbinu alizozitumia mshairi huyu wa kimaigizo, tumekuwa vilevile tukiutazama ushairi wake kama kazi ya kisanaa inayojiashiria. Hatuwezi kamwe tukadai kuwa ushairi wake ni sanaa ya vina na urari wa mizani tu. Mazingatio ya kisemiotiki yametimizwa katika ushairi wake. Jukumu la lugha yake ya kishairi limefana katika kuibua hisi ya maigizo.

Kufuatana na ufunuo huu tulioutoa, semiotiki ya ushairi pia inaweza ikaelekezwa kwa ushairi wa kimabadiliko. Haja ya kuzamiwa kwa ushairi huu inaelezwa na Mohammed (1990: 142), ambaye, akiutetea msimamo wake wa kulibagua shairi huru na la kijadi, anasema;

> ...Kwanza, mitindo au mikondo hii miwili ya mashairi inaonyesha tofauti kubwa, kiasi cha kwamba kumekuwa na haja ya kuitenganisha. Pili, shairi huru lina sifa zake ambazo ingawa mwahala mwingine zimetajwa hazikufafanuliwa kwa upana sana.

Hima ya kupigwa darubini kwa ushairi wa kisasa ipo. Uyakinifu wa vijengo mbalimbali vya ushairi huru utaielea hadhira kwa kuziweka bayana ishara tofauti tofauti ambazo waasisi wa kundi hili wanadaia ushairi huu. Tungo zilizotia fora, zikiwemo

Kichomi na Karibu Ndani za Kezilahabi, na shairi 'Ngoma na Violini' la E.Hussein ni maandiko ambayo yanahitaji kupekuliwa kwa undani ili kuzibainisha mbinu mahsusi za kimawasiliano zinazoushamiri ushairi huru.

Tumeuchambua ushairi wa Abdilatif kimaigizo. Katika kufanya hivyo, tumekuwa vilevile tukiifafanua na kuieleza dhana ya usomaji wa tungo hizi kimaigizo. Hili limetuwezesha kuibuka na aina maalum ya semiotiki. Kazi hii inaweza kuwa mwenge wa usomaji madhubuti unaomwongoza msomaji kuipata tajriba badalia ya kazi nyinginezo zilizotungwa kimaigizo. Kwa kuvizingatia vipengele mbalimbali wanavyovitumia waandishi wa kijukwaa, tajriba ya kazi hizo inaweza ikapatikana bila ya wasomaji kuingia kwenye jumba la kuigizia. Kinachohitajika, kwa upande wa msomaji, ni kulinoa bongo lisipitwe na baadhi ya mambo ambayo huenda hata yakapuuzwa au yakaonekana ya kisadfa mwanzoni.

Msomaji sharti asaili kila jambo au wazo ambalo mwandishi analizungumzia. Ni sharti, kwa mfano, asaili umuhimu wa kutumika kwa vifaa fulani kwenye jukwaa kama sehemu ya mandhari au matumizi ya vifaa hivyo na mhusika fulani.

Katika kazi hii, tumejaribu kuonyesha jinsi Abdilatif alivyoteuwa njia mwafaka za kuwasiliana na hadhira yake. Ushairi wake, mbali na kuhimili sifa za kazi ya kishairi, unatumia mbinu za kimaigizo ambazo zinammulikia msomaji maswala mbalimbali ya kijamii. Mshikamano uliodhihirika kati ya mirengo hii miwili ya nyenzo za mawasiliano au mbinu za kimaigizo na maana katika jamii ni kielelezo cha sanaa pevu ambayo itakuwa jambo tunu la kuigwa, si katika taaluma ya ushairi, bali katika dira nzima ya uwanja wa fasihi.

## MAREJELEO


Abdalla, A. (1973) Sauti ya Dhiki. Nairobi: Oxford University Press.

Abdulaziz, M.H. (1979) MUYAKA: 19th Century Swahili Popular Poetry. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Ali, A.Y. (1963) The Holy Qur'an. Maryland: Amana Corp.

Anozie, S.O. (1981)Sructural Models and African Poetics: Towards a Pragmatic Theory of Literature. Boston: Routeledge and Kegan Paul.

Barry, T. (1970) Dramatic Sructure: The Shaping of Experience. London: University of California Press Ltd.

Bradley, A.C. (1992) Shakesperean Tragedy. 3rd Edition. London: Macmillan Education Ltd.

Brecht, B. (1991) The Cuacasian Chalk Circle. Nairobi: Heinemann Kenya Ltd.

Carpenter, W.E. (ed. 1975) Instructor's Manual for tha Art of Drama. 2nd Edition. U.S.A. : Holt, Rinehart and Winston.

Chacha, N.C. (1992) Ushairi wa Abdilatif Abdalla: Sauti ya Utetezi. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

____________ (1987) Hukumu. Nairobi: Longman Kenya Ltd.

Eagleton, T. (1983) Literary Theory: An Introduction. Minneapolis: University of Minnesota Press.

___________ (ed. 1988) John Milton: Language, Gender, Power. Oxford: Basil Blackwell.

Elam, K. (1980) The Semiotics of Theatre and Drama. New York: Methuen and Company.

Esslin, M. (1990) 'The Signs of Drama' in Walder, D. (ed.) Literature in the Modern World. New York: Oxford University Press.

Frost, A. & Yarrow, R. (1993) Improvisation in Drama. London: The Macmillan Press Ltd.

Gianakaris, C.J. (1975) Foundations of Drama. Boston: Houghton Mifflin Company.

Giraud, P. (1971) Semiology. Boston: Routeledge and Kegan Paul.

Gituku, A.N. (1990) 'Maigizo ya Kienyeji ya Watoto Kenya: Nafasi ya Kuyatumia katika Ufundishaji'. Tasnifu isiyochapishwa ya M.A., Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Gogol, N. (1987) The Government Inspector. Nairobi: Heinemann Kenya Ltd.

Haji, A.I. (mh. 1981) Misingi ya Nadharia ya Fasihi. Zanzibar: Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni/ Wizara ya Elimu Zanzibar.

Hall, D. (1987) To Read Literature: Fiction, Poetry, Drama. 2nd Edition. CBS College Publishing House.

Hawkes, T. (1977) Structuralism and Semiotics. London: Methuen and Company.

Hawthorn, J. (1985) Studying the Novel: An Introduction. England: Edward Arnold Publishers.

Hodge, R. & Gunther, K. (1988) Social Semiotics. Oxford: Basil Blackwell Ltd.

Hough, G. (1966) An Essay on Criticism. Whiltshire: Redwood Press.

Hurrow, K.W. (ed. 1992) Faces of Islam in African Literature, Portsmouth: Heinemann Educational Books Inc.

Hussein, E.N. (1985) Mashetani. Nairobi: Oxford University Press.

Jefferson, A. & Robey, D. (1982) Modern Literary Theory: A Comparative Introduction. New Jersey: Barnes and Noble Books.

Kahigi, K.K. & Mulokozi, K. (1979) Kunga za Ushairi na Diwani Yetu. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Kaplan, C. (ed. 1986) Criticism: The Major Statements. New York: St. Martins Press, Inc.

Kelsall, M. (1985) Studying Drama: An Introduction. London: Edward Arnold Ltd.

Kennedy, X.J. (1979) Literature: An Introduction to Fiction, Poetry and Drama. 2nd Edition. Boston: Little Brown and Company.

Kernan, A.B. (1963) Character and Conflict. New York: Harcourt, Brace and World, Inc.

Kezilahabi, E. (1976) Ushairi wa Shaaban Robert. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kiango, S.D. (1973) 'Maendeleo ya Michezo ya Kuigiza' katika Kioo cha Lugha. Dar es Salaam: Toleo la III, Chama cha Kiswahili.

Knappert, J. (1967) Traditional Swahili Poetry. Leiden: E.J. Brill.

Kuhenga, C. (1977) Tamathali za Usemi. Nairobi: East African Literature Bureau.

Leonard, J. (1990) Naming in Paradise: Milton and the Language of Adam and Eve. Oxford Clarendon Press.

Loewenstein, D. (1990) Milton and the Drama of History. New York: Cambridge University Press.

Lucy, S. (1980) William Shakespeare: Julius Caeser. Beirut: Longman York Press.

Massamba, D.P.B. (1983) 'Utunzi wa Ushairi wa Kiswahili' katika FASIHI: Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III. Dar es Salaam: TUKI.

Masoko, D.L.W. (mh. 1984) 'Msamiati ya Muda ya Fasihi' katika Mulika Na. 16. Dar es Salaam: TUKI.

Matteru, M.L. (1975) 'Sauti ya Dhiki' katika Abdalla (mh.) Mulika Na. 7. Dar es Salaam : TUKI.

____________ (1983) "Fasihi Simulizi na Uandishi wa Kiswahili", Katika Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III Fasihi, TUKI, Dar es Salaam.

Mnyampala, M. (1980) Diwani ya Mnyampala. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Mohammed, S.A. (1990) Mbinu na Mazoezi ya Ushairi. Nairobi: Evans Brothers Ltd.

____________ (1977) 'Fani katika Sauti ya Dhiki' katika Honero (mh.), Mulika Na. 11. Dar es Salaam: TUKI.

____________ (1992) " Fasihi", Mswada wa Kitabu Kisichochapishwa.

Msokile, M. (1993) Misingi ya Uhakiki wa Fasihi. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Muhando, P. & Balisidya, M. (1976) Fasihi na Sanaa za Maonyesho. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Muir, K. (1971) Shakespeare Survey Na. 24. London: Cambridge University Press.

Mwita, S.M. (1994) "Tamthilia mbili za Ibrahim Hussein: Arusi na Kwenye Ukingo wa Thim", Tasnifu isiyochapishwa ya M.Phil., Chuo Kikuu cha Moi.

Nassir, A. (1971) Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa. Nairobi: Oxford University Press.

Needlands, J. (1984) Making Sense of Drama: A Guide to Classroom Practice. Heinemann Educational Books Ltd.

Nyerere, J.K. (1970) Mabepari wa Venisi. Nairobi: East African Publishing House.

O.U.P. & TUKI. (1981) Kamusi Sanifu ya Kiswahili. Nairobi: Oxford University Press.

Peck, J. & Coyle, P. (1984) How to Study Literature: Literary Terms and Criticisms. Macmillan Educational Books.

Perrine, L. (1988) Literature: Structure, Sound and Sense. 5th Edition, New York: Harcourt Brace Jovanovich, Inc.

Pomorska, K. & Rudy (eds. 1985) Roman Jakobson: Verbal Art, Verbal Sign, Verbal Time. Oxford: Basil Blackwell Publishers Ltd.

Reinart, O. (1970) Classic Through Modern Drama: An Introductory Anthology. Boston: Little, Brown and Company.

Rohrberger, M. & Woods (1971) Reading and Writing About Literature. New York: Random House, Inc.

Rowe, K.T. (1960) A Theatre in Your Head. New York: Funk and Wagnalls Company.

Scholes, R. (ed. 1982) Elements of Literature. 3rd Edition. New York: Oxford University Press.

Scholes, R. (1974) Structuralism in Literature: An Introduction. New Haven: Yale University Press.

____________ (1990) 'Towards a Semiotics of Literature' in Walder, D. (ed) Literature in the Modern World. New York: Oxford University Press.

Senkoro, F.E.M. (1988) Ushairi: Nadharia na Tahakiki. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

____________ (1987) Fasihi na Jamii. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Shackford, M.H. (1960) Shakespeare, Sophocles: Dramatic Themes and Modes. New Haven: United Printing Services, Inc.

Shariff, I.N. (1991) 'Islam and Secularity in Swahili Literature: An Overview' in Hurrow (ed.) Faces of Islam in African Literature, Portsmouth: Heinemann Educational Books, Inc.

Stina, I. (1971) " 'More Pregnantly than Words': Some Uses and Limitations of Visual Symbolism" in Muir, K. (ed) Shakespeare Survey No. 24. London: Camdridge University Press.

Syambo, B. & Mazrui, A. (1993) Uchambuzi wa Fasihi. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Topan, F.M. (1971) Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili. Nairobi: Oxford University Press.

Walder, D. (ed. 1990) Literature in the Modern World. New York: Oxford University Press.

Wallah, W. (1988) Malenga wa Ziwa Kuu. Nairobi: Heinemann Kenya Ltd.

Waugh, L. (1985) 'The Poetic Function and the Nature of Language' in Pomorska & Rudy (eds.) Roman Jakobson: Verbal Art, Verbal Sign, Verbal Time. Oxford: Basil Blackwell Publishers Ltd.

Webster, R. (1990) Studying Literary Theory: An Introduction. New York: Routledge, Chapman and Hall, Inc.

## KIAMBATISHO I
## MWONGOZO WA MAJADILIANO

Katika utafiti huu, tulikuwa na maswali yaliyonuiwa kutekeleza madhumuni yetu ya utafiti. Maswali haya yaligawanywa mara mbili. Kwanza, tulikuwa na maswali yaliyojaribu kututolea mwanga juu ya uwezo wa ushairi wa kijadi katika kujadili maudhui yoyote ile. Pili, tulikuwa na maswali yaliyogusia eneo la drama na maonyesho kwa ujumla. Katika kuyatimiza hayo, tuliwasaili wataalamu wa maeneo hayo mawili, yaani ya ushairi na drama. Hapa chini tumeonyesha mgawanyo huo wa eneo na wataalamu waliohusika. Mahojiano haya yalifanyika baina ya mwezi wa Machi na Agosti, 1994.

Sehemu A: Ushairi

Maswali;

1. Ushairi, unavyofahamika, ni utanzu mgumu hasa katika kusomwa na kueleweka. Unafikiri ni jambo gani linaloufanya utanzu huo uonekane kuwa mgumu?
2. Kwa maoni yako ungesisitiza mambo, au maswala, gani muhimu katika utunzi na usomaji wa mashairi? (fani na maudhui)
3. Ungetoa maoni yapi kuhusiana na ushairi wa kijadi, hususani ushairi unaozingatia vina na urari wa mizani? Unafikiria kwamba vina na mizani huleta pingamizi katika utungaji wa mashairi?

Waliohojiwa;

1. Bw. Mahiri Mwita: Mhadhiri, Chuo Kikuu cha Egerton, Idara ya Lugha na Isimu.
2. Bw. James O. Ogolla: Mhadhiri, Chuo Kikuu cha Egerton, Idara ya Lugha na Isimu.
3. Nassoro 'Zoa' Mwamzandi: Mshairi na mwigizaji maarufu.

Sehemu B: Drama na Maonyesho

Maswali;

1. Abdilatif Abdalla ni mshairi maarufu anayefuata kanuni za kijadi katika utunzi wake wa mashairi. Baadhi ya kazi zake ni kama vile Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa na Sauti ya Dhiki. Baadhi ya wahakiki waliozisoma tungo zake wamedai kwamba tungo hizo zina uwezo wa kuonekana zikitendeka kwenye bongo la msomaji. Ni mambo gani yaliyowafanya waseme hivyo?
2. Ni mbinu zipi za kimaonyesho zinazohitaji kuzingatiwa ili kazi yoyote iweze kuonekana ikitendeka au ikiigizwa kwenye bongo la mtu?
3. Unafikiri ipo njia maalum ya kuzisoma tungo hizo ili msomaji apate kuziona zikiigizwa?
4. Mbinu hizo za kimaonyesho zinamsaidia vipi msomaji wa tungo hizi hasa katika kuuelewa ujumbe husika?
5. Abdilatif ana ujumbe gani kwa wasomaji na washairi wengine kwa jumla hasa tukizingatia maoni kuwa ushairi wa kijadi unasisitiza vina na urari wa mizani tu?

Waliohojiwa;

1. Bi. Clara Momanyi: Mhadhiri, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika.
2. Bw. Matti: Mhadhiri, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Idara ya

Kiswahili na Lugha za Kiafrika.
3. Bw. Yusuf Maitaria: Mhadhiri, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika.
4. Bw. Mahiri Mwita: Mhadhiri, Chuo Kikuu cha Egerton, Idara ya Lugha na Isimu.

## KIAMBATISHO II

## MUHTASARI WA MATOKEO YA MAJADILIANO

Kutokana na mjadala wetu maswala yafuatayo yalijitokeza.

Sehemu A: Ushairi

1. Ilidhihirika kuwa ushairi wa kijadi hauna pingamizi zozote katika utungaji wa mashairi. Wazo hili linategemea ustadi wa mshairi husika. Ustadi, au uanagenzi, wa mshairi husika katika kuiteua fani sadifu pamoja na maudhui husika, ndiyo mambo muhimu yanayoujenga, au kuumbua, ushairi wa kijadi. Ni msuko huu wa vipengele hivi vya fani na maudhui ambavyo vinaupatia ushairi sifa ya kuwa mgumu.

Sehemu B: Drama na Maonyesho

1. Kwa kuzingatia uwezekano wa kuonekana kwa tungo za Abdilatif kwenye bongo la akili za wasomaji, kulikuwa na mitazamo miwili. Kwanza, sifa za ushairi kama utanzu wa kifasihi. Sifa iliyotia fora ilikuwa ni taswira au lugha ya picha. Pili, ni rai za kimaigizo ambazo zilisisitiza kudhihirika kwa mzunguko wa utatu katika maigizo husika. Mzunguko huo ni ule wa kuwepo kwa jukwaa, hadhira na waigizaji (wahusika) katika matini inayoshughulikiwa. Maoni haya ndiyo tuliyoyatumia katika kuziangalia matini za Abdilatif kama ushairi, na kisha kama maigizo.
2. Mwisho ni maoni ya jinsi nafasi ya mwanamke inavyojitokeza katika Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa. Maoni yaliyotolewa yaliuona utenzi huu kama kiwakilisho cha kugandamizwa kwa mwanamke.

UNIVERSITY LIBRARY